ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1. Mhe. Ali Abdalla Ali	Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini.
2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni.
3. Mhe. Mgeni Hassan Juma	Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake.
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais.
5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani.
6. Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais.
7. Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/Jimbo la Tumbatu.
8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais.
9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais.
10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
11. Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.
12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa na Rais.
13.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais.
14.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais.
15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni.
16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge.
17.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/\Jimbo la Jang'ombe.
18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara,Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni.
19.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando.
20.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi

	Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi.
21.Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni.
22.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole.
24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka.
25. Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake.
26.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais.
27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake.
28.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi.
29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara,Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni.
30.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae.
31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake.
32.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu.
33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
35.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
36.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
37.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
40.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake

43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
44.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
45.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
46.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
47.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
48.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
49.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
53.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
54.Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Jimbo la Kiembesamaki
55.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
56.Mhe. Marina Joel Thomas	Kuteuliwa na Rais
57.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando)	Jimbo la Mkwajuni
58.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma	Jimbo la Bumbwini
59.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
60.Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohamemdali	Jimbo la Uzini
61.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi	Jimbo la Chambani
62.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
63.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
65.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
66.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
67.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
68.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
69.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
70.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi

71.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
72.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
75.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
76.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
77.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake
Ndugu Yahya Khamis Hamad	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Ishirini - Tarehe 12 Juni, 2014

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 55

Ukweli Kuhusu Kero za Muungano

Mhe. Saleh Nassor Juma - Aliuliza:-

Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye pia ni Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalum la Katiba, akiwa katika Bunge la Katiba aliwaambia Wajumbe wa Bunge hilo kwamba SMT imejitahidi sana kutatua kero za Muungano kwani imebakisha kero moja tu, kinyume na kauli ya Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete alisema kwamba zimebakia kero tano za Muungano.

Je, ukweli uko wapi katika kauli mbili hizo zilizotofautiana.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Saleh Nassor Juma Mwakilishi wangu wa Jimbo la Wawi swali lake namba 55 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kiutaratibu katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Rais anakuwa na kauli ya mwisho katika mambo yote ya serikali. Hivyo hakuna Waziri wa Serikali atakayekuwa na kauli tofauti mbele ya Mhe. Rais.

Mhe. Spika, kauli ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalum la Katiba kauli yake ya kuwaambia Wajumbe wa Bunge la Katiba kuwa Serikali ya Muungano wa Tanzania imejitahidi sana kutatua kero za Muungano na kubakisha kero moja hakuwa na nia ya kutofautiana na Mhe. Rais bali huu ulikuwa ni muono wake katika hatua zinazoendelea katika kuzipatia ufumbuzi kero za muungano, kutokana na mambo yaliyobakia kwa kiasi kikubwa yalihitaji majibu ya kikatiba ambao mchakato wake unaendelea.

Mhe. Spika, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alizitaja kero sita ambazo hazijapata ufumbuzi kwa maana ya kwamba bado hazijaondolewa kwenye orodha ya kero za Muungano kwa kusainiwa rasmi. Ingawa kero hizo zipo katika hatua nzuri ya kumalizika. Hivyo kauli ya Mhe. Rais ndio kauli ya mwisho na hakuna Waziri anayeweza kutofautiana na kauli hiyo.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri mpiga kura wangu hapa Mhe. Mohamed Aboud naomba niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Mawaziri wote wanaingia katika vikao vya Baraza la Mawaziri, ambapo Mhe. Rais huwa anaingia kwa mujibu wa ratiba yake huwa analihutubia kila baada ya kipindi.

Na kwa kuwa sisi wafuasi wao kioo chetu zaidi ni Baraza la Mawaziri la hapa na lile la Jamhuri ya Muungano, Mhe. Waziri huoni kwamba Waziri kutoa kauli iliyotofautiana na Mhe. Rais ni kutuyumbisha sisi wafuasi wenu katika hili. Na kama ni kutuyumbisha, hamuoni kama baadhi ya mawaziri hamko makini katika vikao vya Baraza la Mawaziri.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, ningeomba la pale mwisho alirudie sikumsikia vizuri.

Mhe. Spika: Mheshimiwa rudia swali hasa sehemu ya mwisho.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Hili la mwisho nilisema kwamba kwa sababu Mawaziri mnahudhuria siku zote katika vikao vya Baraza la Mawaziri, ambapo Mwenyekiti wenu ni Mhe. Rais, kutoa kauli tofauti baina ya Rais na Mawaziri wake, hamuoni kama ni kutuyumbisha sisi wafuasi wenu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kwamba huo ulikuwa muono wake yeye Mhe. Waziri na hakuwa na nia ya kutafautiana na Mhe. Rais ama kuyumbisha wananchi bali huo ni muono wake, lakini kama nilivyosema kwamba kauli ya mwisho ni ya Mhe. Rais.

Na mtazamo ule unatokana na Mhe. Waziri kwamba tayari mambo mengi ya muungano yameshughulikiwa na yale ambayo sasa yanahitaji majibu ya kikatiba ndio alikuwa na mtazamo kwamba yatapata ufumbuzi kupitia Katiba, ndio akaja na kauli ile, lakini nirudie tena kwamba kauli ya Mhe. Rais ndio kauli ya mwisho, na naamini sote tutakubaliana na kauli hiyo.

Napenda tu kumshauri Mhe. Mwakilishi kwa kuwa yeye anaye Mbunge wake ambaye wanaelewana sana Mhe. Hamad Rashid Mohammed angeweza tu kumpa swali hili ili ukalipata jibu kutoka kinywa cha mwenyewe Mhe. Waziri. Ahsante sana. *(Makofi).*

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Rais alipokuwa akiomba kura ili tumchague Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalum la Katiba miongoni mwa mambo yaliyotushawishi sana *statement* yake ya kuonesha juhudi yake aliyoifanya katika kutatua kero za muungano mpaka ikabakia moja tulishawishika sana. Na kwa msingi huo tukamchagua kuwa Makamu Mwenyekiti.

Sasa kwa kuwa *statement* yake hiyo inaonesha haina ukweli, je Mhe. Waziri huoni haja ya kuungana na mimi kwamba huyu mtu anapaswa kujiuzulu nafasi ile.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwanza Mhe. Spika, sioni kwamba Mhe. Waziri angepaswa kujiuzulu kwa kauli yake ile, kwa sababu kama nilivyosema ule ulikuwa muono wake na ni vizuri zaidi Mhe. Spika, kama nilivyomshauri Mhe. Saleh swali hili ni vyema Waheshimiwa Wawakilishi kupitia Wabunge wao wakawapa hili swali ili wakamuuliza mwenyewe wakaisikia kauli kutoka kinywani mwake je, alikuwa na dhamira gani na alikuwa na madhumuni yepi, ili ukweli ukapatikana Mhe. Spika.

Nam. 37

Ukosefu wa Fedha za Maendeleo kwa Wizara Katika Kipindi cha Robo ya Mwisho ya Bajeti

Mhe. Saleh Nassor Juma (Kny.Mhe. Jaku Hashim Ayoub) - Aliuliza:-

Pamoja na Baraza la Wawakilishi kupitisha makadirio ya fedha kwa Wizara mbali mbali Wakati wa Kikao cha Bajeti kila mwaka, kumekuwa na malalamiko ya Wizara mbali mbali inapofika mwisho wa mwaka, kutofikishiwa fedha hizo kulingana na bajeti, hasa fedha za maendeleo.

(a) Je, tatizo la kutofikishwa fedha hizo ni nini.

(b) Je, tatizo hili litamalizwa lini.

Mhe. Waziri wa Fedha - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa heshima kubwa kabla ya kujibu swali la Mhe. Jaku Hashim Ayoub Mwakilishi wa wananchi Jimbo la Muyuni lenye vifungu (a) na (b) kwanza naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, uchumi wa Zanzibar bado ni mchanga hivyo kupelekea mapato ya Serikali kuwa madogo na kuifanya Serikali kuendesha Bajeti yake kwa utaratibu wa fedha taslim *(Cash budget*). Aidha, utekelezaji wa bajeti yetu unategemea mambo mbali mbali yakiwemo yafuatayo:-

(i) Mapato yanayokusanywa (kutoka nje na ndani).

(ii) Kiwango cha matumizi ya serikali ya lazima na ya mwanzo kulipwa kama vile mishahara, pencheni, huduma za lazima za hospitali na vyuo vya mafunzo.

(iii) Matumizi ya mambo ya dharura na ya haraka.

(iv) Mchango wa Serikali katika miradi ya maendeleo, na;

(v) Matumizi ya uendeshaji wa shughuli za serikali.

Mhe. Spika, licha ya juhudi zinazochukuliwa za ukusanyaji wa mapato, bado kasi ya mahitaji ya Serikali inaendelea kukua na hivyo kupelekea matumizi kuwa makubwa siku hadi siku ukilinganisha na mapato yanayopatikana.

Mhe. Spika, misaada kutoka kwa washirika wa maendeleo inaendelea kupungua siku hadi siku na hii pia hupelekea Serikali kuwa na mapungufu katika mipango yake ya matumizi.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kumjibu Mhe. Jaku swali lake kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, kuchelewa au kutokupatikana kwa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Serikali kwa wakati, kunatokana zaidi na uhaba wa mapato kulingana na mahitaji yanayohitajika kwa wakati ule.

(b) Mhe. Spika, tatizo hili litamalizika pale wananchi wote watakapoamua kujituma kwa ukamilifu kwa lengo la kukuza uchumi wa Zanzibar na kutoa uwezo wa mapato zaidi kwa Serikali yatakayoweza kukidhi mahitaji ya wananchi.

Aidha suala la uzazi wa mpango ni muhimu kupewa kipaumbele na kutekelezwa kwa ukamilifu, hii itasaidia sana kupunguza kasi ya ongezeko la idadi ya watu na hivyo kupunguza kasi ya mahitaji.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Waziri wetu katika masuala ya fedha Mhe. Omar Yussuf Mzee naomba niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa uchumi wa nchi nyingi hasa hizi zetu ndogo ndogo na hizi zilioko huku Kusini mwa jangwa la Sahara zinategemea zaidi afya ya walipa kodi wake.

Kwa hivyo mlipa kodi mwenye afya ndiye anayelipa kodi vizuri zaidi na kupanua uchumi. Je, Mhe. Waziri huoni wewe kwamba kuendelea kuwawekea bajeti ndogo Wizara ya Afya huoni kwamba utateremsha kwa kiasi kikubwa pato la nchi kwa sababu watakuwa wagonjwa na watakuwa hawawezi kufanya kazi wakalipa kodi. *That is* (a).

Kwa kuwa nayo Wizara ya Elimu vile vile shilingi ni ndogo halafu hamuipi fedha wakati tena fedha zinakuwa ndogo. Je, hamuoni kuendelea kuwanyima fedha Wizara ya Elimu ni kuongeza ngumbaru na watu waliokosa elimu katika nchi yetu.

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Spika, ukitizama vitabu vyetu vya bajeti katika miaka 4 iliyopita utazame bajeti ya kila Wizara bajeti ya *recurrent;* yaani bajeti ya kawaida na bajeti ya maendeleo, Wizara tatu hizi zinaongoza.

Wizara ya Miundombinu, Wizara ya Afya na Wizara ya Elimu haya siyo maneno yangu ni maneno ya bajeti inayopitishwa na Baraza lako Tukufu. Kwa maana hiyo serikali inatilia maanani kwamba afya ya mwananchi ni muhimu katika kukuza uchumi, na elimu ya mwananchi ni muhimu katika kukuza uchumi. Vile vile miundombinu nayo ni muhimu katika kukuza uchumi. Kwa maana hiyo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inayoongozwa na Dr. Ali Mohamed Shein, itaendelea kutoa kipaumbele sekta hizi muhimu.

Mhe. Mahmoud Thabit Kombo: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza ninamshukuru sana Mhe. Waziri kwa majibu yake yaliyokuwa mahiri sana na yenye ufafanuzi wa kina. Kuna usemi mmoja wa Kiingereza wa zamani sana unasema "*there is no power of spending without power of earning".* Yaani hakuna nguvu za kutumia bila ya nguvu za kuzalisha kwanza. Na huwezi kutumia kabla ya kuzalisha.

Sasa Mhe. Spika, swali langu liko hapa, katika vitabu vya bajeti tumekuwa mara nyingi tunaona sehemu ya kutumia zaidi ingawa ni Makadirio ya Mapato na Matumizi na mara nyingi mapato inakuwa sehemu ndogo yaani haiko *itemize.* Pia katika muundo wa Wizara maeneo makubwa ni ya kutumia zaidi kuliko maeneo yaliyowekwa kwa ajili ya kufanya ubunifu wa kuzalisha zaidi. Mfano nitatoa *fiscal policy unit* ndio inashughulikia mambo ya kuzalisha.

Je, Mhe. Waziri anaweza kunambia kwamba wanapanga kitu gani baadae kuweka *department* ambayo itakuwa inabuni kuzalisha zaidi kabla ya kupanga kutumia. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Spika, kwanza ninakubaliana naye mia kwa mia kwamba mapato yana umuhimu mkubwa katika kupanga mipango yoyote ile ya nchi hata mipango ya kaya, lakini vile vile nataka nimwambie kwamba serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeliona hilo tatizo ambalo analolizungumza yeye. Hivi sasa tunataka kuunda kitengo chini ya Wizara ya Fedha ambacho kitasaidia kufanya uchambuzi wa kodi na kuielekeza serikali katika kutafuta nyanja mpya za kodi pamoja na za kuinua uchumi.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri lakini na mimi nataka kumuuliza swali la nyongeza lenye (a) na (b).

Mhe. Spika, kwa kuwa lengo la serikali ni kutimiza malengo yake iliyojipangia kuziingizia fedha Wizara nusu au robo, kuzifanya Wizara zikashindwa kuendeleza miradi iliyojipangia ili kupeleka maendeleo kwa wananchi.

Pili, kwa kuwa uchumi wetu ni mdogo, ni kwa nini tunapanga malengo makubwa ambayo tunapozitaja fedha hapa kwa asiyefahamu anaweza akaona fedha hizo zinapatikana na zinatumika. Je ni kwa nini tunapanga malengo hayo makubwa na ambapo hatuwezi kuyafikia.

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Spika, kwanza nataka akubaliane na mimi kupanga ni kuchagua, na serikali huwa inachagua halafu inapanga inaleta Baraza la Wawakilishi na Baraza linaidhinisha tunakwenda kutekeleza. Tatizo tulilonalo ni moja tu mipango yetu tunayoipanga utekelezaji wake unategemea vile vile fedha kutoka nje, laiti ingekuwa utekelezaji wake unategemea fedha za ndani tu nadhani tungeliweza kutekeleza hata asilimia 90. Lakini tunategemea zaidi fedha kutoka nje na ninayo takwimu hapa Mhe. Spika nataka nizitoe kidogo kwa faida ya Wajumbe wako.

Mwaka 2010/2011 mapato yetu ya ndani yameweza kufikia asilimia 106 ya makadirio, lakini mapato ya nje tuliyokuwa tukiyategemea yalifikia asilimia 64 ya makadirio.

Mwaka 2011/2012 mapato yetu ya ndani yalifikia asilimia 99 ya makusanyo lakini mapato ya nje tuliyokuwa tukiyategemea yalifikia asilimia 63.9.

Mwaka 2012/2013 mapato yetu ya ndani yalifikia asilimia 91 ya makadirio. Mapato yetu tuliyokuwa tunayategemea kutoka nje yalifikia asilimia 68 tu, hivi sasa mwaka huu tunaokwenda nao. Katika miezi sita mapato yetu ya ndani yamefikia asilimia 87 miezi kumi na moja mpaka Mei, lakini mapato ya nje tuliyokuwa tukiyategemea yamefikia asilimia 57.

Kwa hivyo, mategemeo yetu ni kwamba tunapanga kutegemeana na mapato kutoka nje; cha muhimu hapa ni kuanza taratibu kujitegemea tuondokane na utegemezi. Kama nilivyojibu swali langu kuondokana na utegemezi kutahitaji mambo ya msingi. Kwanza kujituma Wazanzibari sote tujitume lakini vile vile uzazi wa mpango tuupe kipaumbele,

kwa sababu ongezeko la watu ni kubwa mno. Zanzibar leo kila mwaka Mhe. Spika tunaongezeka asilimia 2.8 sawa na watu 40,000 kwa mwaka wanaongezeka. Maongezeko hayo yanaongeza gharama kwa sekta zote, sekta ya elimu, sekta ya afya, sekta ya maji kila mwaka. Kwa hivyo, uzazi wa mpango akina mama na akina baba tuupe kipaumbele.

Nam. 56

Ujenzi wa Barabara ya Ole-Kengeja na Upanuzi wa Uwanja wa Ndege

Mhe. Saleh Nassor Juma - Aliuliza:-

Hivi karibuni kumekuwa na taarifa za ujenzi wa barabara ya Ole - Kengeja, sambamba na upanuzi wa ujenzi wa uwanja wa ndege wa Pemba.

(a) Je, dhamira hizo za serikali bado zipo.

(b) Kama zipo miradi hiyo itaanza lini na kumalizika lini.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:- Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Wawi swali lake Nam. 56 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, dhamira ya serikali ya kutekeleza miradi hiyo ipo.

b) Mhe. Spika, kwa taarifa ni kuwa barabara ya Ole/Kengeja yenye urefu wa kilomita 35 itajengwa kwa kutumia fedha za mkopo kutoka mfuko wa nchi zenye kusafirisha mafuta kwa wingi duniani na fedha za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

   Jumla ya dola za Kimarekani milioni 12 zinatarajiwa kutumika ikiwa dola milioni 11 ni mkopo na dola milioni 1 ni mchango wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika mradi huo. Tayari Mhandisi Mshauri ameanza kazi rasmi kwa kushirikiana na wataalamu wa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano.

   Kazi za upimaji wa barabara (*survey*) zinaendelea ambapo eneo lenye urefu wa kilomita 11 tayari limeshapimwa. Aidha, tathmini ya nyumba na vipando vya wananchi vitakavyoathirika wakati wa ujenzi itafanyika hivi karibuni.

Mhe. Spika, wizara pia imeanza taratibu za ununuzi wa baadhi ya vifaa na mitambo itakayotumika katika ujenzi wa barabara hiyo. Ujenzi (*physical works*) utaanza rasmi mara tu baada ya serikali kukamilisha taratibu za uingizwaji wa fedha na kupatikana kwa fedha za kuanzia. Serikali iko katika hatua za mwisho kukamilisha taratibu za upatikanaji wa fedha za mwanzo (*first disbursement*) ambazo ni dola za Kimarekani 465,000. Ujenzi wa barabara hiyo utafanywa na Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara na unatarajiwa kuchukua kipindi cha miaka mitatu kukamilika kwake.

Mhe. Spika, kwa upande wa Mradi wa Uendelezaji wa Uwanja wa Ndege wa Pemba malengo ya serikali ni kuufanya uwanja huo kuwa wenye hadhi ya kikanda. Wizara mwanzoni ilikusudia kutekeleza mradi huu kwa kupitia Jumuiya ya Afrika Mashariki na baadae serikali ilitenga fedha kupitia miradi ya maendeleo. Hata hivyo, utekelezaji wake kupitia vyanzo viwili hivyo umekuwa mgumu kutokana na ukosefu wa fedha.

Mhe. Spika, kutokana na hivyo, serikali inaendelea kuwasiliana na Washirika wa Maendeleo ili kupata ufadhili au mkopo wa kutekeleza mradi huo. Hivi karibuni wenzetu wa Uturuki wameonesha nia ya kutupatia mkopo kupitia *Exim Bank* ya Uturuki, mazungumzo hayo yamepelekea kufanywa kwa upembuzi yakinifu wa awali na ripoti kuwasilishwa serikalini kwa ajili ya kupitiwa na kutolewa maoni na taasisi husika. Aidha, serikali inatafuta mtaalamu wa kujitegemea kwa ajili ya kuipitia na kutoa ushauri muafaka kwa serikali.

Mhe. Spika, kulingana na ripoti hiyo muda wa ujenzi unakadiriwa kuwa ni miaka miwili baada ya kazi kuanza. Uimarishaji wa kiwanja cha ndege hicho utajumuisha kuongezwa urefu wa njia ya kutulia na kurukia ndege kutoka urefu uliopo hivi sasa wa mita 1500 hadi mita 2500.

Kuongeza upana wa eneo la kuegesha ndege kutoka mita za mraba 13,500 hadi kufikia mita za mraba 24,000. Upanuzi wa njia ya kupita ndege kutoka mita za mraba 14,000 hadi mita 27,000. Ujenzi wa jengo jipya la abiria lenye ukubwa wa mita za mraba 2240. Ujenzi wa uzio kuzunguka uwanja mzima, uwekaji wa mfumo wa usalama wa moto, uwekaji wa vifaa vya usalama, uwekaji wa taa za kuongozea ndege wakati wa kutua na kuruka, ukarabati wa jengo la abiria, la sasa kuwa ghala ya mizigo na sehemu ya Zimamoto. Kiwango cha gharama kwa ajili ya kazi hiyo bado hakijajulikana kwa vile mazungumzo bado hayajakamilika.

Mhe. Spika, masharti ya awali ya mkopo huu ni kuwa mjenzi ni lazima atoke nchini Uturuki pamoja na asilimia 10 ya wafanyakazi wake. Aidha, mkopo huo utatakiwa kulipwa ndani ya miaka 10 ambapo malipo yake yataanza miezi sita baada ya kukamilika kwa ujenzi husika.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu ya maneno tu aliyoyatoa Mhe. Naibu Waziri naomba niulize swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa barabara ni kiungo baina ya wananchi, wakulima, wajasiriamali kutoka sehemu moja hadi nyengine. Na kwa kuwa miaka ya nyuma aliyekuwa Katibu Mkuu wa Afro Shirazi Mhe. Mzee Thabit Kombo Jecha alitoa kauli mbiu ya Afro Shirazi inayosema kwamba maneno yawe mafupi lakini vitendo viwe virefu. Na kwa kuwa huu ni karibu mwaka wa sita barabara ya Ole/Kengeja itajengwa na hadi leo hii haijajengwa zaidi ni maneno tu.

a) Je, huoni Mhe. Naibu Waziri kuendelea kusema maneno na kuwaacha wajasiriamali wa Mwambe, Mtambile, Kengeja wakikosa kuuza biashara zao za mikungu, vyetezo katika Mji wa Wete huoni ni kuongeza umasikini katika nchi.

b) Kuhusiana na suala zima hili la ujenzi wa Uwanja wa Ndege vile vile limekuwa la siku nyingi kiasi ambacho tunapata shida. Kuna watu wana wake wawili mmoja yuko Pemba na mmoja yuko Unguja na wanapenda kwenda zamu wakati wa usiku na ndege pale hazipati kutua usiku. Aidha, Rais wetu huwa anataka vile vile kuja kutuangalia wananchi wake wakati wa usiku hapati. Je, huoni kwa kuendelea kutokijenga kile kiwanja cha Pemba na kuendelea kupiga piga maneno kama unavyopiga hivi sasa Mhe. Naibu Waziri si kuendelea kuwanyima raha wale wenye wake Pemba na Unguja na Mhe. Rais kumnyima raha ya kuja kutuona sisi wananchi wake kule Pemba usiku, huoni kwamba kuna siku nyengine anataka kufutari pale Pemba hapati.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, ni kweli kwamba barabara hii imekuwa mdomoni mwa serikali kwa muda mrefu, lakini kama atasoma vizuri kitabu chetu, na kama atakuwa amenisikiliza vizuri maelezo yangu tumeeleza kwamba kikwazo kikubwa ilikuwa ni upatikanaji wa fedha za kuweza kukidhi ujenzi wa barabara hiyo. Barabara hii ina urefu wa kilomita 35 kwa bei ya soko hivi sasa ukijenga kilomita 1 gharama ya chini ni shilingi 850,000,000 kujenga kwa kiwango cha lami.

Ukizichukua fedha za ufadhili kutoka *IFAD* milioni 11 ukizigawa kwa gharama hiyo ya chini ya milioni 850,000,000 kwa kilomita moja huwezi kujenga barabara hiyo. Wafadhili hawa waliitaka serikali kuongezea fedha za ziada ili kuweza kujenga kwa kiwango cha lami, serikalini hatukuwa na fedha za kutosha. Sasa kwa muda mrefu serikali ilikuwa ikifanya mazungumzo na kuwaomba wenzetu hawa waweze kuongeza kiwango cha fedha ili tuweze kutekeleza mradi huo. Kwa bahati mbaya wenzetu na wao wamekuwa wagumu.

Kwa hiyo, mazungumzo na serikali tumefikia pahali tumekubaliana kwamba kiwango hiki hiki cha milioni 11 serikali itaongeza milioni 1 tutajenga kwa kutumia wataalamu wetu wa ndani (*UUB*). Makubaliano ya serikali na wafadhili hawa ni kuona kwamba fedha hizo zitumike kwa kununulia vifaa vya kuweza kuwapa nguvu *UUB* ili waweze kutekeleza mradi huu, zitumike kwa ajili ya kununulia *material;* kokoto, lami na nyenginezo. Lakini pia kuwepo na *incentives* kwa wafanyakazi wetu watakaoshiriki katika ujenzi wa barabara hiyo.

Kwa hiyo, nikutoe hofu Mhe. Saleh kwamba ni kweli imesemwa muda mrefu lakini kikwazo chetu ni fedha, baada ya kutathmini vizuri tumeona milioni 11 tukiongeza na milioni 1 dola za kwetu SMZ barabara hii kwa kutumia wataalamu wa ndani tutaijenga. Naomba sana nikutoe hofu kwamba azma ya serikali ipo na jambo hili litatengenea,

na hatua iliyopo hivi sasa kama tulivyoeleza kwamba kilomita 11 tayari imeshafanyiwa *survey* katika bajeti yetu tumeomba milioni 500,000,000 mwaka huu tupate kwa ajili ya kuanza taratibu za ujenzi huu wa barabara ili wananchi uliowataja na maeneo yote waweze kuondokana na usumbufu wanaoupata, kwani sote tunatambua uimarishaji wa miundombinu ndiyo namna ya kushajihisha uchumi wa nchi yetu uweze kukua vizuri zaidi.

Mhe. Spika, suala la pili lilielekezwa kwamba kuna watu wanashindwa kupanga zamu kati ya Unguja na Pemba kwa sababu ya ndege ya usiku. Nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba mradi huu nao umesemwa muda mrefu, hatua ya kwanza tulitegemea kwamba wenzetu wa Jumuiya ya *East Africa* wangetusaidia kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu, haikuwa hivyo.

SMZ tuliomba fedha kwa ajili ya kufanya jambo hili nalo tukashindwa kupata fedha za kutosha tukaweza kuya-*locate* maeneo mengine ikiwa ni pamoja na kwenda kulipa madeni ya wakandarasi wanaotufanyia kazi. Lakini hatua tuliyofikia ni kwamba tayari mazungumzo yetu sisi na wenzetu wa Uturuki, na wao wamechukua jitihada sasa wameshaanza kufanya *study*, na *study* ya awali wameshatupatia sisi serikalini. Wajibu wetu kama serikali kupitia taasisi zetu kutoa michango yetu huku tukiendelea na utaratibu wa kupata *independent surveyor* atakayejiridhisha na kuipitia *study* ile, baadae kutupa zile *comments* zake tumrejeshee mfanyaji *study*. Baada ya kuona kwamba *study* haina matatizo tutaendelea na taratibu za mbele ikiwa ni pamoja na ujenzi na taratibu za kukamilisha utaratibu wa kuweza kujenga uwanja huu.

Matarajio uwanja huu ukijengwa kama tulivyoeleza katika majibu mama kwamba maeneo ya maegesho, barabara ya kurukia ndege, jengo, huduma za zima moto na nyengine zote nazo zitakuwa zimeimarika. Kwa hiyo, Mhe. Mwakilishi ni kweli kwamba mradi huu umechukua muda mrefu, lakini kikwazo ilikuwa ni fedha za kuweza kutekelezea, hivi sasa tuko sehemu nzuri ya mazungumzo ambapo tunaamini mradi huu nao utakwamuka ili kuweza kutimiza azma ya serikali.

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri nataka vile vile niongezee kwa kumpa taarifa tu Mhe. Saleh baba yangu huyu kama ifuatavyo:-

Hatuzungumzii sasa maneno matupu kwa ajili ya Uwanja wa Ndege wa Pemba, sasa hivi Uwanja wa Ndege wa Pemba uko katika hatua za mbali zaidi, hata barua kutoka SMT kwa ajili ya kupata mkopo tayari imeshakwenda katika Benki ya Uturuki. Kwa hivyo, nia yetu ya mwanzo ilikuwa kuongeza *runway* kwa ajili ya utuaji wa ndege kubwa, lakini imeonekana kwamba ile iliyopo sasa hivi haitaweza kuhimili ndege kubwa. Kwa hivyo, nayo vile vile ile iliyopo sasa hivi inabidi ifanyiwe utaratibu wa kuongezwa *layer* ili iweze kutua ndege kubwa. Kwa hivyo, wenzetu hawa Waturuki tayari wameshamaliza, na sisi kwa upande wetu tumeshatoa *intention letter* kupeleka katika Benki ya Uturuki kwa ajili ya kuweza kupata hizo fedha. Nadhani katika muda wowote ule, kwa sababu kama mtakumbuka wenzangu tuliokuwa katika kampeni ile ilikuwa ni moja ya ahadi za Mhe. Rais wa Zanzibar Dk. Ali Mohamed Shein. Kwa hivyo, na sisi tunalifanyia kazi kwa nguvu zetu zote, siyo maneno matupu, namwambia Mhe. Saleh kwamba siyo maneno matupu, hivyo avute subra kama ni kwenda kulala zamu Pemba atalala, hivi karibuni tu atalala.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi kuuliza swali (a) na (b) la nyongeza. Napenda kumuuliza Mhe. Naibu Waziri kwa kuwa mwaka huu wa fedha wizara imekusudia kukamilisha ujenzi wa barabara ya Ole/Kengeja, na kwa kuwa kila bajeti barabara hii inakuwemo kwa kutengenezwa.

a) Je, kwa nini serikali haipangi miradi kiasi kwa mujibu wa fedha kuliko kupanga miradi mingi na ikabakia njiani.

b) Je, utatueleza nini ikiwa barabara hii kwa mwaka huu wa fedha haikumalizia.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, mradi huu serikalini umepangwa kuanza kutekelezwa mwaka huu wa bajeti, lakini kipindi cha kukamilika kwake ni kipindi cha miaka mitatu, kwa hiyo na mwakani Mwenyezi Mungu akitujaalia tutakuja nao tena kuomba fedha kwa ajili ya kuendeleza mradi huo. Kwa hiyo, malengo ya serikali kama utaangalia vizuri bajeti yetu mara hii hatuna miradi mipya ambayo tumeiongeza, miradi yetu ni ile ile tuna *carry on* kwa ajili ya kuomba fedha ili tuweze kutekeleza vizuri na isikwame kama mwaka uliokwisha ambapo kwa sehemu kubwa miradi yetu mipya tulishindwa kuianzisha kutokana na ukosefu wa fedha.

Kwa hiyo, miradi iliyopo hivi sasa huu sio mradi mpya, kwa hiyo tunauanza mwaka huu, mwakani utakuja tena katika kipindi cha miaka mitatu ndiyo kukamilika kwake.

Nam. 83

Tatizo la Watoto Taahira

Mhe. Saleh Nassor Juma (Kny: Mhe. Jaku Hashim Ayoub) – Aliuliza:-

Kwa kuwa tatizo la kuzaliwa kwa watoto taahira au wale waliofanana linaongezeka siku hadi siku na kufanya idadi ya watoto wa aina hiyo kuwa kubwa.

(a) Je, serikali inaweza kueleza tatizo hilo husababishwa na nini.

(b) Je, serikali imewahi kufanya utafiti wowote kuhusiana na tatizo hili.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 83 lenye kifungu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza ningependa kuwafahamisha watu wote kwamba jila la taahira hivi sasa halitumiki, kwani ni la unyanyasaji wa kimaumbile kwa watu wenye ulemavu, na linalotumika sasa ni hilo la watu wenye sura mfanano. Kwa hiyo, kabla sijaanza kueleza mambo, ningeomba kwanza Mwakilishi huyo anayemwakilisha Mhe. Jaku Hashim Ayoub asimame kwanza aombe radhi kwa kutumia jina hilo ambalo sasa halitumiki. Nasubiri. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Naibu Waziri nafikiri hili halina haja ya kuomba radhi ila ilikuwa linahitaji taaluma. Nahisi kwa kiasi fulani umetuelimisha kwamba si sahihi sasa watu ambao wana tatizo hilo kuwaita watu wenye akili taahira. Hiyo sasa ni taaluma unatupa na Wajumbe wanaipokea. Mheshimiwa endelea. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, taaluma inatolewa na watu wote wanajua, kakusudia tu! *(Kicheko)*

Mhe. Spika, watu wenye sura mfanano jina hilo limetokana na muonekano wao, wote kuwa na sura moja hata azaliwe wapi, na jamii ipi, bado wanakuwa wanafanana. Kwa jina la kitaalamu hali hiyo huitwa *"Down's Syndrome" (DS),* jina la Mwana Sayansi mmoja wa Kiingereza aitwae John Langdon Down ambaye ndiye aliyeeleza kwa ukamilifu tatizo hilo kwenye mwaka 1866 ingawa tatizo lilikuwepo zamani.

Mhe. Spika, tatizo hilo linatokana na kuwepo kwa moja ya kinasaba (*DNA*) kiitwacho *"trisomy 21"* chenye kinasaba kimoja cha ziada badala ya mbili za kawaida na kuwa na mpangilio usio sahihi kwa binadamu wa kawaida. Kutokana na ongezeko hilo la kinasaba, watu wanaozaliwa wanakuwa na matatizo mengi ya kimaumbile ukiachilia mbali kufanana.

Tatizo hili linaweza kugundulika kabla ya mimba kutunga kwa kupima wazazi na kuangalia vinasaba vya wazazi *"prenatal Screening"* au kama mimba ishatunga vipimo kama *Ultrasound*, au kutoa maji yanayomzunguka mtoto kwenye fuko la uzazi (*amniocentesis*) vinaweza kugundua matatizo ambayo mtoto aliyeko tumboni.

Pia matatizo haya yapo zaidi kwa wale ambao wanaozaa katika umri mkubwa, lakini pia ni sababu ya mimba nyingi kuharibika.

Mhe. Spika, tatizo hili tafiti nyingi zimeshafanywa na maradhi haya yapo tangu zama za dunia kuundwa, kwa sisi kila daktari analifahamu kwa sababu linasomeshwa katika masomo ya msingi ya udaktari.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, nataka Mhe. Naibu Waziri atuelezee zaidi, kwa sababu naona ametueleza hii *Down's Syndrome* tu, hawa wengine naona hukutueleza au hukujibu hili jengine.

Mhe. Spika: Rudia swali Mheshimiwa.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Kwa kuwa amesema kwamba mbali ya hao *Down's Syndrome* ambao wamefanana na ambalo ndio suala la msingi, alitaka kujua kuongezeka kwa hili tatizo la watu wenye sura mfanano, kwa sasa ongezeko hili linasababishwa na nini.

Mhe. Naibu Waziri: Swali halifahamiki, lakini nitajaribu kumfahamisha. Nimesema katika hili jawabu nililojibu kwamba, hawa watu mbali tu ya kufanana wana na matatizo mengi ikiwemo na hilo la kuwa akili zao kidogo zinakuwa sio nzuri. Sasa labda tu nimpe matatizo ya watu wenye sura mfanano.

1. Wanakuwa na kinga dhaifu ya mwili na kusababisha matatizo mengi ya kiafya.
2. Ukuaji wa mwili kuchelewa na kushindwa kuzungumza vizuri.
3. Tabia zisizokomaa kulingana na umri, uwezo mdogo wa akili kwa kijana mtu mzima ni sawa sawa na mtoto wa miaka 8 au 9, maradhi ya akili, msongo wa mawazo, ugonjwa wa kusahau na kifafa. Nafikiri hapa ndipo penye swali lako kwamba hayo pia yako. lakini sio hivyo tu,
4. Mara nyingi hawa wanakuwa na matatizo ya mtoto wa jicho, presha ya macho na uoni hafifu, mara nyingi wanaishia kuwa vipofu.
5. Kutosikia vizuri, mashikio yanayotoa usaha na maambukizi.
6. Tatizo la tezi la shingo.
7. Moyo wenye tundu, mishipa ya moyo kukomaa, Saratani ya damu.
8. Kuziba pumzi usingizini na kufariki ghafla.
9. Kiungulia, kutopata choo kikawaida na choo kigumu.
10. Kisukari cha kuzaliwa nacho na hakitibiki kwa *insulin*.
11. Nyonga kuchomoka ovyo na matatizo ya uti wa mgongo.
12. Kwa wanawake uzazi wao ni mdogo, ugumba, kumaliza hedhi katika umri mdogo na wengi wao wakipata watoto wanakuwa pia wa mfanano.

Wanaume kukosa kizazi na saratani ya makende. Hayo ndio matatizo waliyonayo watu wa aina hii. Kwa hivyo, wana matatizo mengi kiasi.

Mhe. Mahmoud Thabit Kombo: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali dogo la nyongeza. Watoto hawa wana *facilities* zao pale Skuli ya Jang'ombe, mimi nilibahatika kuwatembelea zaidi ya mara tano pamoja na wataalamu mbali mbali waliotoka nje ambao wanawasaidia watoto wale pale Skuli ya Jong'ombe. Pale wanakaa kwa mchanganyiko wako hao wa *Down's Syndrome*, *Jensen syndrome* na wako wale waliopata taathira ya ubongo, kusikia pamoja na matatizo mengine yanayotokana na maradhi ya malaria. Kwa bahati nzuri Mwalimu Mkuu wao pale alibahatika kwenda mafunzo ya nje kwenda kusomeshwa, mara nyingi kule nje huwa wanaitwa *Mongolians* au *Mongol Children*.

Sasa kwanza kabisa naomba nimuulize je, ameshawahi kukitembelea kituo hiki ambacho kiko chini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Pili, je, kuna mashirikaino yoyote kati ya Wizara ya Afya na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa watoto wale. Kwa sababu watoto wale wako wengi kina Khalfan, Mabrouk, wakati huo Farashuu, watoto wale huwa wanajaaliwa na kitu kimoja cha mapenzi makubwa mno na watu wanaowatembelea. Sasa nilikuwa nataka nimuulize hayo Mhe. Naibu Waziri.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, *facility* hiyo anayoizungumza ya Skuli ya Jang'ombe naifahamu, lakini sijawahi kutembelea, najua watoto wapo maana ni karibu na ninapoishi kwetu, nawaona wakipita lakini mimi kama mimi sijawahi kwenda.

Jina la *Mongolism* nalo lilikuwa linatumika huko nyuma nalo pia sasa hivi halitumiki, kwa sababu wenyewe watu wa Mongolia walikwenda *WHO* kwenda kulikataa rasmi, kweli wanafanana kwa sababu wengi wana macho ya kuvuta na wanafanana nao sana. Kwa hivyo, amri ikatolewa rasmi na ndio hapo lilipokatazwa jina hilo na hayo mengine yote ambayo tunawapachika watoto wale. Kwa hiyo, sura mfanano ndio jina lililokubalika hivi sasa na naomba tulitumie hilo.

Kuhusu mashirikiano na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Hawa watoto wako chini ya Ustawi wa Jamii, inapokuwa Wizara ya Afya inaungana na Ustawi wa Jamii tunapaswa kwenda pale, bahati mbaya nimeikuta Wizara ya Afya ikiwa peke yake. Kwa hivyo, siwajibiki kwamba lazima niende pale, watu wa Ustawi wa Jamii bila shaka watakuwa wana mashirikiano nao.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2014/2015 - Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa asubuhi hii kupata nafasi ya mwanzo kuchangia katika Wizara hii ya Miundombinu na Mawasiliano. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Baraza hili kutoa maoni yangu machache yanayohusu wizara hii.

Mhe. Spika, pia nikupongeze wewe kwa jinsi unavyotuongoza katika Baraza hili. Hotuba yako ya jana ya maelekezo yako tumeifahamu na leo nadhani tuko vizuri. Vile vile nimpongeze Waziri kwa hotuba yake aliyotupa jana kwa umakini na wakati anawasilisha ni miongoni mwa mawaziri walioshangiriwa sana.

Mhe. Spika, mimi nianze na Idara ya Usafiri na Leseni ambayo katika kitabu hiki iko katika ukurasa 29, ningeomba nianze hapo. Ningeomba ninukuu kidogo kifugu cha 64 cha kitabu hiki.

Kifungu 64 kinasema kwamba:

> "Mhe Spika, idara hii inasimamia usalama wa watumiaji wote wa barabara, kuendesha shughuli za ukaguzi wa vyombo vya moto, kusimamia mafunzo ya udereva, upasishaji madereva, wanafunzi na walimu wa skuli za udereva, utoaji huduma za usafirishaji abiria na mizigo kwa njia ya barabara pamoja na kutoa vitambulisho vya utingo.....".

Mhe. Spika, *point* yangu iko hapa kusimamia usalama wa watumiaji wa barabara wote. Katika kipindi hiki katika mji wetu wa Unguja; Darajani hili suala la usalama wa watumiaji wa barabara kidogo uko mashakani. Katika marekebisho ya Baraza la Mji kuhamisha vituo mbali mbali vya stendi za daladala kumeongeza usumbufu mpya.

Mhe. Spika, "*kugeuza kitanda si dawa ya nyumba ivujayo*", kwa sababu tumeondoa msongamano Darajani lakini leo mchukulie mtu anayetoka Pemba kateremka boti anataka kwenda Fuoni akifuate kituo hicho Kisonge, na serikali inasema inatuhurumia sana raia wake na inatupenda. Je, kumbebesha mtu mizigo kichwani kutoka bandarini hadi Kisonge ni kumpenda? Kama huko ndio kupendwa, mimi itakuwa kupendwa sijui. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ningeiomba serikali idara hii kushirikiana na vyombo vyengine vinavyohusika ifanye utaratibu wa kuondoa usumbufu huu, huu si upendo, haya ni mateso tena ya makusudi. Mimi kwa kweli naona ni jambo la aibu serikali kusema inatupenda au inapenda raia wake na ikawa inafanya mateso ya makusudi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mara nyingi mimi huwa natembea mjini, huwaona watu jinsi wanavyosongamana, wanavyosukumana kuwania daladala, tatizo limezidi kuliko lile ambalo tunasema tumeliondoa ndio maana nikasema, "*kuvuta kitanda si dawa ya nyumba ivujayo*", tutafute matibabu ya tatizo hili lakini hivi tulivyofanya tumeongeza usumbufu badala ya kuuondoa. Nimesema katika wizara hii kwa sababu ya *point* moja tu, wao wanahusiana na utendaji wa barabara na usalama wa watumiaji, hapa usalama wa watumiaji uko hatarini.

Mhe. Spika, nije katika kitu kinachoitwa matengenezo ya barabara. Hapa imetajwa barabara ambayo inatengenezwa ni barabara ya Mgagadu - Kiwani, Mkanyageni - Kangani. Lakini huku juu kuna ujenzi wa barabara tatu za Kaskazini Pemba. Hizi zinatajwa kuwa zinajengwa, lakini Mgagadu - Kiwani imetajwa kuwa inatengenezwa. Kwa sababu hali hii barabara hizi zote bado haziko katika kiwango cha lami, ningelitaka kujua hii ya Mgagadu - Kiwani inatengenezwa vipi na hii ya Wete - Konde inajengwa vipi.

Mhe. Spika, katika utengezaji wa barabara hizi kwa kweli kuna changamoto kadhaa, mradi ambao wa barabara hii ya Mgagadu - Kiwani kabla ya Baraza hili kuingia sisi kila siku iko Mgagadu - Kiwani, Mgagadu - Kiwani bila ya kufika mwisho wake. Kwa kweli ni jambo ambalo hatuwatendei haki wananchi. Kwa sababu serikali inapotamka wananchi wanaingia tamaa, wanategemea kuwa serikali yao lile tatizo lililosemwa linataka kushughulikiwa, lakini ikiwa ni wimbo wa kila siku hatimaye watahisi kuwa hakuna lolote linalotendeka isipokuwa watu wanakwenda pale wakizungumza hatimae wanaondoka. Ningeomba wizara hii ijidhatiti kutekeleza miradi yake ili kuwajengea wananchi imani juu ya serikali yao.

Mhe. Spika, barabara ya Mkanyageni - Kangani kwa miaka kadhaa iliyopita ilikuwa inatajwa kuwa itajengwa baada ya kumalizika barabara ya Mgagadu - Kiwani. Lakini mara hii lugha imebadilika kuwa itajengwa bila ya kutegemea kumalizika kwa barabara hii. Ningeomba isije ikawa hadithi kama ile ya nyuma, kila siku kuwa itajengwa na ilikuwa hakuna kinachofanyika.

Mhe. Spika, nirudi katika barabara tatu za Kaskazini Pemba. Sisi mara baada ya kamati kumalizika, Kamati yangu ya Mawasiliano na Ujenzi iliteua Waheshimiwa wawili kwenda Pemba kuziangalia barabara hizi tatu. Kwa bahati Makamu Mwenyekiti wangu wa Kamati Mhe. Panya Ali Abdalla aliongoza ujumbe wa hao walioteuliwa kwenda huko Pemba.

Mhe. Spika, tulioshuhudia ni kuwa ile kazi ilikuwa haipo, lakini kwa sababu mjenzi alipata habari kwamba inakuja kamati wakafanya kazi ile, kama Serikali inavyofanya pahala ambapo anakwenda Rais kufanya huduma ya haraka haraka ili aone kuwa hapa pana kitu. Kwa hiyo na njia hii ya Konde - Wete tuliikuta inatiwa kifusi zile sehemu ambazo zimechimbuka zaidi ili tuone kuwa kazi inaendelea. Lakini kwa kweli ilikuwa kifusi kile kwa nilivyosoma mimi ni kwa sababu ya ile ziara yetu, lakini barabara waliyoikusudia kufanya kwa kipindi kile nadhani ilikuwa ni Wete - Gando. Huko ilikuwa kwa kiwango fulani wanamwaga kifusi na tuliwakuta wanafanya kazi zao. Lakini tulipokaa kwenye mazungumzo na wao mjenzi alionesha masikitiko yake kwamba amekwamishwa muda mrefu na kazi imekuwa ngumu, vifaa vyake vimechakaa hata vyengine kushindwa kufanya kazi.

Tulipotaka sisi tujue barabara hii itatiwa lami lini, ahadi aliyotoa ni kuwa mara tu mvua za masika zitakapomalizika. Bahati mbaya sijafanya *follow up* kuwa tayari ameanza au la, kwa sababu sina hakika kuwa mvua Pemba imemalizika. Lakini mvua za masika zimemalizika tarehe 21 mwezi wa 5, na leo ni tarehe 12 mwezi wa 6. Kwa hiyo sina hakika kuwa mjenzi huyo anaendelea na kazi hiyo au la.

Mhe. Spika, barabara hizi ni za muda mrefu sana, na jinsi inapochelewa kumalizika ndivyo Serikali inavyopata hasara. Kila siku Serikali inatenga pesa kwa kitu ambacho kimalizike miaka mitatu au miwili iliyopita nyuma. Katika malipo aliyolipwa kulikuwa na fedha nyingi alizolipwa mjenzi huyu kama ni fidia ya kucheleweshwa na Serikali. Kwa hiyo Serikali haioni kumchelewesha mkandarasi waliyempa kazi ni kujiongezea mzigo. Mzigo haibebi Serikali anabeba mlipa kodi. Kwa sababu ni sawa na mfanyabiashara anapoongeza bidhaa yake bei yeye haathiriki anayeathirika ni mtu wa mwisho; mlaji. Hapa Serikali inapochelewesha malipo kwa kazi mbali mbali, Serikali inajihisi kuwa inajiongezea mzigo, lakini anayeongezewa mzigo ni mlipa kodi. Kwa hiyo hapa ningeiomba Serikali iwaonee huruma walipa kodi.

Mhe. Spika, nije katika matengenezo ya barabara. Mhe. Spika, barabara ya Ole - Kengeja imezungumziwa kuwa itaweza kujengwa na itamalizika miaka mitatu ijayo. Ni barabara ndefu yenye kilomita 35 inayohitaji kujengwa kwa umakini, mfumo wa *labour base* ambao ni wa majaribio kwa barabara hii. Mhe. Spika, niiulize Serikali kwa nini kila jaribio la barabara lipelekwe Mkoa wa Kusini Pemba. Barabara 6 zilizopita nyuma zote zilikuwa *labour base* kwa majaribio Mkoa wa Kusini, Jimbo la Mtambwe lilikuwa na barabara 2 zote mbovu leo, kwa hiyo jaribio hili limefeli. Barabara ya Chambani mbovu jaribio limefeli. Barabara ya Mgagadu - Wambaa mbovu. Leo mnatuletea tena jaribio lile lile ambalo limefeli. Ujenzi huu duniani mmeupata wapi nyinyi? Kwa nini iwe Kusini Pemba tu. Kaskazini Pemba mmejenga barabara mwanana kabisa.

Mhe. Spika, katika majaribio haya Serikali huwa inakata miti yetu ikiwemo miembe na mikarafuu. Barabara hizi za Mtambile - Muwambe, Mtambile - Kangani bado wananchi hawajalipwa fidia ya vipando vyao. Mhe. Spika, miongoni mwa miti iliyokatwa ni mikarafuu, karafuu ambayo sasa hivi ni mali kweli kweli kule Pemba. Watu wanaookota karafuu mbichi wanaziuza ule mfuniko wa chupa kawaida kwa shilingi 800/= hadi 1,000/=. Leo mkarafuu ule Serikali imeukata haina habari ya fidia ya aliyekatiwa mkarafuu wake, unamletea maendeleo lakini unamtia umaskini. Maendeleo yenyewe hayapo kwa sababu barabara uliyoijenga gari ya ng'ombe ikipita kwato zinaifukua.

Mhe. Spika, ningeomba wizara hii iniahidi ni lini wananchi waliokatiwa vipando vyao kwa barabara ya Mtambile - Muwambe na Mtambile - Kangani watalipwa fidia. Kwa sababu muda umekuwa mrefu isiwe mtoto wa kuku kesho, kesho, kesho. Mhe. Spika, Serikali lazima ijali na ithamini raia wake. Mali zimeharibiwa kwa ajili ya maendeleo, kwa hiyo lazima hatua ya kulipa fidia ichukuliwe sambamba na uharibifu uliotokea.

Mhe. Spika, nije kidogo Idara ya Mawasiliano katika taasisi ambayo haimo katika wizara moja kwa moja, lakini kwa kuwa ni ya mawasiliano niizungumzie hii Kampuni ya *Zantel.* Mhe. Spika, tuliwahi kufanya ziara katika kampuni hii hapa Zanzibar na kule Bara na tulipata malalamiko ya wafanyakazi. Wafanyakazi wenye cheo cha aina moja hawatofautiani kielimu. Yule ambaye anafanya kazi Bara na anayefanya kazi Unguja maslahi yao ni tofauti mno. Mhe. Spika, hili nalisema ingawaje halimo ndani ya wizara, lakini wizara kwa kima fulani inahusika.

Halafu kampuni hii imeanzisha utaratibu siku hizi wa kuwafukuza wafanyakazi kiholela. Sasa unamfukuza mtu kazi halafu wanaajiriwa watu ambao tayari wamestaafu kazi. Kwa sababu wanawafukuza kazi watu ambao wamewaajiri mwanzo wamewatoa. Wana mpango wa kuajiri nasikia kuna kundi la wastaafu waliojikusanya wanaitwa UMAWA, wanaweka watu ambao tayari ni wastaafu. Sasa unamtoa mtu ambaye anafanya kazi unamrudisha mtu ambaye amestaafu. Sijui mantiki ya kufanya hivi iko wapi. Pengine unamstaafisha ambaye umri wake wa kustaafu haujafika unamuajiri mtu ambaye kwa masharti ya utumishi tayari umri wa kustaafu umefika, lakini ndio unamrudisha yeye kazini unamtoa yule ambaye ana uwezo wa kufanya kazi. Mhe. Spika, mtindo wa aina hii kwa kweli si mzuri na unawavunja moyo wafanyakazi.

Mhe. Spika, mimi kwa sababu ni Mjumbe wa Kamati ambayo inasimamia Wizara hii kwa sababu hiyo nitaunga mkono hoja. Ahsante sana.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutufikisha siku ya leo tukiwa hai na kutupa hazina ya uzima na afya njema hadi hapa. Hii ni hazina kubwa anayostahiki kushukuriwa *Allah.* Aidha, nichukue fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii.

Mhe. Spika, hoja iliyopo mbele yetu ni kujadili hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mhe. Spika, kama kuna wizara muhimu sana katika nchi basi Miundombinu na Mawasiliano ni moja katika wizara hiyo. Umakini na umahiri mkubwa katika kuendesha wizara kama hii unahitajika. Pale ambapo Serikali haikuwa makini sana katika kusimamia wizara hii, mashaka na madhila makubwa huwafika walipa kodi wa nchi kama yanavyotufika sisi hivi sasa.

Mhe. Spika, nianze na ukurasa wa 3 wa hichi kitabu cha Mhe. Waziri ibara ya 8 inayoelezea utekelezaji wa kazi za kawaida na maendeleo kwa miaka ya 2013/2014 na malengo ya mwaka 2014/2015. Mhe. Spika, nianze kwa kunukuu kama ifuatavyo:

"Utekelezaji wa kazi za kawaida na maendeleo kwa mwaka 2013/2014 ulizingatia dira ya taifa ya maendeleo ya mwaka 2020, malengo ya mikakati ya kukuza uchumi na kupunguza umaskini (MKUZA II)."

Mhe. Spika, la kusikitisha sana utekelezaji wa kazi hii badala ya kupunguza umaskini na kuwaongezea wananchi maskini kipato, basi kwa kiasi kikubwa umewapa umaskini badala ya kuwapunguzia.

Mhe. Spika, ni kweli kuweka *infrastructure* katika nchi ni maendeleo, lakini katika kuweka hizi lazima tuwe makini sana na hawa wananchi wa kawaida, lazima tuwe waangalifu na rasilimali za wananchi wa kawaida pale ambapo Serikali inataka kuleta maendeleo katika eneo husika.

Mhe. Spika, inasikitisha sana kwamba Serikali hii kabla ya kupeleka maendeleo pahala haifanyi uchunguzi wa kina, upembuzi yakinifu katika kuona kwamba miundombinu au jambo lolote watakalolifanya litawaathiri kwa kiasi fulani wananchi, hatimaye wananchi wale kupata fidia zao au kuwapatia chochote. Wao wanafanya tu, matokeo yake hapa Mhe. Mohammed Haji Khalid amesema kwamba walipojenga barabara ya Kengeja - Muwambe mali za watu nyingi zimeathiriwa ikiwemo mikarafuu na hadi leo hii hawajalipwa fidia.

Mhe. Spika, maendeleo tunayataka sana, lakini pia tunataka kuishi. Unapomkatia mtu mikarafuu yake, unapomkatia mtu minazi yake, unapomng'olea mtu rasilimali zake, wewe unaleta maendeleo, yeye je? Huyu baada ya kuleta maendeleo haheshimiki. Mhe. Spika, inasikitisha, hii ni dhulma!

Mhe. Spika, katika jimbo langu la Wawi hawa jamaa zangu wa Miundombinu na Mawasiliano wana *crusher* zao kule, walipoona wanateketea kwa kutumia *diesel* katika zile mashine zao wakapeleka umeme. Hapo mazao ya watu wengi sana tena miti ya kudumu kabisa ikang'olewa. Huu ni mwaka wa tatu napiga kelele katika Baraza hili jinsi ya watu walivyong'olewa miembe yao, minazi yao, michungwa yao na kadhalika. Hiyo ni katika maeneo ya Kibokoni, Vunjameme, Umangani na kadhalika. Serikali imeziba masikio na nashukuru sana kwamba mdogo wangu Mhe. Mohamed Aboud Mohamed pale ambaye ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ananisikiliza kwa makini sana.

Mhe. Spika, kwa kweli ni tatizo. Sisi ajira za Serikali kule kwetu vijijini ni tabu kupatikana, tunategemea zaidi kilimo na mifugo. Hata mimi Mwakilishi wao hapa ni mfugaji na mkulima mkubwa. Mhe. Spika, nilizungumza na Mhe. Rashid Seif Suleiman tukiwa nje ya ukumbi akaniambia kwamba kabla hajaanza yale yatalipwa, kwa sababu tunataka kumkodisha mfanyabiashara hizo *crusher,* akishatulipa zile *crusher* tutawalipa. Alinipa kauli hiyo karibu miaka mitatu nyuma. Nikizungumza humu ninakuwa mbaya, sina pa kuzungumzia zaidi ya hapa. Sasa mimi naogopa kumfuata nyumbani kwake ikaja ikawa mashaka mengine, bora nizungumze humu humu. Mhe. Spika, watu wana njaa wamewakatia minazi yao, miembe yao, mifenesi yao na kadhalika.

Mhe. Spika, nikupe mfano wa familia moja. Familia ya Omar bin Najim iliyopo Vitongoji Vunjameme wamekatiwa miembe 8 boribo kubwa zile Muyuni, kila mboribo anakodisha, tena mboribo mmoja mkubwa unazaa mara mbili kwa mwaka. Kwa maana mvua za vuli na mvua za mwaka. Kila msimu anakodisha boribo Muyuni baina ya laki mbili na nusu mpaka laki tatu (250,000 - 300,000). Muembe mmoja tu huo tufanye laki mbili tu mara nane ni milioni moja la laki sita(1,600,000). Huyu Bw. Omar bin Najim kila mwaka yeye kwa sababu hana kazi (1,600,000) milioni moja na laki sita ni pesa nyingi kwake. Wamemkatia miembe yake hiyo anapata shida, mbali minazi, mbali mifenesi. Mimi nimempigia hesabu ya miembe tu. Huu mwaka wa tatu wapo hawa karibu watu 30. Miti mingine sitaki niitaje nimetoa *sample* moja tu,lakini kuna watu karibu 30 wa Vitongoji pale wamekatiwa mazao yao na hadi hii leo, wewe unaniambia unapunguza umaskini kitabu hichi, sio umetuongezea umaskini watu wa Vitongoji. (*Makofi*).

Mhe. Spika, atakapokuja Mhe. Waziri sitaki tena kwamba nimekodisha hivi, nimefanya vile, aniambie Waziri ni lini na saa ngapi atakwenda kuwalipa. Kwanza nataka Mhe. Ali Juma Shamuhuna ambaye ni Waziri wa Elimu ninampongeza sana, alipoanza kufanya *process* ya kulipa alinishirikisha, akifanya malipo ananiambia leo nafanya malipo. Hajamaliza na yeye, naomba amalize Mheshimiwa lakini kila *step* ananimbia. (*Makofi*).

Juzi nilipokwenda kule wamekuja kudokolewa watu wawili hapa Fidel Castro kupewa malipo, zaidi ya watu 28 hadi leo hii hawajalipwa. Jamani hii si fedheha au kuna haja gani kuambiwa mimi ni Mwakilishi wao? Sisi hapa bwana tunawatetea wananchi sio maslahi yetu, kama ni maslahi yetu sisi wengine ni wakulima na wafugaji tulikuwa Vitongoji huko, lakini kama alivyosema Mhe. Mohammedraza Hassanali hichi kiti si changu, ni kiti cha watu wa Vitongoji na jimbo zima la Wawi. Sasa usipokuja na maelezo hapa Mhe. Waziri tutabanana hapa hapa, yawafurahishe watu wa jimbo langu, kinyume na hivyo tutabanana hapa! (*Makofi*).

Mhe. Spika, kuna tatizo jengine. Sisi watu wa Vitongoji na ukanda mzima huu wa mashariki tunategemea ardhi ya Makaani katika suala zima la kutupatia riziki. Kulima tungule na kufanya mambo mengine. Leo yanapokuja makampuni haya ya ujenzi, wanapewa katika yale maeneo ambayo si ya kwetu, kwa sababu ardhi ni mali ya serikali, lakini ndio tumezaliwa pale. Kwa mfano mimi familia yangu imenisomesha pale ikawa tunapata riziki kupitia kilimo cha tungule na mahindi pale Vitongoji. Kipindi kirefu hicho nikasoma tangu darasa la kwanza mpaka darasa la nane nikaingia darasa la tisa mpaka la kumi na mbili, la kumi na mbili mpaka la kumi na nne, *father* auze tungule zile apate ada ya kunisomeshea mimi.

Sasa munapeleka makampuni munatuhamisha katika yale maeneo, munachimba vifusi vinaweka mashimo yazuka chumvi, sisi hatuna pa kulima. Sasa mimi nadhani katika hili, sitaki niseme kwamba tulipwe lakini Mhe. Spika, ni lazima Mhe. Waziri muone kwamba unapomuonesha mtu katika ardhi ile, humuongezei utajiri kama unampunguzia umaskini kama ulivyoandika kwenye kitabu. Sijui tufanye nini ili kuwasaidia wale wakulima badala ya kuwapa hawa makampuni wakayafanya visima wao waelekee wapi.

Mhe. Spika, mimi nashauri mbali ya umaskini tunaowekewa watu wa Vitongoji na maeneo ya Micheweni huko, vile vile kuna *powerful destruction* ya mazingira. Yaani hawaambiwi kama wakishamaliza wakafukie wapande miti, wao wanaondoka tu. Nilisema siku za nyuma kama wale ni lazima walipe *ten percent* ili ije ikidhi kwenye yale mazingira. Lakini mazingira yanaachwa vile vile, matokeo yake tunaendelea kupata shida na mashaka katika maeneo yale.

Mhe. Spika: Una dakika 5.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, dakika 5 ni kidogo sana lakini niende sasa niipe tanbihi serikali katika madaraja. Daraja letu lile la Vitongoji baada ya kupitisha makampuni makubwa makubwa kujenga barabara, sasa hivi nendeni mukaangalie inaweza ikasababisha ajali wakati wowote. Ukiingia lile daraja la kupandia pale Umangani lile daraja kubwa linalounganisha Chake-Chake na sehemu inayochukuliwa kokoto, lile daraja limeshakuwa bovu, vyuma vimeshaanza kuharibika mule ndani. Kwa hivyo nataka mukaangalie muone wakati wowote inaweza ikatokezea *accident* pale.

Mhe. Spika, sasa naona niende katika mradi wa ujenzi wa barabara. Barabara za Kusini tunazoletewa nenda haraka bado dakika 5, barabara zinazosisima kwa mkono hivi, hazina umadhubuti, yaani kama nyumba za kienyeji tu zasizimasizima siku mbili zimeshabovuka. Mbona hawa wenzetu wa Kaskazini munawapelekea madhubuti au muko *very bias* katika hili. Kama ni zile bora hiyo Kengeja mpaka mutakapopata huo uwezo ndio muje kutujengea barabara lakini kwa barabara ya kusizima, kuanzia Ole kuelekea Kengeja kwa kusizima kwa mkono, bora musiijenge ikiwa hamujapata kampuni itatuletea uoza. Uoza huo hatuutaki.

Waheshimiwa Wajumbe ninawaombeni sana Wawakilishi ikiwa barabara hii ya Kengeja itakayojengwa ni kama uoza unaotoka hapa Chanjamjawiri kwenda Tundauwa, basi uoza ule hatuutaki. (*Makofi*).

Mhe. Spika, nije katika mradi wa ununuzi wa meli mpya, kuna tatizo hapo. Siku zote meli mpya ilipopata ajali tukaambiwa baada ya muda mutajengewa meli nzuri na nini. Leo tunaambiwa ati vyuma vya mkuku mpaka mwezi wa ngapi ndio vinaanza kutandikwa sasa chini, yaani mwezi wa saba. Haya jamani hiyo 2015. Mimi naona hawa Waheshimiwa hawasemi kweli.

Sisi tulipokuwa tunajenga meli ya MV. Mapinduzi kupitia TVZ, kila hatua tulikuwa tukiwaonesha wale jamaa zangu wakiangalia, walikuwa wakiiona kama sisemi kweli wanisute. Sisi tulikuwa wazi katika kufanya matendo sio kusema sema tu maneno. Meli tunaitaka ifike kama mulivyoahidi. Haikufika hapa basi lazima muwajibike. (*Makofi*).

Mhe. Spika, niende katika Mamlaka ya Uwanja wa Ndege. Mhe. Spika, mamlaka hii kuna tatizo. Mhe. Spika, hivi ni visiwa. Leo akienda pale Waziri anafungiwa gari yake akitaka kusafiri, na ukimwambia Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano aah! ile ni mamlaka, si ni jambo gani. Haya mamlaka itashinda mihimili mitatu ya dola, mamlaka itashinda serikali, mamlaka itashinda mahakama, mamlaka litaishinda Baraza la Wawakilishi hili, wawakilishi wanadhalilishwa. Kama mamlaka ile ina nguvu tutaizuia sisi humu kufanya kazi zake. (*Makofi*).

Mhe. Spika, nimalizie naona kwa ile *Pemba Airport*. Hichi ni kizungumkuti. *Pemba airport* siku zote tunadanganywa. Kama kuna sehemu muhimu sana basi ni ile *Pemba airport,* kwa sababu pale pana wajasiriamali wengi wanataka kufanya shughuli zao hapa Dar es Saalam, eeh! wapo. Unapowaunganisha Wapemba na Dar es Salaam, unawapounganisha Pemba wakawa wanaingia usiku na mchana uchumi wa nchi utaongezeka. Leo kila kukicha barabara tunataka kuweka hivi, kilomita ngapi, Waturuki wameshasema. Maneno tu humu ndani.

Mhe. Spika, *kula uhondo kunataka matendo, asiye matendo hula uvunda*. Hebu fanyeni matendo ili tule uhondo sio mutulishe uvundo kwa maneno maneno.

Mhe. Spika, nimalizie kwa ile hoja ya wajasiriamali kwamba wapo wengi. Meli hakuna. Ilipokuwepo *Virgin Butterfly* hapa, yule jamaa aliyekuwa ana *Virgin Butterfly*, alikuwa akiwaunganisha Wazanzibari mpaka Mombasa, unaondoka Dar es Salaam, unakuja Unguja, unakwenda zako Pemba, unakwenda Tanga, unakwenda Mombasa unarudi siku hiyo hiyo. Wafanyabiashara hawa akina Bopar wametononoka kupitia siku zile, ndio wakainuka hawa akina Bopar.

Kwa sababu biashara zile za kupeleka ndizi za mkono wa tembo kule Mombasa, vietezo hawa wanaotengeneza akina Mhe. Hija Hassan Hija kule kwao wanavihitaji sana kule Mombasa, Pate, Lamu kuna wale Wamahara wanakuja kuangalia jamaa zao pale kwa Wagunya pale, wananunua vietezo. Hawa wajasiriamali wa kule Muambe, bizari yao inapendwa sana kule. Ukiwa na chombo cha uhakika cha usafiri, wanaweza wakafanya shughuli zao kule Mombasa. Inasikitisha kwamba leo tunaambiwa ndio kwanza mkuku unajengwa sasa. Jamaa mutatuua! (*Makofi*).

Mhe. Spika, ahsante. (*Makofi*).

Mhe. Spika: Ahsante sana. Nimkaribishe Mhe. Ismail Jussa Ladhu, Mhe. Marina Joel Thomas anajitayarishe na Mhe. Rufai Said Rufai pia anajitayarisha. Tumsikilize Mhe. Jussa.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, ninaanza kumshukuru Mola wetu Mtukufu kwa kuturuzuku neema zake za uhai na uzima tukaendelea na shughuli zetu hapa katika chombo hichi muhimu cha wananchi wa Zanzibar. Nikushukuru na wewe Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii na mimi kuichangia wizara hii ya Miundombinu na Mawasiliano.

Tatu Mhe. Spika, nimpongeze Mhe. Waziri kwa kuwasilisha kwa ufasaha mkubwa hotuba yake ya bajeti ambayo imejaa maneno lakini haina vitendo.

Mhe. Spika, mwaka jana nilipochangia katika bajeti ya wizara hii, nilisema neno ambalo na leo ninalirejea tena. Kama Mhe. Rais anataka kujitendea haki yeye na kuwatendea haki wananchi wa Zanzibar wasije wakamuhukumu vibaya, basi wizara hii anapaswa kuivunja kutoka juu mpaka chini. (*Makofi*).

Mhe. Spika, nilisema mwaka jana na ninarejea tena mwaka huu. Ninasema haya nikiwa ni Mjumbe wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ambayo ilisimamia wizara hii.

Mhe. Spika, moja ambalo linaonekana pale, mengi wanayolalamikia Waheshimiwa Wawakilishi ni kwamba haitaki umahiri mkubwa kugundua kwamba katika wizara ile hakuna *team work*, hakuna moyo wa pamoja kufanya kazi baina ya viongozi wake na watendaji wakuu. Unayaona hata katika vikao vya kamati Mhe. Spika. Katika hali ambayo hakuna imani miongoni mwao, hakuwezi kupatikana tija yoyote Mhe. Spika, hilo ni moja. (*Makofi*).

Lakini pili Mhe. Spika, bado ninasema katika wizara yangu ni hii hali inaonekana sasa hivi. Wamesema hapa Waheshimiwa Wajumbe, tunachokiona katika wizara hii ni usanii. Mhe. Spika, kuna barabara zinapigiwa kelele mwaka mzima zimeachwa. Mwezi huu wa Mei na Juni kwa sababu ya bajeti inakuja ndio tunatiliwa viraka viraka mitaani huko. Unamfanyia nani usanii huu. (*Makofi*).

Mhe. Spika, wamesema hapa Waheshimiwa tuliomba kamati tukakague mradi wa barabara tatu za Kaskazini Pemba ambazo kila siku ni nyimbo. Vimepelekwa vifaa vya kubabaisha watu lakini kimsingi Mhe. Spika, hakuna kilichofanyika pamoja na kwamba *MECCO* ameshalipwa pesa zote alizokuwa akizidai. (*Makofi*).

Mhe. Spika, hii ni muhimu kwa sababu watu watakuja kupima mafanikio katika miaka mitano mwakani tukijaaliwa. Mhe. Spika, hapo hapo kwa sababu ya muda leo itabidi niseme kwa ufupi sana katika hoja, kwa sababu nina nyingi na muda ni mchache mumetupunguzia.

Mhe. Spika, ninamwambia Mhe. Waziri nitaizuia bajeti yake kwa kuiondolea shilingi mpaka aniambie milioni 40 za Mji Mkongwe walizozichukua wamezipeleka wapi. Jana Mhe. Mohammedraza Hassanali kazungumzia barabara zake. Mfuko wa Mbunge wa Mji Mkongwe umetoa milioni 40 kutengeneza barabara ya Mtendeni na kumalizia vipande vidogo vidogo viliomo katika Mji Mkongwe. Walikuja wakatufanyia usanii Mkunazini wakatuachia mashimo mpaka leo pale, lakini milioni 40 zimetafunwa na wizara yake hakuna chochote. Kama sijapata maelezo ya kina, bajeti hii nitaizuia na nitawaomba wenzangu tuizuie bajeti hii. (*Makofi*).

Mhe. Spika, miradi ya wizara hii imekuwa ni wimbo wa taifa, unaimbwa tu kila asubuhi munanyanyuka basi, lakini hakuna utekelezaji. Wamesema wenzangu kwa sababu ya muda ninaokoa, barabara ya Ole/Kengeja kaisoma jana Mhe. Mohammed Mbwana Hamad hapa, vitabu vya miaka mitatu vya bajeti vinarejea maneno yale kwa yale, hakuna chochote kilichokuwa. (*Makofi*).

Huu ndio utendaji wa serikali hii Mhe. Spika. Barabara tano za Kaskazini Pemba zimerithiwa tangu Serikali ya Awamu ya Sita mpaka Awamu ya Saba inamaliza muda wake mwakani tukijaaliwa hakuna kitu. Barabara ya Wete/Chake-Chake ilikuwa ni sehemu, ukisema barabara tano za Kaskazini Pemba, moja ilikuwa ni hii. Hatimaye imeondolewa inaitwa barabara ya tatu, lakini imebakia barabara mbili tu, ya tatu imetolewa imeundwa mradi wake mbali hakuna kilichokuwa mpaka leo. (*Makofi*).

Kuna maneno ya barabara zilizoingia mjini Unguja, hakuna chochote Mhe. Spika. Barabara ya Amani/Mtoni inaimbwa sijui mwaka wa ngapi haimaliziki barabara ile, kila siku unakuta barabara visingizio vipya. (*Makofi*).

Mhe. Spika, lakini la ajabu mimi ninatuhumu kwamba kuna mkakati wa watu kutafuna fedha katika miradi hii. Kwa sababu kila mwaka kunaombwa fedha za kuambiwa matayarisho ya ujenzi. Kwa mfano mwaka huu tunaomba barabara ya Ole/Kengeja kwamba zitengwe milioni 500 matayarisho ya ujenzi. Matayarisho haya kila mwaka, zitakuwa hazitimii pesa lakini hizo hizo za udoho udoho zinazochukuliwa hazipatikani zote zinachukuliwa, zinazopatikana zinachukuliwa hakuna kinachokuwa.

Barabara zinazoingia mjini Unguja tunaambiwa hazipata mfadhili lakini bado kunaombwa tena milioni 50 za mradi huu, za nini?

Mhe. Spika, wamesema wenzangu hapa kwamba kumekuwa na utaratibu kwa huu utaratibu wao wa utekelezaji miradi, kila siku ukisoma vitabu hivi Mhe. Spika, cha miradi kwamba barabara imeshajengwa, hatuna kifusi. Tunatengeneza kifusi, inachongwa inawekwa sawa inakuja mvua inachafua tena, kila siku inatia hasara tu, fedha za walipa kodi maskini wa Zanzibar, zinatafunwa namna kama hii. (*Makofi*).

Mhe. Spika, kutafuna pesa si lazima kama kuwe kuiba. Ukizipeleka katika kitu ambacho unajua hakina tija, pia ni kuzitafuna pesa za walipa kodi wa Zanzibar. Kila mwaka unakwenda kuweka kifusi, hakitiwi lami, kinaondoka na mvua, kila siku hayo kwa hayo maji ya futi na nyayo, tumechoka Mhe. Spika! (*Makofi*).

Halafu Mhe. Spika, ninataka maelezo kutoka kwa Mhe. Waziri vile vile au serikali kwa ujumla wake. Kuna miradi mingi humu haitolewi maelezo ya fedha ya barabara, tunaambiwa inachangiwa na Mfuko wa Barabara. Lakini ukitaja Mfuko wa Barabara huambiwi kima cha fedha, utaambiwa iko Wizara ya Fedha, lakini Wizara ya Fedha akija, anatupa ya jumla jumla tu, hatuwekei kwa miradi iliyokuwepo Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano. Kwa nini Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano isitwambie mradi mmoja mmoja katika fedha inazochukua kwenye Mfuko wa Barabara ambazo zinachangiwa na walipa kodi wanapotumia barabara? Kila wanaponunua mafuta kwamba kwa nini hawatwambii kima cha fedha zilizotumika katika matengenezo ya barabara ni hizi. Mimi Mhe. Spika, ninatuhumu kwamba kuna mambo yao ndani watendaji ndio maana hawataki kueleza gharama halisi za miradi hii. (*Makofi*).

Mhe. Spika, matokeo yake leo Mhe. Waziri anatwambia katika kitabu hichi kwamba ati kwa mwaka ujao wanategemea kutumia Mfuko wa Barabara fedha zake kututengenezea barabara kilomita 697, *what's a joke*? Kilomita tatu, mbili munatuahidi katika ukurasa, humu katika ile Idara ya Ujenzi wa Barabara 697 mnatwambia mutatengenezea kwa mwaka mmoja Mhe. Spika, si tunadanganya hapa? (*Makofi*).

Mhe. Spika, nije katika Mamlaka ya Viwanja vya Ndege. Mhe. Spika, ni aibu na ni *shame* kwa nchi hii. Nchi inayotegemea utalii. Katika nchi zinazoongoza kuwa na viwango vikubwa vya *airport service charges*, moja ni Zanzibar duniani. Sasa *airport service charge* inaitwa ni *airport service* kwamba inatakiwa itoe *service* ambayo tunailipia. Leo hakuna *service* yoyote ya maana.

Mhe. Spika, mpaka leo aibu unakuja mgeni unamwambia afungue begi lake unatia mikono katika begi lake ukisasakura, kama vile mtu ambavyo amepelekewa banjo harusini; *x-ray machines* hazifanyi kazi. Leo tunaambiwa katika *apron* mpya pale, mabasi yanayotuchukua Mhe. Spika, yanayotuchukua yameandikwa *private hire* kama daladala za mjini. Aibu na *shame* Mhe. Spika, kwa nchi yetu. Wanapokuja wale wazungu wakawa wamemiminika mule kwa mamia, ninajiuliza hizi fedha wanazolipa zinakwenda wapi? (*Makofi*).

Mhe. Spika, tena ajabu tunaambiwa ndani ya kitabu hichi kwamba kuna mafanikio, kwa maana ya mapato kwa sababu abiria wameongezeka; mwaka jana walikuwa wamehudumiwa 649,724 mwaka huu ni 727,151.

Miaka iliyopita kwenye mizigo ilikuwa ni tani 850, mwaka huu 1326. Sasa ongezeko hili si linazidisha mapato. Mbona hayaonekani katika *improvement* ya *service* kwenye *airport* zetu.

Lakini jengine Mhe. Spika, ninasema kwa ufupi sana kwa sababu ya muda. Nitaizuia tena bajeti hii, nitaizuia shilingi mpaka nipate maelezo kuhusu suala la kadhia ya madawa ya kulevya, mabegi mawili yaliyokamatwa katika *airport* yetu.

Mhe. Spika, serikali inawajibika kwa pamoja hapa kwa mujibu wa ibara ya 43 (5) ya Katiba ya Zanzibar, wasitupiane mipira humu ndani. Ukimuuliza huyu, anakwambia huyu, na huyu anasema yule, wanatupiana mipira tu Mawaziri humu ndani. (*Makofi*).

Kila wizara inayogusa tuambiwe serikali kwa pamoja inawajibika humu, nini kadhia ya madawa ya kulevya. Yalikuwa ya nani tusifichwe. Kuna nini katika mchezo wa *CCTV camera* pale ambazo zilirekodi mambo yale, kunafichwa nini? Mhe. Spika, tuambiwe. (*Makofi*).

Mhe. Spika, leo wanawadhulumu, wamewanyang'anya wafanyakazi wadogo wa *ZAT* pale wanaambiwa wakubwa wanatamba humu. Wakati *CCTV camera* zilikuwepo, mimi nina hakika wameonekana, kuna nini kinafichwa katika bajeti. Nani aliyehusika na mabegi yale mawili ya madawa ya kulevya. (*Makofi*)

Mhe. Spika, vile vile nimuombe Mhe. Waziri akija aje aniambie mapato ya Zanzibar katika taasisi za Muungano, kila mwaka nimekuwa nikiliulizia, kuna taasisi za Muungano ambazo ziko katika wizara yake.

Nitatoa mfano mmoja tu Mhe. Spika, Mamlaka ya Usafiri wa Anga, tunaambiwa kwa mwaka inaingiza dola milioni 2, Zanzibar inapata kiasi gani, anga yake ni sehemu ya Anga ya Jamhuri ya Muungano inaendeshwa kwa pamoja, lakini nataka maelezo kuhusu *TMA, TTCL,TCRA,TPC,TCAA* zote ziko kwake tunapata kiasi gani sisi Zanzibar kutokana na mamlaka hizi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, bahati mbaya muda leo sio rafiki. Naomba niende katika suala jengine la *Airport Terminal.* Suala hili mwaka jana nililizungumza kwa ukali na ukafikia Mhe. Spika, ulikitumia kiti chako ukaipitisha wewe bajeti ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano. Nikuombe sana Mhe. Spika, jana nilipokuona umekuja kwa wizara hii nikasema sitegemei kama utanifanyia kama yale ya mwaka jana Mheshimiwa. *(Makofi)*

Kwa hivyo, nikuombe utuachie Waheshimiwa Wawakilishi tutake maelezo. Mwaka jana nilipolisimamia suala la Mradi wa *Airport Terminal* nilisema hapa, na nikaja na ripoti zote za wataalamu. Ripoti ya *ADPi*, ya *CMS* nikasema kunafichwa nini Mhe. Spika. Serikali ilitupa maelezo mengi na nimekwenda ku-*print hansard* yote ya kupitisha vifungu vya mwaka jana ninayo hanidanganyi mtu, aliyoyasema yote yamo humu. Alichotuambia Mhe. Omar Yussuf Mzee kimo ndani humu, alichotuambia Mhe. Rashid Seif kimo ndani humu na alichotuambia Mhe. Mohamed Aboud kimo ndani humu. Leo yote Mhe. Spika, yameanguka.

Mhe. Spika, kwa ufupi sana kwa sababu ya muda, kulikuwa kuna *option* tatu zilitolewa hapa. Tukasema kwa maslahi ya Zanzibar kwa nini Mhe. Spika, kama lile jengo limekwama lisibomolewe likarudishwa nyuma likajengwa jengo kwa mujibu wa kiasi kinachotakiwa, tukaambiwa ni gharama. Mhe. Waziri wa Fedha alituambia litagharimu milioni 140 dola, lakini hili la kunusuru lilikuwa milioni 114 dola.

Mhe. Spika, tumekwenda kamati, leo tukuambie ukweli hapa. Tumekwenda kamati hawatuambii ukweli hawa, wametuambia ndani ya kamati gharama zimeshaongezeka, zilikuwa milioni 70.4 dola mwanzo, zikaongezwa nyengine 11.8 milioni dola, zikaongezwa nyengine 46.5 milioni dola, mpaka sasa hivi Mhe. Spika, ni 128 milioni dola zinakwenda katika mradi ambao haujulikani mwanzo wala mwisho.

Mhe. Spika, niliposema mwaka jana hapa kwamba ilikuwa kulifungua wale wa *ADPi* wenyewe walisema, ingeongeza milioni 13 dola katika milioni 114. Mhe. Spika, maana yake ingekuwa 127 milioni, zimeshafikiwa sasa kwa jengo la kulibakisha pale pale, hasara hii anaibeba nani Mhe Spika. Mbali ya kutuambia kwamba lingefunguliwa kulikuwa kuna tija ya ku-*save* gharama za umeme, takriban dola 460,000 kwa mwaka, tungepata mapato kwa kuongeza maeneo ya biashara kwa dola takriban milioni 1.5 kwa mwaka, zote zingerudisha gharama zile ambazo tungeziingia ndani ya miaka mitano.

Mhe. Spika, yametupiliwa mbali yale, wamelazimisha msimamo wao na walikuwa wanawalinda watu wao wanaowajua wenyewe, leo tumeshafika 128, tumeambiwa ndani ya kamati haya. Tukawaambia kwa nini hatuelezi ukweli, kila mmoja alikuwa anamunya munya maneno tu katika Kamati.

Mhe. Spika, kwa sababu ya muda nimalizie kwa suala moja au mawili kwa haraka. Nataka maelezo kuhusu mradi wa uwanja wa ndege wa Pemba, kwa nini tunapigwa dana dana kila siku kwa masuala haya, kunafichwa nini?

Vile vile Mhe. Spika, tuambiwe ripoti ya ukaguzi wa *FILTEX* iliyokwenda kukagua ile *register* ya meli ya kimataifa ya Zanzibar pale. Baraza la Wawakilishi lilitoa agizo mpaka leo ukaguzi ule ripoti yake haijaletwa.

Mhe. Spika, nimalizie kwa kusema kwamba namtaka Mhe. Waziri aje anipe majibu ya kina ya masuala haya, na masuala mengi nimeyaacha kwa sababu ya muda. Lakini nimuambie kwamba vipaumbele vya serikali hii bado navipigia kelele. Mhe. Spika, aje aniambie Mhe. Waziri, ndani ya mwaka mmoja Katibu Mkuu wake kasafiri mara ngapi? Safari tu ndio kipaumbele cha serikali hii, ndani ya miezi miwili iliyopita aje atuambie Katibu Mkuu wake kasafiri mara ngapi na yeye mwenyewe. Hiki ndio kipaumbele cha serikali hii, kusafiri, kusafiri, na huku wakitafuna posho, lakini huduma za wananchi ziro.

Mhe. Spika, siiungi mkono bajeti hii, nitaizuia mpaka nipate maelezo ya kina juu ya hoja zote ambazo nimezitoa. Mhe. Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Ismail Jussa Ladhu na nakushukuru pia kwa kuokoa muda. Sasa naomba nimkaribishe Mhe. Marina Joel Thomas na Mhe. Rufai Said Rufai akijitayarisha na hatimaye Mhe. Farida Amour Mohammed.

Mhe. Marina Joel Thomas: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuweza kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano.

Mhe. Spika, kwanza naomba nitoe pongezi za dhati kabisa kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa uongozi wake imara, wenye lengo na nia njema kwa wananchi wake ya kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, pia naomba niwapongeze Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Wakurugenzi wote na watendaji wote wa wizara hii kwa kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

Mhe. Spika, nitachangia katika maeneo manne. Kwanza miradi ya maendeleo, sekta ya usafiri wa barabara, sekta ya usafiri baharini pamoja na Mamlaka ya viwanja vya ndege.

Mhe. Spika, naanza katika miradi ya maendeleo, nitaanza na mradi wa barabara za vijijini Kaskazini Pemba. Katika kitabu cha hotuba ya bajeti Mhe. Spika, mradi huu umehusisha barabara tano za Kaskazini Pemba, zenye ukubwa wa jumla ya kilomita kama 35. Barabara zenyewe zimeelezwa humu ni Mzambarau -Mbandani ambazo ni kilomita 7.9, barabara ya Mtambwe kilomita 13.6, barabara ya Chwale Kojani kilomita 1.9, barabara ya Kipangani hii imejengwa kilomita 8.9 na Mzambarau - Mapofu barabara hii imejengwa kilomita 8.9.

Mhe. Spika, miradi hii imekamilika katika mwaka huu. Kwa hivyo, naipongeza serikali kwa dhati kabisa kwa jitihada yake kubwa ya kukamilisha miradi hii. Miradi hii imezinduliwa na viongozi mbali mbali wa serikali hii, akiwemo Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Naipongeza sana serikali kwa kazi kubwa waliyoifanya.

Mhe. Spika, ukiangalia katika kitabu chetu hiki kwenye kiambatanisho namba 2, kimeeleza baadhi ya miradi mingine pia nayo imekamilika katika jadweli hili. Kuna miradi kama sita hivi nayo imekamilika katika kipindi hiki cha mwaka huu wa 2013/14. Kwa hivyo, pia hapa napenda kutoa pongezi za dhati kabisa kwa serikali hii.

Mhe. Spika, nitakwenda katika mradi wa barabara tatu za Pemba pia. Barabara ya Wete- Konde na Wete-Gando. Mhe. Spika, mradi huu kweli ni wa siku nyingi na ulikuwa umesita kutokana na Mkandarasi kutolipwa fedha zake. Lakini kutokana na ripoti ya kitabu hiki imeelezwa kwamba Mkandarasi amelipwa fedha zake, amelipwa bilioni

2.855 katika barabara za Amani- Mfenesini-Dunga, Bumbwini -Mahonda na bilioni 6.079 pia amelipwa ili kuendelea na kazi hiyo, na katika ripoti hii imesema kazi hiyo inaendelea vizuri.

Mhe. Spika, hapa pia natoa pongezi kwa serikali kwa jitihada za kumlipa Mkandarasi, ili kuona kwamba zile barabara zinaendelea kuliko kuziacha zikaendelea kuharibika, na hasa ukizingatia kulikuwa na kipindi kikubwa cha mvua zilinyesha na barabara nyingi zimechimbika. Kwa hivyo, natoa shukrani kabisa kwa kulipa deni hili kwa Mkandarasi na hivi sasa yumo anaendelea na shughuli zake za ujenzi.

Mhe. Spika, nikiendelea kile kiambatanisho ambacho nilikisema cha miradi ambacho kipo kwenye ukurasa 63 kimeeleza kuna barabara ya Amani - Mtoni, kuna Kivunge-Mkokotoni, Mkwajuni-Mshelishelini, Kwa Abasi Hussein, kuna barabara ya Msitu wa Ngezi, kuna Chake -Wesha. Hizi zote Mhe. Spika, zimekamilika na ameonesha katika kiambatanisho chake. Wakati mwaka jana katika bajeti hii hii ya mwaka jana miradi hii ilikuwa haijakamilika, kwa hivyo naipongeza serikali.

Mhe. Spika, nitakwenda katika Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara. Mhe. Spika, idara hii ni muhimu na inategemewa kwa ujenzi na ukarabati wa barabara. Katika idara hii Mhe. Spika, kuna changamoto ambayo inaikabili idara hii, kuna suala zima la ukosefu wa vifaa vya kutosha, na hivyo vifaa vyenyewe haviko vya kutosha na pia vya uhakika.

Kwa hivyo hapa nilikuwa naiomba serikali iangalie sana idara hii, kwa sababu ndio inayobeba mambo yote, iingiziwe fedha za kutosha kwa ajili ya kitengo chake ambacho ni cha matengenezo ya zana.

Ukiangalia katika bajeti ya mwaka huu kitengo hiki kimetengewa shilingi milioni 2.8, kweli kitaweza kutengeneza vifaa vya kufanyia kazi, hizi ni fedha kidogo sana. Mhe. Spika, naiomba sana serikali ikiangalie sana hiki kitengo ili kuweze kufanya kazi zake kwa ufanisi bila ya matatizo yoyote.

Mhe. Spika, nikiendelea nitakwenda kwenye Sekta ya Usafiri wa Baharini. Katika sekta hii kuna suala zima la ujenzi wa meli. Hapa niipongeze serikali pia kwa kuwajali wananchi wake kwa kutafuta meli kubwa ya kisasa na hivi sasa inaendelea kutengenezwa. Meli hii Mhe. Spika, itasaidia kurahisisha usafiri kwa wananchi wetu.

Vile vile hapa nilikuwa na wito nawaomba hawa watendaji wanaosimamia suala zima la utengenezaji wa meli. Kwa suala hili nawaomba watendaji wawe wazalendo, waadilifu,waaminifu na wafanye jukumu lao hili zito ambalo wamepewa ili kuleta maendeleo katika nchi yetu.

Mhe. Spika, nitakwenda katika ukaguzi wa vyombo vya usafiri. Mhe. Spika, suala la ukaguzi wa vyombo vya usafiri ni muhimu sana, kwa sababu tukifanya ukaguzi katika vyombo vyetu tunaweza kugundua mambo mbali mbali ambayo pengine tunaweza kuzuia kwa kiasi fulani matatizo ambayo yangeweza kujitokeza. Kwa hivyo, hapa nilikuwa nawaomba kitengo ambacho kinashughulikia suala la ukaguzi, kisisite kiendelee na taratibu zake za kukagua. Najua kinakagua, lakini kiendelee ili kuhakikisha vyombo vyote vinakwenda katika hali ya uzima na visije vikaleta matatizo katika kipindi kijacho.

Mhe. Spika, suala zima la tiketi bado ni tatizo, tiketi zipo za kiholela. Pia nawaomba mamlaka husika ilifanyie kazi suala hili la ulanguzi wa tiketi.

Mhe. Spika, Shirika la Bandari kwa mwaka huu lilipangiwa kukusanya shilingi bilioni 12.81 lakini hadi kufikia Machi 2014 Mhe. Spika, shirika hili limekusanya bilioni 14.6 sawa na asilimia 114.

Mhe. Spika, hii ni hatua nzuri, shirika linahitaji kupongezwa, kwa sababu pesa hizi ambazo zinakusanywa zitasaidia sana katika shughuli mbali mbali za maendeleo, na maendeleo hayo ni kwa ajili ya wananchi wetu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwenye mafanikio hapakosi changamoto. Shirika hili linakabiliwa na ukosefu wa eneo la kujenga mnara katika maeneo yalioko bandarini. Hapa niiombe serikali iwatafutie eneo ambalo watajenga mnara huo, kuliko hivi sasa wanakodi majengo ili kuweka mnara huo, kwa hivyo nawaomba watenge maeneo maalum katika maeneo ya bandarini ili kujenga mnara huo, ili kuweza kusaidia kufanya kazi zao vizuri kabisa. Pia itasaidia kupunguza gharama ambazo wanalipa kutokana na kukodi majengo hayo.

Mhe. Spika, nitakwenda kwenye Sekta ya Usafiri wa Anga. Katika sekta hii napenda kuipongeza wizara pamoja na mamlaka ya uwanja wa ndege kwa kazi nzuri wanazofanya, wanajitahidi sana, kwenye ukweli tuseme, changamoto zipo. Lakini Mamlaka ya Uwanja wa Ndege inajitahidi na katika makusanyo pia imeeleza kuwa mwaka huu wamekusanya bilioni 3.1 na katika vianzio vyake mbali mbali vya mapato, ikiwemo utuaji wa ndege, kodi za ofisi, faida za biashara, ada za maegesho ya magari na mapato mengineyo.

Mhe. Spika, katika kipindi cha nyuma mamlaka ilikuwa haikusanyi mapato namna hii, lakini kutokana na uongozi imara wa Mkurugenzi wa Mamlaka hii, ameweza kukusanya fedha hizo ambazo zitasaidia kuendesha shughuli mbali mbali za nchi hii.

Mhe. Spika, nataka niseme kidogo tu kuhusu maendeleo. Maendeleo hayaji bila ya changamoto, ukitaka kujenga barabara itabidi uvunje nyumba za watu, tunataka maendeleo, tunataka wananchi wetu wanaopeleka biashara zao wapate usafiri wa uhakika. Kwa hivyo, maendeleo hayaji bila ya changamoto.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo, naona nimalizie hapa. Baada ya kusema hayo naunga mkono kwa asilimia mia moja. Ahsante Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Nakushukuru sana Mhe. Marina Joel Thomas kwa mchango wako huo na kwa kuokoa muda. Nimkaribishe basi Mhe. Rufai Said Rufai na yeye kama atafanya hivyo nitafurahi sana, halafu tumsikilize Mhe. Farida Amour Mohammed, wakati Mhe. Hassan Hamad Omar anajitayarisha.

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Spika, awali ya yote kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia asubuhi hii ya leo kuwa mzima wa afya na nikaweza kuja kusimama hapa.

Pia nikutakie na wewe uzima, Mwenyezi Mungu akujaalie uwe mzima zaidi na kuweza katika watu wengi walioomba kuchangia wizara hii na mimi ukaweza kunipa nafasi kuweza kutoa mawazo yangu katika hotuba hii ya Makadiro ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii ya Miundombinu na Mawasiliano ya Mhe. Rashid Seif Suleiman.

Mhe. Spika, mimi nitaanza katika ukurasa wa 8 wa hotuba hii unaoelezea mradi wa barabara tatu za Kaskazini Pemba. Mhe. Spika, mradi huu ni miongoni mwa miradi mikongwe ambapo kazi zake zinaendelea, lakini bado hazijafikia mwisho.

Mhe. Spika, mradi kama huu unapokwama ukawa haumaliziki, basi tutarajie kwamba kubwa serikali inabeba madeni ambayo ni ya kujitakia, na hatima yake madeni haya wanakuja kulipa wananchi wetu ambao sisi ndio walipa kodi.

Mhe. Spika, hii kampuni ilipoanza kufanya kazi za barabara hapa Unguja, mwanzoni ilikuwa inakwenda vizuri, ikajenga barabara vizuri hapa, hatima yake kampuni hii ikapewa na barabara tatu zile za Kaskazini Pemba na wananchi wa Pemba walifurahi sana, kuja kwa Kampuni hii ya *MECCO* kujenga barabara. Lakini mimi sitaki niilaumu sana kampuni, lawama hizi nazipeleka kwa serikali, kwa sababu serikali ndio wawezeshaji wa kampuni. Kwa hivyo, Mhe. Spika, na kampuni haifanyi kazi kama mkandarasi hajaenda kwa ajili ya kuweka mambo sawa, watu wa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano pamoja na wale watu wa tathmini ya nyumba na vilio vya wananchi wetu.

Mhe. Spika, lakini ndani ya barabara hizi tatu mbili zinaelekea kuwa na mwelekeo na mwelekeo huo ni mbovu sana. Kwa mfano, tukiangalia barabara ya Wete/ Konde kwa kweli ni barabara ambayo inatisha sana, kwa sababu maji yamechukua kifusi chote na halafu kifusi chengine kije kuingizwa tena na tunazidi kuchafua mazingira katika maeneo yale yanayochimbwa kifusi.

Kwa kweli kifusi kinakaa kinaposhindiliwa vizuri na kikapata kupigwa na jua sana kuliko mvua. Mhe. Spika, mara nyingi kifusi kikipata mvua na magari yanapopita barabarani yanabeba kile kifusi, kwa hiyo utakuta haraka barabara inapata kuchimbuka mashimo na ikichimbuka mashimo ndio tatizo linapozidi, na yale mashimo kuwa makubwa na hatimaye ikasababisha *survey* nyengine.

Mhe. Spika, barabara hizi kwa kweli wananchi wamekata tamaa kwamba haitofikia kuweza kumaliza kwa barabara hizi. Vile vile tumesikia watu wa Kamati kwamba walikwenda kuangalia huo ujenzi unavyoendelea, na mfano

walioutoa ni kweli nakubaliana nao, kwamba ukisikia kama kuna mtu au Kamati inakuja basi watu watawekwa sawa angalau zile zana ziwekwe barabarani na zipigwe *start* na ziwekwe *silence* kwamba wakifika pale waone hii kazi wakati wowote itaendelea.

Pia hali kama hiyo, hata watu wetu wa Miundombinu na Mawasiliano kuhusu ujenzi wa barabara wanaposikia kwamba Mhe. Rais atafanya ziara ya kwenda eneo fulani, watu watakwenda na kufukia mashimo na mashine zitawashwa, ili ziara ile ipite tu au imalizike na wala hakuna jambo jengine litakaloendelea. *(Makofi)*

Kwa hivyo, sisi tumewafundisha watu na watu wametusoma na wao sasa wanafanya hivyo. Kwa hivyo, Mhe. Spika tutadanganyana mpaka lini, kwa sababu huu ni udanganyifu na wala si mwendo mzuri huu, wakati tayari serikali imeshalipa jambo la msingi ni usimamizi, ili barabara hizi ziweze kumalizika.

Ndani ya barabara hizi Mhe. Spika, wananchi walikatiwa miti yao mingi sana pamoja na kuvunjiwa nyumba zao na bado baadhi yao katika nyumba hizo hawajalipwa. Kwa mfano, barabara ya Wete/Gando maeneo ya Utaani hadi Junguni kuna wananchi hapa nyumba zao zimevunjwa hadi leo hii fedha zao bado hawajalipwa.

Sasa wananchi hawa karibuni wameshakata tamaa, kwa sababu wenzao wamelipwa na wao hawakulipwa fedha zao na familia hizi zinaishi vibaya, yaani hahe hohe, wanaishi katika nyumba ambazo si nyumba za kuishi binadamu, hivi Mhe. Waziri suala hili mpaka lini wananchi hawa watalipwa.

Vile vile kuhusu vipando vyao; kuna wananchi maeneo ya Kinyasini Bungala kwenda Mgogoni barabara ile ya zamani ya kawaida barabara hii iliachwa na ikapita eneo jengine. Sasa hili eneo lililopita barabara ni eneo ambalo lilikuwa na mikarafuu mingi sana na barabara ikachukua. Mhe. Spika, baadhi ya familia hizi tayari wazee wao ni marehemu na wala hawapo tena duniani na fedha zao hizi bado hawajalipwa, wengi katika hao tayari wameshakata tamaa kwamba fedha hizi zitalipwa.

Kutokana na hali hiyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, wakati atakapokuja kufanya majumuisho atueleze bayana kabisa na awaeleze wananchi kama watalipwa au hawatolipwa tena fedha zao hizi, ikiwa watalipwa tujue tarehe ngapi malipo haya yataanza, lakini kila siku tukiambiwa tu kwamba serikali italipa, hivi atalipa nani? Kwa hivyo, tunataka tupate jawabu ya msingi kuhusu vipando vya wananchi wetu hao waliopitiwa na barabara hii ya Wete/Konde na Wete/Gando.

Nikiendelea na mchango wangu sasa naomba nizungumzie barabara ya Ole/Kengeja. Mhe. Spika, barabara hii ina historia refu sana, kwa sababu hii barabara au sijui ilikuwa ni maneno ya watu au vipi, lakini tokea miaka ya 1980 inazungumzwa barabara hii ya Ole/Kengeja, miaka ya 1990 ikazungumzwa barabara ya Konde/Ole Ole/Kengeja kwa ajili ya kuunganishwa pamoja na kujengwa kwa barabara hizi, lakini kwa bahati ikajengwa ya Ole/Konde na ikakosa kujengwa ya Ole/Kengeja, kwa hiyo historia ya barabara hii ni refu sana.

Mhe. Spika, mpaka hivi sasa bado ninasema ni ndoto tu ya alinacha, kwa sababu huu ni mwaka wa tatu na mafanikio yake ni madogo mno na wala si mafanikio ya kuwatia tamaa wananchi wanaoishi katika ukanda huo; kwamba barabara hii itafanikishwa vizuri. Hata hivyo, huo ujenzi wake utakaojengwa si barabara ambayo itakuwa ni madhubuti.

Kwa maana hiyo, na mimi niungane mkono na wale waliosema kwamba kama serikali haijawa tayari kwa kujenga barabara kuziziba kwa mikono na barabara ambayo ina urefu wa kilomita 35, kwa kweli ni kuziharibu fedha za wananchi kwa sababu wananchi ndio watakaolipa kodi ya fedha hizi ambazo zitakopwa. Mhe. Spika, naiomba sana serikali kama haijawa tayari bado tutaendelea kuhesabu miaka, lakini ikijengwa barabara basi ijengwe barabara ambayo ina kiwango kizuri kabisa.

Mhe. Spika, niseme kwamba katika Mradi wa Barabara Vijijini Kaskazini Pemba na hii inapatikana kwenye ukurasa wa 11. Kwa kweli serikali imefanya jambo la maana sana kwa mradi huu kuweza kukamilika na kujengwa barabara hizi tano katika ukanda huu wa Kaskazini Pemba, ambazo barabara hizi zina urefu wa jumla wa kilomita 35.

Naomba nichukue fursa hii kupitia kwako Mhe. Spika, kuwaomba wananchi waliopitiwa na barabara hizi kwamba waziheshimu sana tena wazijali pamoja na kuzienzi, kwa sababu barabara ni gharama kubwa sana. Kwa hiyo, kitu kinapokamilika na kikakosa matunzo, kwa kweli itakuwa ni hasara kwa muda mrefu, pengine kama ni kodi basi

itakuwa haijamaliza kulipwa barabara ile itakuwa tayari imeshachafuka. Tunataka wananchi kwamba wazienzi hizi barabara na ziweze kuleta tija kwa wananchi wetu, ili mazao yao yaweze kufika katika masoko na kuweza kupata bei kwa wakati unaofaa.

Hata hivyo, ndani ya barabara hizi Mhe. Spika, bado kuna changamoto kubwa kwa baadhi ya maeneo katika malipo ya kuwalipa wananchi waliovunjiwa nyumba zao. Mhe. Spika, nikisema hivyo kwamba maeneo ya barabara inayotoka Mzambarauni kuja Mapofu Jimbo la Mgogoni maeneo ya Kinazini, hapa kuna wananchi wetu ambao bado hawajalipwa fedha za nyumba walizovunjiwa.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, umebakiwa na dakika tano.

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Spika, ahsante. Baadhi ya wananchi hao walifika mpaka wakaambiwa wafungue *account* benki, ili fedha zao zipitie kwa njia hiyo, lakini mpaka leo si kwa wale waliofungua *account* wala wale ambao hawajafungua hakuna hata mmoja aliyepata fedha hizo. Kwa hivyo, hapa bado wananchi hawa hatujawatendea haki.

Mhe. Spika, hili ni tatizo, na wananchi hawa ni Wazanzibari ambao ni miongoni mwa walipakodi, na jambo baya zaidi ni kwamba wenzao wengine tayari wameshalipwa na wao bado mpaka leo hawajalipwa. Kutokana na hali hiyo nina wasiwasi watu hawa wakasahaulika, kwa sababu na wao wanayo haki kama wenzao wengine.

Nikiendelea na mchango wangu sasa naomba nizungumzie kuhusu suala la Bandari ya Mpigaduri. Mhe. Spika, katika Bajeti ya Serikali juzi hapa miongoni mwa Wawakilishi wachache waliochangia Bandari hii ya Mpigaduri na mimi ni mmoja. Kwa hivyo, na leo narejea tena kuzungumzia suala la Bandari ya Mpigaduri.

Mhe. Spika, katika kuwekeza moja ni suala zima la Bandari. Kwa kweli nchi nyingi zimepiga hatua za maendeleo kwa kuwekeza mambo ya bandari, lakini hapa Zanzibar tunaona kama bandari sio kitu cha kuwekeza na tunatumia muda mrefu kutoyajali mambo kama haya. Bandari hii hata tukitizama maelezo ya kitabu hichi cha Mhe. Waziri, maelezo yake ni finyu sana, yaani ni maelezo machache, lakini Mwenyezi Mungu ajaalie uchache huu yawe na mafanikio zaidi.

Kwanza naomba niseme kwamba kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa ule utayari basi wao tayari wameshapeleka barua ya kuomba mkopo katika Benki ya *Exim* ya China, niseme kwamba Mwenyezi Mungu iwe kheri, lakini Mhe. Spika bandari hii serikali iache iliyonayo na ikaze nati na Mhe. Waziri wa Fedha akazane kabisa kuizungumza Serikali ya Jamhuri, ili mkopo huu uweze kupatikana na hii bandari ijengwe.

Kwa kweli itakapokamilika bandari hii serikali itaingiza mapato mengi katika nchi hii, pia wananchi watafaidika na nchi itapiga hatua. Kwa hivyo, kama hatukulitilia mkazo hili Mhe. Spika na kujengwa bandari hii, hivyo Zanzibar bado itakuwa tuko nyuma kimaendeleo na itakuwa kila kitu tunawakwamisha wananchi wetu kama vile kupandisha vitu bei hali ya kuwa uchumi upo kwa maeneo mbali mbali ya kuijenga hii nchi.

Mhe. Spika, nashukuru na ninaunga mkono hotuba hii.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, sasa naomba nimkaribishe Mhe. Farida Amour Mohammed, Mhe. Hassan Hamad Omar anajitayarisha na Mhe. Nassor Salim Ali pia anajitayarisha.

Mhe. Farida Amour Mohammed: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kutoa mchango wangu mdogo kuhusiana na Hotuba ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano.

Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ameniwezesha kusimama hapa leo katika Baraza lako na kwa ajili ya kutoa mchango wangu kidogo.

Vile vile naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa jinsi walivyoandaa kitabu chao hichi cha bajeti na Mhe. Waziri akaja kutosomea na tumekifahamu.

Mhe. Spika, tunakuomba utuvumilie Wawakilishi wako, nasema hivyo kwa sababu kila anayesimama hapa anazungumzia kuhusu suala la barabara tatu Kaskazini na Kusini Pemba, pia barabara za Unguja. Kutokana na hali

hiyo, tunakuomba utuvumilie kwa sababu jambo hili linatuuma sana, na ndio maana kila mmoja wetu anayesimama hapa analizungumza. *(Makofi)*

Pia nitawapongeza watu wa wizara hii kwa kukamilisha miradi ya barabara za vijijini Kaskazini Pemba. Kwa kweli naomba niwapongeze kwa sababu ya kukamilisha barabara hizi tena kwa ufanisi wa hali ya juu, kwamba inaonesha barabara zimekamilika nzuri, zinapendeza watu waliovunjiwa nyumba baadhi yao tayari wameshalipwa. Kwa hiyo, lazima niwashukuru kwa kufanya suala hili, kwa sababu mtu akifanya mema anatakiwa apongezwe, na akifanya mabaya ataambiwa kwamba amefanya mabaya. *(Makofi)*

Baada ya kuwapongeza katika barabara hizi tano za vijijini Mhe. Spika, sasa naomba nitoe lawama pamoja na masikitiko yangu ambayo haya nitaendelea kusikitika daima kwa barabara hizi za Kaskazini Pemba. Mhe. Spika, barabara za Kaskazini Pemba Wete/Gando na Wete/Konde zimekuwa kero na zimekuwa zinaleta athari kwa wananchi baada ya kupata faida, ambapo kuwa tegemeo la wananchi wa Kaskazini Pemba kwa barabara zile ilikuwa ni kupata faida na maslahi, lakini kinyume chake wamepata matatizo.

Mhe. Spika, ninasema hivi kwa sababu hii Kampuni ya *MECCO*, ambayo inatengeneza barabara hizi za Mkoa wa Kaskazini inaonesha hata mpangilio wao wa kazi sijui hawaufahamu au wameamua kutufanyia makusudi watu wa Kaskazini Pemba katika barabara hizi, sifahamu.

Kwa kweli watu hawa kifusi kimeshaingizwa sijui mara ngapi katika barabara zile na zikabakia katika kiwango cha lami, lakini baadaye kifusi kile chote kinapotea na hivi sasa wanachukua kifusi chengine kipya na hali hii ni kuitia hasara serikali kila siku kwa kuongeza kifusi hapa na pale.

Vile vile mbali na kutia kifusi hichi na kuitia hasara serikali pia wananchi wetu wanaingia hasara. Mhe. Spika, wanatengeneza barabara hizi kutoka Hoteli ya Wete mpaka Kuungoni na Wete/Gando. Katika kipindi cha nyuma kidogo wakati nilipokuwepo Pemba walitia kifusi katika maeneo ya mjini barabarani bila ya kutia hata yale maji angalau ya kuondolea vumbi.

Mhe. Spika, athari iliyotokea pale wenye maduka wote, wakati zinapopita gari ni lazima wayafunge maduka au zile biashara zao zote zinaharibika kwa vumbi, na wafanyabiashara wadogo wadogo wanaojitafutia riziki wengi wao wakiwa wanawake kwa kweli wanadhalilika sana.

Sasa kibaya zaidi katika hili ni kwamba barabara hizi hazimaliziki, kwa sababu barabara hizi zilikuwa na lengo la kumalizika kwa kipindi cha miaka mitatu, na hivi sasa ni mwaka wa nne na wa tano unakaribia, na kwa kweli watu wameshakata tamaa na kumalizika kwa barabara hizi.

Namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, wakati atakapokuja kufanya majumuisho, naomba anipe maelezo ya kina kabisa kuhusu barabara hizi lini zitamalizika angalau watu na wao wapate faida na maslahi katika barabara hizi.

Nikiondoka hapo sasa naomba niendelee katika eneo jengine kuhusu malipo ya nyumba za wananchi zilizovunjika na wala hazikaliki. Mhe. Spika, katika barabara ya Wete/Gando kuna magari yanayopita kwa kasi kwa sababu kuna fidia za namna nyingi, na suala hili kila kipindi ninaposimama hapa ninalizungumza, wapo watu waliovunjiwa kabisa.

Vile vile wengine walioathirika kwa kupita zile zana nzito za magari yaliyopita na watu hawa nyumba zao zimeathirika vibaya sana na wengine wameshazihama nyumba na wengine wamepangishwa katika maeneo mengine, na watu hawa wizara inawaambia haiwalipi mpaka barabara hizi zitakapomalizika. Kwa bahati mbaya sana barabara hizi hazimaliziki Mhe. Spika.

Kutokana na hali hiyo, ninamuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, wakati atakapokuja hapa kwa ajili ya kufanya majumuisho atueleze ni lini wananchi hawa walioharibikiwa na nyumba zao kwa kupita zile zana nzito za magari, lini watalipwa ili wapate mahala pengine pa kuishi na wastirike na familia zao. *(Makofi)*

Mhe. Spika, sasa naomba nizungumzie kuhusu Bandari ya Wete. Kwa kweli eneo hili la bandari hii wakati nilipokuwa nikichangia Hotuba ya (OR), Tawala za Mikoa na Idara Maalum nililizungumza suala hili la bandari hii.

Tangu kuzama kwa *MV. Spice Islander* imekuwa ile bandari imehamwa, Mhe. Spika nataka niseme kwamba Pemba walikuwa wakiitumia ile bandari katika kusafirisha bidhaa zao mbali mbali.

Sasa baada ya kuzama ka *MV. Spice,* sasa imekuwa ile Bandari haitumiki, sasa wananchi wetu wa Mkoa wa Kaskazini ambao kuwa ni wazalishaji wakubwa kama Jimbo langu la Ole Wilaya ya Wete na Majimbo mengine ya Kojani na sehemu nyengine yanazalisha embe kwa wingi na biashara hii wenyewe walikuwa wanaisafirisha kupitia Bandari ya Wete, ukitoka maeneo ya Gando ni wazalishaji wazuri wa mihogo na ndizi, hata katika kipindi hiki cha Ramadhani ni tegemeo sana kwa watu wa Kisiwa cha Unguja wananunua wa vitu kutoka huko, lakini kwa bahati mbaya sana kufa kwa Bandari hii ya Wete kumewafanya watu mpaka ule uchumi wao kupotea, kwa sababu sasa inabidi mtu asafirishe vitu apeleke Mkoani, akifika Mkoani gharama za usafiri zinazidi hasa pale Wete bado Bandari haijafanya kazi.

Mhe. Spika, kwa hivyo, naiomba sana serikali kupitia wizara hii atakapokuja hapa Mhe. Waziri, aniambie hasa wana mpango gani wa kuifufua Bandari hii ya Wete angalau meli ziweze kufunga gati pale na wafanyabiashara na wananchi wetu wa Zanzibar wapate kunufaika.

Mhe. Spika, nije katika baadhi ya utekelezaji wa ahadi za viongozi katika Wizara hii, kuna barabara ya Wawi/Vikunguni barabara hii ni miaka mingi Mhe. Rais wa awamu ya sita alitoa ahadi ya kutengenezwa ile barabara ya Wawi/Vikunguni, lakini ile barabara hadi hii leo hatujaona matengenezo yake, barabara ni mbovu sana na barabara inatoa vitu vingi kama ninavyokwambia Zanzibar yetu kila pembe inazalisha, sasa watu wanapata tabu kutoa vitu vyao kusafirisha kupeleka katika maeneo ya masoko. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri, atakapokuja hapa aniambie hivyo lini hii barabara nayo itaingizwa katika mpango wa kufanyiwa marekebisho.

Mhe. Spika, sasa kidogo naomba nije kwenye usafiri wa anga. Katika kitabu hiki nimekiangalia sana katika miradi hii ya utengenezaji wa Viwanja vya ndege, lakini kwa bahati mbaya sana sijaona eneo lililosema au sijaona bajeti ya eneo lolote lile inayosema itatengeneza Uwanja wa ndege wa Pemba. Wenzangu wengine jana walisema hapa na leo pia wameendelea kusema kuletwe mishumaa, lakini mimi sitosema paletwe mishumaa, mimi nasema ni aibu kubwa kwa serikali yetu kufika wakati Kiwanja cha ndege kikawa hata taa hakina, naiomba sana wizara hii na naiomba sana serikali kile kiwanja cha ndege cha Pemba kinakusanya mapato mengi, ndege nyingi zinakuja pale, lakini bado hawajakifikiria kukifanyia matengenezo ya aina yoyote.

Mhe. Spika, Zanzibar ni Unguja na Pemba, ndiyo iliyotengeneza kuwa Zanzibar. Kwa hivyo, naomba sana watakapofanya matengenezo, matengenezo yote ya Uwanja wa ndege mara hii nayaona Unguja, pale Pemba wale abiria pale pakukaa kitako kutafuta ile sehemu wanayotaka kusafiri kama ni wakati wa mchana hapakaliki kwa jua, ikinyesha mvua pale maeneo ya nje pale panapouziwa tiketi, basi kila mtu anaroa kwa mvua. Kwa hivyo, naomba sana Wizara iliangalie hili kwa jicho la huruma likiendelea kutengenezwa ule Uwanja wa ndege wa Pemba mapato makubwa yatakuja serikalini, sie raia tutapata faida kwa sababu tunakaa pahala pazuri, lakini serikali ndio inayopata mapato kutokana na viwanja hivi.

Mhe. Spika, naomba nimalizie kwa kusema barabara ya Ole/Kengeja ni nyimbo ya muda mrefu, kila siku inaimbwa, bajeti zote inaimbwa, lakini mategemeo yetu hatujayaona, sasa mimi naiomba serikali kama haijawa tayari katika hili wasiwatie watu tamaa kwa kusema tutajengewa barabara, lakini barabara yenyewe haionekani, naomba sana kama wana lengo la kujenga barabara ile, ijengwe kama hawana waondoe kwanza mpaka wasubiri siku ya uzinduzi waje waseme leo tunazindua barabara, lakini wasilete maneno ya kila siku barabara ya Ole/Kengeja na sisi watu wa Ole tuna hamu sana ya kujengewa ile barabara yenye urefu wa kilomita 35 nakushukuru. *(Makofi)*

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii kabla ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahu Wataala* aliyenijaalia kuwa katika hali ya uzima na afya inaniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasilino kwa uwasilishaji wake wa hotuba yake nzuri na mwanana kabisa ambayo tumeifahamu vya kutosha. Pia, nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa utendaji wake mahiri kijana aliyechipukia, lakini niwapongeze na watendaji wote wa Wizara hii.

Mhe. Spika, nikianza na mchango wangu, nitakwenda moja kwa moja katika ukurasa wa 40 wa kitabu hichi katika sekta ya usafiri baharini, sekta ya usafiri baharini ni muhimu sana kwa kuzingatia nchi yetu ni ya visiwa (kisiwa cha

Unguja na kisiwa cha Pemba), lakini tukiangalia hali ya usafiri ya Unguja na Pemba bado ni tete kabisa pamoja na huduma tunapata, lakini bado hali ya usafiri wa Unguja na Pemba ni tete, hii kwa sisi watu wa visiwa ni njia na njia yetu kuu ni hii ya baharini, wananchi wetu hawana uwezo wa kupitia njia ya anga, walio wengi tunatumia njia hii ya baharini. Kwa hivyo, sekta hii ni muhimu sana tukaiboresha na huduma zao zikawa sahihi ambazo ni nzuri kwa wananchi wetu.

Mhe. Spika, hapa hapa katika sekta ya usafiri baharini kuna usumbufu sana wa upatikanaji wa tiketi za wasafiri wanaokwenda Unguja na Pemba, hapa pamekuwa na kikwazo kikubwa sana, wananchi wetu wanatoka masafa kufuata tiketi sehemu zinazouzwa, lakini kunakuwa na matatizo makubwa sana, mtu anaweza kutoka Matemwe akaja mjini kufuata tiketi akienda katika Ofisi husika akaulizia tiketi, akaambiwa bado, anaambiwa zunguruka na ukizunguruka kidogo ukiuliza tena, unaambiwa tiketi zimekwisha, kulikoni hapa! Kuna tatizo kubwa sana, tunawaletea wananchi wetu usumbufu wa kutosha jambo ambalo haliingii akili kwa wananchi wetu kuwatesa.

Mhe. Spika, si kwamba haitoshi ukiangalia hizi tiketi, zimekuwa na ulanguzi wa kutosha, hapa ndipo kwenye matatizo makubwa na hali hii inaendelea siku hadi siku na naomba hapa nitoe mfano ulio hai, mimi mwenyewe binafsi jana nilikuwepo Bandarini kwenda kukata tiketi ya mtu wangu ambae nilikuwa namsafirisha katika Ofisi ya shirika la meli, nikaambiwa tiketi zimeisha, lakini hapo hapo akatokea kijana akanambia kama unataka tiketi mimi ninayo na thamani yake ni shs. 25,000, nadhani tiketi hii inauzwa shs. 15,000 au 17,000 za uhalali, lakini ananiambia Shs. 25,000, ulanguzi huu ambao ni unasababishwa, mimi nasema ni rushwa na rushwa ni adui wa haki, ndio hivi inavyokwenda, ni tatizo kubwa sana na hili tumelisemea sana hata katika bajeti iliyopita, lakini suala hili linaendelea. Mimi sidhani kama serikali inashindwa kulisimamia hili na ikawa limeondoka moja kwa moja, hii ni dharau na inaonekana kwamba watu wana maslahi yao na ingekuwa hakuna maslahi, basi shughuli hii ingelikuwa imemalizika, zamani mbona Darajani walivyoamua kuondoa watu wameweza, serikali imeweza kabisa, kwa nini watu wachache waliopo pale wasiondoke na kwenda kupata riziki zilizokuwa halali? Ni tatizo.

Mhe. Spika, naomba suala hili lifuatiliwe, watendaji wafanye kazi kwa kina, hili waliondoe, mimi hali yangu afadhali si kama wananchi wa hali ya chini, nikitaka safari naweza kulanguliwa na naondoka, si utaratibu, lakini uwezo huo wa kuipata tiketi hiyo, ninao uwezo, lakini mwananchi wa kawaida hana uwezo huo ameshajipangia tiketi Shilingi elfu kumi na tano na elfu tano ni nauli ya gari, lakini ukienda pale unalanguliwa elfu ishirini na tano unazipata wapi mwananchi masikini. Mhe. Waziri, atakapokuja atuelezee kwa kina kama tatizo lile litaondoka, bihairi ya hivyo, pataruka kivumbi hapa katika bajeti yake.

Mhe. Spika, sote ni mashahidi kuwa tumepata majanga mbali mbali kwa usafiri wa baharini, naomba hii isisahaulike, tukajisahau moja kwa moja, kwa sababu siku zote sisi ni wananchi wa kupita baharini, basi tusisahau, naomba nitoe mfano kwamba sasa hivi kutakuwa na tatizo la usafiri kutoka Pemba kwenda Tanga na kutoka Tanga kwenda Pemba, ni matatizo hakuna usafiri, wananchi wanaotoka Pemba kwenda Tanga hawapati usafiri wa uhakika na wanaotoka Tanga kuja Pemba hawapati usafiri wa uhakika, nadhani sote tunajua kwamba meli zetu hizi za serikali ambazo za Shirika la meli zilikuwa zinafanya safari yake hapo nyuma kwenda Tanga na Pemba ikiwemo *MV*. Maendeleo na *MV*. Mapinduzi, wakati huo tulikuwa nazo zote zilikuwa zinafanya safari, naiomba serikali japokuwa mara moja kwa wiki, basi ifanye safari za Tanga kwa sababu pale kuna wananchi wetu wanaofanya safari za Tanga na Pemba itakuwa si vyema na hatukuwatendea haki bila ya kupata usafiri wa uhakika kama wanavyopata watu wa Unguja na Pemba tukizingatia kwamba vyombo vilivyokuwepo pale ni majahazi na majahazi tumekataza wasisafirie. Kwa hivyo, kuna haki na wao kupelekewa meli japo mara moja kwa wiki ikenda mara moja Tanga.

Mhe. Spika, tunamshukuru sana mfanyabiashara Salum Bakharesa kwa huduma anazotoa ambazo ni Kampuni binafsi, lakini siku zote nasema penye uzuri hapakosi kasoro, mfanyabiashara huyu anatusaidia sana kuhusu usafiri wa Unguja na Pemba kwa meli yake hii moja *Azam Sealink*, lakini meli hii imekuwa ni kikwazo kikubwa sana kwa wananchi wanaoondoka Unguja kwenda Pemba, inaondoka muda sio muafaka, meli hii inasubiri abiria kutoka Dar-es-salaam wawapakie meli ya *Azam Sealink*, ni matatizo muda wa kuondoka, tumeondoa safari za usiku za baharini, tumeweka safari za usiku katika njia kavu, ni matatizo.

Mhe. Spika, meli zinazotoa huduma ni mbili tu, nasema ni Meli ya *MV*. Maendeleo na *Azam Sealink* kwa Pemba, Kilimanjaro inakwenda siku moja moja na siku hizi kabisa imeshakatisha haiendi, sasa tuwafikirieni wananchi wanakwenda sehemu mbali, kuna watu wanapanda meli hapa mpaka Mkoani wanakwenda Makangale au Msuka, huyu lazima afike saa mbili mpaka saa tatu usiku nyumbani kwake, lakini kama meli itaondoka saa moja au saa moja na nusu itafika na wakati *Azam Sealink* inatembea masaa sita, ikiondoka hapa saa mbili inafika saa nane, saa

nane mpaka kumi na mbili natumaini watu wameshafika majumbani, lakini kuondoka hapa saa tatu, nne mpaka tano, haina muda maalum, inawatesa wananchi.

Mhe. Spika, hili ni jambo la kuliangalia kweli kweli, tunawatesa wananchi wetu sio kwamba wote wanafikia mjini, watu wengi wanakwenda mashamba. Kwa hivyo, tunamuomba Mhe. Waziri, atufikirie kabisa kwa sababu sekta ya usafiri baharini ndio wanaosimamia jambo hili tunaomba ikimaliza bajeti hii ratiba iwe imeshapangwa vizuri, wananchi waondoke kwa wakati, hasa ukizingatia bahari asubuhi siku zote inakuwa ni shuwari, lakini ikifika saa nne, saa tano bahari inachafuka na ukiona asubuhi imechafuka, basi huko hakwendeki, lakini kama unaondoka mapema saa nne, saa tano, umeshakata mkondo wa Nungwi ule, lakini kama itaanza kuchafuka hapa Bandarini, basi hakwendeki, ni mdharuba huo. Kwa hivyo, tunaomba meli ya *Azam Sealink* izingatie hilo na ipangiwe muda muafaka.

Mhe. Spika, mimi niwapongeze sana Shirika la Bandari kwa utendaji wao mzuri hasa kwa kushirikiana na huyu mfanyabiashara kwenda kututengenezea mambo mazuri yale tunayoyaona, lakini hapa napo tuwaambie kuwa huyu mfanyabiashara anafanya vitu vizuri kama vile, lakini mpaka Ofisi yake leo haijulikani pale pa *manager* tungemshauri, hana Ofisi inayolingana na hadhi ile aliyotengeneza sehemu ile pale, hebu muoneeni huruma, mpeni sehemu ajenge Ofisi ambayo inatambulikana, kunakuja watalii mbali mbali pale na huyu bwana jina lake ni kubwa na ukija kuangalia Ofisi inayokatwa tiketi za Bakharessa, ndio pale ni tatizo. Naomba Mhe. Waziri, pamoja na watendaji wake na serikali kwa ujumla ishirikiane wampe sehemu.

Mhe. Spika, lakini vile vile, niseme tu nidhamu ndogo Bandarini, baadhi ya askari wetu wanaosimamia katika sehemu ya mageti haya ya Bandari tunayopita, nidhamu inakuwa ndogo, mimi napendelea sana kwenda Bandarini, nilikwenda kusafirisha mama mkwe wangu pale juzi nikafika kwenye geti pale na gari yangu mwenyewe nikamuomba askari, naomba kumpeleka mama yangu ndani ya meli ya *MV*. Maendeleo wakanambia nafasi hakuna sehemu magari yamejaa, nikaomba na kupiga magoti kuzidi kuomba *Wallahi* hakuniruhusu.

Mhe. Spika, lakini kwa bahati mbaya Mwenyezi Mungu kataka kumhukumu mnafiki yule ikaja gari la lori mbele kuna mwanamke, gari ile ikapita na mimi ndio nikapita, lakini nilimwambia *Wallahi* huyu hapiti, naomba ukanishitaki ndio atapita, lakini kama sijaja kuchukuliwa na askari hapa siondoki, huyu nani na mimi nani, akanambia huyu mfanyakazi nikamwambia na mimi nimekuomba kwa ridhaa zote mpaka akaja mtu akamwambia yule ni Mheshimiwa, hajasema basi nikamwambia nimekwambia mimi ni Mheshimiwa, nakwenda kumpeleka mama yangu, nampeleka safari. *Wallahi* matatizo hayo yanatufika, ndio maana Mhe. Waziri wa Fedha akapigwa mtama hapo Uwanja wa ndege, Mhe. Subeit mara mbili ameshashikwa koo na mimi ni shahidi na alisema sitokwenda tena sasa Mhe. Waziri wa Fedha ndio huyo yameshampata hapo na mwengine bado wewe Mhe. Spika, sijui wewe itakuwaje. Nidhamu katika sehemu ya utendaji wa kazi zote ni sehemu tu hizi, cheo ni dhamana, leo upo kesho hupo.

Mhe. Spika, lakini niseme tu zile raha tunazoziona katika Bandari ya Unguja, basi na kule Pemba tunataka tuzione sehemu ya Bandari ya Pemba pale Mkoani, wananchi wetu hasa ikifika wakati wa masika mvu inakuwa ni shida kutoka pale mpaka ukafika kwenye jengo mizigo mingi inaharibika, pamoja na jua kali na watoto. Kwa hivyo, miundombinu iliyofanywa hapa Zanzibar Unguja, basi na kule Pemba nayo ifike.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu, sasa naelekea moja kwa moja Shirika la meli katika ukurasa wa 47, kifungu 109, imeelezewa katika Shirika la meli kwamba meli zetu ni chakavu, mimi nakubaliana na wewe kwamba meli zetu ni za siku nyingi na chakavu, lakini katika kitabu hiki hakikuelezea upatikanaji wa meli yetu mpya, hakutupa hata matumaini na wakijua meli zetu ni chakavu, wakati wowote meli ya Maendeleo inaweza kutembea na ikazimika baharini kwa uchakavu wake. Kwa hivyo, Mhe. Waziri, atakapokuja hapa atueleze ni lini matumaini ya kupatikana meli yetu mpya, wakati wizara zote zilinyofuliwa mafungu yake na kupelekwa katika upatikanaji wa meli mpya.

Mhe. Spika: Una dakika tano.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Spika, nikielekea katika mradi wa ujenzi wa barabara vijijini Kaskazini Pemba, na mimi nashukuru kama Mhe. Rufai alivyoshukuru na kuwapongeza sana kama mradi ule umekamilika na tunaendelea vizuri, kutoka Chwale/Kojani, pale sasa hutembei kwa mguu, vigari saa 24 vipo vikeri, sasa tunatembea kwa muafaka muda wowote mtu akitaka safari gari zipo, haya ndiyo maendeleo, lakini bajeti iliyopita *Hansard*

yangu hii ipo, nilieleza barabara ile katika kupita wengine wanafaidika na wengine wanaathirika. Nilimueleza hapa na nikamwambia nikamtajia majina kama watendaji wake wachukue majina hayo ili wawafanyie kazi. Sijaona nguvu yoyote inayotumika au kitendo haki wananchi ambao hawakufanyiwa makisio katika upitishaji wa barabara ile ambao wameathirika.

Mhe. Spika, ndani ya *Hansard* hii wamo watu hao walioathirika na barabara na mpaka sasa hivi taratibu zote za kisheria wamepitia, lakini *Wallahi* hakuna chochote kinachofanyika. Majina yapo hapa tena nataka nikutajie watu 14 hawa, lakini naomba kwa sababu katika *Hansard* hii yamo, nikimaliza shughuli au mfanyakazi achukue ampe Mheshimiwa yule awafanyie kazi ili wapate haki zao za kisheria, ni hasara kubwa.

Mhe. Spika, hata juzi katika huo mtaro uliochimbwa pale, Mkuu wa Mkoa yeye mwenyewe ni shahidi wa Kaskazini Pemba alikwenda pale palitokea matatizo makubwa sana, maji yamefungwa upande mmoja yakabomoa kule. Kwa hivyo, sisi hatusemi kwa utashi, tunafanya utafiti wa kutosha. Naomba watu 14 hawa Mhe. Waziri, pamoja na watendaji wako muyafanyie kazi na wapate haki zao zinazostahiki. Sina haja ya kuwataja tena majina yapo hapa.

Mhe. Spika, nikitoka hapo kwa kumalizia nizungumzie katika Mamlaka ya Viwanja vya ndege na hasa kwa leo nitazungumzia katika kiwanja cha Pemba. Kiwanja cha Pemba imekuwa ni hadithi kubwa sana kama kila sikui kitafanyiwa matengenezo ambayo yatastahili kama ni Kiwanja cha ndege, lakini mimi nasema pale tunamdhalilisha Mhe. Marehemu Muasisi wa nchi hii (Mhe. Abeid Amani Karume) kwamba ukipinda tu ukitoka Chake Chake mjini pana bao linaonesha Karume *Airport* kuelekea Uwanja wa ndege huko. Sasa ili tulitukuze jina hili tufanye mambo mazuri au mimi naiomba serikali jina lile iliondoe pamoja na Wizara husika, tunamdhalilisha yule mtu wetu, ambaye ni muasisi.

Mhe. Spika, yeye Mhe. Waziri alipokuwa katika Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi alikuwa *challenge* kweli kweli, Mheshimiwa huyu na alisema kama hamna uwezo wa kutia taa, basi hata ile mishumaa ya Ujerumani mtuletee. Sasa leo Mhe. Waziri rungu umepewa wewe, tunaomba ufanye kazi utuletee heshima katika Uwanja wa ndege wa Pemba.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo kwa kujali muda wako, naomba niishie hapo na ujumbe umefika na yasibaki katika karatasi katika maandiko yafanyiwe kazi ndio tutajisikia raha. Kitu chochote cha malengo unachokipanga lazima ukifanyie kazi kama hujakifanyia kazi si lolote si chochote hata ukija na vitabu vingapi. Kwa hivyo, tunaomba tunayoyazungumza hapa hatuzungumzi kwa kusema tu kwa sababu tunapenda, tunazungumza kwa sababu ni maendeleo ya nchi yetu yafanyiwe kazi.

Mhe. Spika, ninakushukuru. Ahsante sana.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Spika, ahsante na mimi kunipa nafasi ya kuweza kuchangia kidogo hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano. Kwanza na mimi nichukuwe fursa hii kumshukuru sana na kumpongeza sana Mhe. Waziri, pamoja na Naibu wake, watendaji wake Katibu Mkuu, Wakurugenzi, kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya. Aidha, niipongeze sana Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika kuifanyia kazi nzuri kwa kuleta maendeleo kwa Wazanzibari kwa visiwa vyote viwili vya Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, nianze na mradi wa ujenzi wa barabara ambayo inaanzia katika ukurasa wa 8. Niseme kwamba kwa kweli serikali imefanya kazi nzuri hususan katika barabara za vijijini hasa Kaskazini Pemba ambapo miradi hii imemalizika. Barabara hizi ambazo zimeoneshwa hapa ikiwemo barabara ya Bahnasa, Daya Mtambwe, Chwale/Kojani, Kipangani/Kangani, Mzambarauni/Mapofu. Kwa kweli nichukuwe fursa hii kuipongeza serikali na hii inaonesha wazi kwamba Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inapeleka maendeleo kwa pande zote mbili, yaani Kisiwa cha Unguja na Kisiwa cha Pemba na haya yote ndio matunda ya Mapinduzi Matukufu ya mwaka 1964.

Mhe. Spika, nikitoka hapo, nije katika mradi wa barabara ya Ole Kengeja. Wenzangu wamezungumza sana, wamesema mengi kuhusiana na mradi huu wa barabara wa Ole/Kengeja. Wewe ni shuhuda tumekuwa tukipiga kelele sana na serikali imekuwa kila mwaka ikielezea kuhusiana na mradi huu wa Ole/Kengeja, ambao ni barabara inayotoka Ole/Kiwani/Kengeja.

Mhe. Spika, wananchi wa maeneo haya, Ole, Kiwani, Kengeja wana hamu kubwa kuona kwamba barabara hii inaanza na inamalizwa kwa muda muafaka ambapo na wao na waonje matunda ya Mapinduzi Matukufu ya mwaka

1964. Sasa ningeomba sana Mhe. Waziri na watendaji wake na serikali kwa ujumla kuhakikisha kwamba barabara hii inaanza na inamalizika haraka iwezekanavyo ili wananchi wafaidike na matunda ya Mapinduzi Matukufu ya mwaka 1994.

Mhe. Spika, nije katika mradi wa barabara zinazoingia mjini Unguja. Barabara ambazo zinaingia mjini Unguja, ukianzia barabara kutoka Tunguu kuja Fuoni mpaka Magomeni, barabara hii kutokana na hali ilivyo na matumizi yalivyo hivi sasa, barabara hii ni hatari na inahitaji kufanyiwa matengenezo ili kuondoa usumbufu kwa wananchi wanaokwenda Makunduchi, Muyuni, Ndijani na Tunguu yenyewe.

Mhe. Spika, ukienda katika barabara hii, hali halisi ya barabara hii ni mbaya, ajali nyingi. Kwa hivyo, ningeiomba Wizara kuhakikisha kwamba barabara hii inatengenezwa na kuwaondolea wananchi matatizo katika barabara hii.

Mhe. Spika, lakini nije katika mradi wa barabara wa vijijini Unguja. Kuna barabara ambayo imekuwa ikizungumziwa kama barabara nyengine kwa miaka mingi, ikiwemo barabara ya Kijini ambayo iko Mkoa wa Kaskazini. Barabara hii kwa muda mrefu sana Mhe. Panya ananambia iko katika wilaya yake, barabara hii iko katika hali mbaya. Ningeiomba wizara kuhakikisha kwanza barabara hii, kwa sababu imezungumzwa kwa miaka mingi, iko hali mbaya na kweli ni wajibu wetu sisi kuzisemea barabara hizi, kwa sababu wananchi wamekuwa wakilalamika sana kuhusiana na barabara hizi na halikadhalika barabara hizi zimo katika ilani ya Chama cha Mapinduzi. Kwa hivyo, nimuombe sana Mhe. Waziri, kuhakikisha kwamba barabara hizi zinajengwa ili kuondoa usumbufu kwa wananchi wetu.

Mhe. Spika, nije katika barabara za mjini kabisa, niishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambao jana tu wizara husika inayohusiana na barabara ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imefanya ziara katika barabara za mjini hususan katika Mji Mkongwe na hii inaonesha dhahiri kwamba Muungano wetu huu wa serikali mbili unaleta tija katika kuleta maendeleo kwa Wazanzibari na Watanzania kwa ujumla.

Mhe. Spika, kwa sababu barabara ambazo ziko katika Mji Mkongwe na Mji Mkongwe unaambatana pia na barabara ya Michenzani, Rahaleo, Magomeni. Sasa niwaombe wizara kwa sababu katika mradi ambao unaendeleza kutengeza barabara za mjini zikiwemo katika barabara hizi ambazo zinaingia katika mjini. Kwa hivyo, kuna matengenezo ya kuweka viraka katika maeneo ya mjini na niiombe sana wizara kuhakikisha kwamba viraka vile ambavyo vinatiwa katika barabara hizi za mjini, basi zitiwe kwa utaalamu na visiwe viraka ambavu vinaleta usumbufu katika barabara zetu.

Mhe. Spika, nikitoka hapo, nije katika Shirika la Bandari. Nimpongeze sana Mkurugenzi wa Bandari kwa kazi nzuri anayoifanya na kwa kweli ni wajibu wetu kumshukuru na kumpongeza Mkurugenzi wa Bandari, kwa sababu mambo ambayo yamefanyika pale katika Bandari yetu ni mambo mazuri na yanahitaji kuyaendeleza na yalete faida katika nchi yetu na wananchi wetu kwa ujumla.

Mhe. Spika, lakini katika Shirika la Bandari kuna wafanyakazi ambao tunawaita vibarua ambao wanafanya kazi kwa siku, lakini wafanyakazi hawa ambao wanakuwa wanafanya kazi kwa vibarua wanakua hawana uhakika wa kazi ile na wananchi wetu wanategemea kufanya kazi zile ili kuendesha maisha yao. Sasa ningemuomba Mhe. Waziri, kuhakikisha kwamba wafanyakazi wale wanaofanya vibarua pale, basi wanaajiriwa na kama hakuna nafasi ya kuajiriwa, basi kuwe na utaratibu mzuri ili kuweza kuendeleza maisha yao na kumekuwa na malalamiko mengi wafanyakazi wale wanaofanya kazi pale kwa njia hii ya vibarua ambao wanakuwa hawana uhakika mtu anatoka Fuoni au Muyuni, anakuja kufanya kazi pale akiambiwa kazi hakuna anarudi nyumbani.

Mhe. Spika, kwa hivyo, inakuwa ni usumbufu na wanakuwa hawana uhakika wa kuendesha maisha yao. Ningemuomba Mhe. Waziri, kuhakikisha kwamba na akija atueleze ni utaratibu gani mzuri ambao ameuweka ili kuhakikisha kwamba usumbufu kwa wananchi wetu unaondoka ili kuweza kujisaidia katika kuendeleza maisha yao.

Mhe. Spika, nikitoka hapo, nije katika Mamlaka ya Viwanja vya ndege. Wenzangu wamesema hapa kuhusiana na hali halisi ya Uwanja wa ndege, mengi yamesemwa. Namshukuru sana Mhe. Waziri wa Fedha ametuelezea mipango madhubuti ambayo Serikali yetu ya Mapinduzi Zanzibar katika kuendeleza Uwanja ule wa ndege, lakini mimi niseme kwamba cheo ni dhamana na tunahitaji sisi ikiwa viongozi tujitahidi sana katika kuongoza wenzetu, hususan katika sehemu nyeti au sehemu ambazo zinaleta maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Spika, laiti kama ingelikuwa si uongozi wako mahiri, ingekuwa tuna malalamiko mengi, lakini tumekuwa tukikupongeza wewe kutokana na usimamizi wako na uongozi wako mzuri. Halikadhalika tumekuwa tukimsoma vizuri sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, katika kuongoza na kuleta maendeleo katika nchi yetu hii ya Zanzibar. Sasa hawa watendaji ambao wanapewa dhamana hususan katika Mkurugenzi wa Uwanja wa ndege, ile ni mali ya serikali ni mali ya wananchi amepewa dhamana ni vyema kwamba aongoze wenzake katika njia ambazo zilizo bora na sio kwamba kuendesha taasisi ile kama ya mtu binafsi.

Mhe. Spika: Unazo dakika tano.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Spika, matatizo yapo mengi katika Uwanja wa ndege, malalamiko yako mengi, wenzangu wamesema hapa,wenzangu wameeleza kuhusiana na kadhia ambayo tumekuwa tukiipata katika Uwanja wa ndege. Sisi Wajumbe wako tumekuwa tukipata mapokezi mazuri wakati tunaposafiri katika Viwanja vya ndege vya Dar-es-salaam, vya Kilimanjaro na sehemu nyengine yote ya Tanzania kuliko ambayo tunayapata katika Uwanja wa ndege huu wetu wa Unguja na nimuombe sana Mhe. Mkurugenzi abadilike na ajirekebishe ili tuendane na hali halisi ya uongozi wetu wa Uwanja wa ndege.Baada ya kusema hayo, niunge mkono hotuba hii kwa asilimia 100, lakini na maelezo ambayo nimeyazungumza mengine nataka majibu. Ahsante sana.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nachukua nafasi hii kwanza kukushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia hotuba hii na naomba univumilie sana kwa sababu dakika 20, kwa kweli ni chache, lakini nitajaribu kujiweka sawa ili nifikie malengo yaliyokusudiwa.

Mhe. Spika, kwanza nilipongeze Shirika la Bandari, maana simpongezi Waziri kwa sababu hii hotuba siiungi mkono, lakini nalipongeza Shirika la Bandari kwa mambo mawili makubwa. Kwanza Shirika la Bandari walivuka malengo ya ukusanyaji, walitwambia kwamba walikadiria kukusanya bilioni 12.81 hadi mwezi Machi, lakini hadi mwezi Machi Bandari wamekusanya bilioni 14.6 sawa na asilimia 114. Kwa hivyo, hii kwangu mimi ni pongezi kubwa kwamba Shirika la Bandari limeonesha sura halisi ya uchapakazi wa utendaji makini na kwamba wameongeza mapato.

Mhe. Spika, lakini pongezi ya pili niwapongeze kwamba licha ya kukusanya fedha hizo wameendelea kutumia fedha hizo kwa mpango mzuri.Walikadiria kutumia bilioni 10.63 hadi mwezi Machi, wametumia bilioni 10.47 asilimia 98 ya kipindi hiki cha makadirio. Kwa hivyo, Shirika la Bandari ninalipongeza kwa sababu wamekusanya kwa kiwango kikubwa zaidi, lakini pia, matumizi yao yameenda sambamba na makadirio ambayo waliyakusudia.

Mhe. Spika, pongezi ya pili, nimpongeze mradi wa barabara vijijini barabara tano Kaskazini Pemba chini ya *MCC*. Barabara hizi zimefikia kiwango kwa sababu ninajua *MCC* walisimamia wao wenyewe, ndio maana zimejengwa kwa kiwango na pia zikatimia zikajengwa kwa wakati muafaka. Kwa hivyo, niwapongeze sana *MCC* na labda niseme kwamba serikali kwa hapa wametuvika nguo, kwa sababu ninaamini wangekabidhiwa wao ungesikia mara hali ya hewa ni chafu, vifaa vimeharibika kuna mashaka mengi, lakini *MCC* kwa kujua hili, walisimamia wenyewe barabara hizi tano na hadi hivi leo wenzetu wa Kaskazini Pemba wanasifia kwamba zimekamilika barabara hizi tano kwa kiwango kizuri na kwa ufanisi mkubwa.

Mhe. Spika, baada ya pongezi hizo sasa niseme kwa jumla kwamba mimi sitounga mkono hotuba hii. Sitounga mkono kwa sababu nikiunga mkono, nina hakika kama ninajidhulumu na nawadhulumu wananchi wa Jimbo la Kiwani walionileta hapa.

Mhe. Spika, bajeti hii maelezo ya Mhe. Waziri, imejieleza wazi kwamba Wizara yake imeshindwa kazi na naomba nithibitishe kwa takwimu ambazo wametupa.Bajeti ya mwaka jana 2013/2014 Mhe. Waziri, alitwambia kwamba wamepanga kutumia bilioni 20.092 kwa bajeti nzima, ikiwa bilioni 5.19 ni kazi za kawaida na bilioni 19.9 ni kazi za maendeleo, lakini walikadiria kukusanya milioni 406.2 makusanyo ya jumla, lakini mwaka huu ili kuthibitisha kwama kazi imewashinda wametwambia wanatuomba bilioni 14.077, kazi za kawaida ni bilioni 5.67 na kazi za maendeleo ni bilioni 8.4, ni punguzo la bilioni 6 za mwaka jana. Kwa hivyo, mwenye akili timamu ikiwa hukutoka taka kwa pipa la maji, utatokaje nongo kwa ndoo ya maji, maana bajeti ya mara hii imeshuka kwa bilioni 6, bajeti ya maendeleo ni dhahiri kwamba hakuna ambacho kuwa kitafanyika kwa mujibu wa tafsiri ya hesabu zao wenyewe walizotuletea.

Mhe. Spika, kwa msingi huo, anayesifu na asifu, anayetetea na atetee, lakini tafsiri ya hesabu zao wenyewe na siyo hesabu za Hija kwamba bajeti yao ina upungufu wa maendeleo ya bilioni sita za mwaka jana, ni dhahiri kwamba hakuna ambacho kitafanyika kwa mujibu wa tafsiri ya bajeti zao.

Mhe. Spika, niseme bila ya aibu kwamba wizara hii kwenye wizara 16 za SMZ, wizara hii inaongoza kwa ubaguzi na nataka niseme kwamba hii wizara inaongoza kwa ubaguzi. Kwanza inaongoza kwa ubaguzi wa Unguja na Pemba, lakini pia, inaongoza kwa ubaguzi wa Pemba Kaskazini na Pemba Kusini na naomba ni-*prove* hizi hoja zangu. Ndiyo na-*prove* hoja zangu nitapinga hoja zangu.

Mhe. Spika, hoja yangu ya kwanza watwambie ni barabara gani ya Kaskazini Pemba au ya Unguja iliyojengwa kwa mtindo ule ule wa kutandika (kusizima) watwambie, wafadhili hao wanaona Kusini Pemba tu ni ubaguzi wa kwanza, ni kwa nini? Kwa sababu wizara hii ukiacha waziri aliyekuja juzi hakuna watendaji wa Kusini Pemba. Kwa hiyo, mtaendelea kutukandamiza kwa sababu hamna watetezi katika wizara.

Mhe. Spika, tumejengewa barabara sita Kusini Pemba mwaka jana Mhe. Rais alizindua wakati wa Sherehe za Mapinduzi, leo zote ni mbovu unawaambia Mfuko wa Barabara sasa wakatengeneze. Kama mko makini kweli barabara hizo sita ambazo mmejenga na mmezindua mwaka jana leo zote ni mbovu *value of money* ya sekta za umma hazipo. Ni ubaguzi ambao wanafanyiwa wa Pemba wenzetu, wananchi wenzetu wa Kusini Pemba kwa kuleta miradi ambayo kuwa haina ufanisi, leo wanatwambia hapa wanataka kujenga barabara ya Ole/Kengeja kwa mtindo ule ule wa kusizima. Ningewashauri Wawakilishi wenzangu hasa wa Kusini Pemba tukataeni usanii huu wa kipumbavu, ni usanii ambao unawadanganya wananchi na kuleta hasara katika Taifa.

Mhe. Spika, barabara ya Ole/Kengeja kilomita 35 ikijengwa mtindo ule wa *labour power*, ni dhahiri Wazanzibar walioko Pemba watalishwa hasara kwa mara nyengine ya pili. Wameshindwa barabara ya Kengeja/Mtambile, barabara ya Mtambile/Kangani, barabara ya Kenya/Chambani, zote tano barabara ni mbovu kwa miaka miwili mfululizo. Leo wanatwambia kwamba watajenga barabara ya Ole/Kengeja kwa mfumo ule ule na hawa wamezoea, *PRISMO* walipewa kazi ya Mkoani/Mtuhaliwa wakatuharibia, lakini haikupelekwa *PRISMO* Kaskazini Pemba, anapelekwa *ACC*, anapelekwa *MECCO* na wengine. Kwa hivyo, ni ubaguzi wa kimaendeleo ambao unafanywa chini ya Mhe. Waziri Rashid Seif. Niwaombe sana Wawakilishi wenzangu mwenye akili timamu na aliye Mwakilishi wa watu asiunge mkono hotuba hii ya Mhe. Waziri.

Mhe. Spika, jengine ambalo niliseme barabara ya Mgagadu/Kiwani, Mhe. Waziri kwa heshima kubwa leo umetudanganya na naomba ni-*prove* kwamba umetudanganya amesema kwenye *page* ya 25 *paragraph* 56 kwamba barabara hii imekamilika kwa hatua ya kifusi chote, maana yake nini? Maana yake barabara hii imefanywa *sub-grade*, baadae ikafanywa *sub-base*, baadae na *base* ni uongo ambao haukubaliki. Kitaalamu ili barabara ifanywe hivyo, maana yake *sub-base* ni *centimetre 20* au *inches 6* mpaka 8 na *base* ni *centimetre* 15 au 6.

Mhe. Spika, naomba uturuhusu leo twende Kiwani barabara ile ikachimbuliwe ikiwa imefanyiwa hivi, mimi leo nitajiuzulu hapa hapa Zanzibar na kama waziri anatudanganya leo na yeye akubali kujiuzulu. Mnadanganya watu kwamba mmefanyia hatua zote za kifusi, si kweli, wamepaka kifusi juu juu na leo kuna mvua tayari imekomba chote kifusi, kwa nini mtufanyie hivi? Kwa nini mtufanyie usanii? Kwa nini mtudanganye watu wazima? Hii si bajeti ambayo inapaswa kupitishwa na wawakilishi walio makini, labda mtu awe kazoea kupoteza njiani haki za watu, ndiyo anapitisha bajeti hii.

Mhe. Spika, Mkanyageni/Kangani eti, badala ya Kiwani mara hii imetajwa Kangani, leo tunaambia *MIVARF* ndiyo watajenga. *MIVARF* ni mradi ambao watajenga barabara kwa kifusi cha juu juu. Kwa hivyo, ni kutoka lami ya SMZ, sasa ni kifusi cha juu juu, ni usanii mwengine ambao kwa kweli unasikitisha sana. Kwa hivyo, Wawakilishi wenzangu niwaambie kwamba hawa watu bwana ama kazi imewashinda, ama ni dharau ambayo wanatuonesha na kama kazi imewashinda, basi wapumzike na mwenye kuamua kupumzika siyo tu Mhe. Rais peke yake na Wawakilishi wanaweza kumuamua Mhe. Rashid apumzike kwa kumpigia kura ya kutokuwa na imani kwa sababu ameshindwa kusimamia sekta ile ya barabara na sekta ya mawasiliano.

Mhe. Spika, *page* ya 38, *paragraph* ya 37, kuna Mamlaka ya Viwanja vya ndege, kuna ununuzi wa *machines* nne za *X-ray*, tunajua kwamba kuna Kampuni ya *HISCO* ya Afrika Kusini ndiyo ambayo itafanya hiyo kazi na Mhe. Waziri, anasema kwamba hatua iliyobakia ni utiaji saini wa mkataba huo. Niwaambie mimi kama Mwakilishi nimeanza kupata mashaka kwamba yale yale ya zamani yanakuja, ninayo hapa nyaraka za hiyo Kampuni ambayo

wamekubaliana, wanaweza wakanambia nimezipata wapi, lakini mimi ni Mwakilishi, *invitation for quotations* imetolewa tarehe 3/04/2014, lakini *invoice* ya bei ilifika tarehe 02/03/2014, maana yake bei imekuja mwanzo kuliko barua ya *invitation*, ni wizi tu. Sheria ya fedha iko wazi, Kanuni Nam. 2 iko wazi kwamba hii ni barua ya *invitation* ya Mkurugenzi tarehe 03/04/2014, lakini *invoice* ya Kampuni kutoka Afrika Kusini imekuja siku moja nyuma kabla.

Mhe. Spika, kwa hivyo, mradi huu utakamilika baada muda fulani na *machines* nne tumeazimwa, watu wazima mnanidanganya. Kwa hivyo, kama serikali iko makini, hii ni dalili ya wizi na hasa maneno yangu kwa sheria ya fedha na Kanuni, mtu mzima anatudanganya mchana, Alhamis tena karibu na Ramadhani, ni aibu na ndiyo pia *Alhaj* ni hatari kubwa. Sheria ya fedha iko wazi kwamba hii ni dalili ya wizi. (*Makofi*)

Mhe. Spika, mwaka jana hawa jamaa uliwasaidia sana, mimi nikuombe sana kwa heshima zote tuachie tutoe funzo kwamba hii serikali kuwa hawa jamaa ni mtihani. Tumesema sana, lakini hawa jamaa hawasikii na mtu akenda na masikio ya chini hatari sana. Bibi yangu aliniambia; "usiombe ukawa na masikio ya chini, husikii chochote". Kwa hivyo, tuachie tusaidie Taifa ili wananchi wasiendelee kukopwa pesa nyingi za umma, halafu watu wakavuruga tu. Kwa mujibu wa sheria na mambo yote hii ni dalili ya wizi na mimi nasema kwamba Wawakilishi musihalalishe wizi ni hatari.

Mhe. Spika, mamlaka hiyo ya Uwanja wa ndege watu wamesema zamani kwamba ni mali ya mtu, mimi naamini kwamba ni mali ya mtu. Jina libadilishwe baada kuitwa Amani Karume, mwite Hija au Asha Bakari au Gavu au mwenyewe kule Uwanja wa ndege, lakini msitudanganye kwamba hii ni mali ya umma kumbe ni mali ya watu, natoa ushahidi wa *X-ray machine*, kuna mtu huyu alipata ajali akawa anakimbizwa India kwa ajili ya kufanya operesheni ya mifupa akalipia elfu 20 ya risiti kwamba anaomba alipie ili aruhusiwe kuingia na gari na akalipia elfu 20,000. Baada ya kuingia adabu aliyoipata, anamjua Mungu. Kwa hiyo, pale Uwanja wa ndege ni wa mtu ikiwa huyu aliyekatika miguu mlemavu anaharibiwa, je, mimi ambaye ni mzima na nimevaa tai leo, watapiga tu, siyo masihara, ikiwa huyu mgonjwa wa Mungu amepata adhabu, je, wewe mzima utapigwa tu.

Mhe. Spika, na mimi namuomba tupigeni sana, tupigeni sana. Siku moja namuomba Mhe. Naibu Waziri wa Habari, alikuja pale akabanwa haingii ndani anapokea wageni, nikawaambia mtieni adabu hivyo hivyo. Niliwaambia mimi na akatae mshughulikieni mpaka akome, kwa nini? Kwa sababu wameshinda kusimamia haki ya watu, mamlaka mshughulikieni kwa sababu Wawakilishi wameshindwa kusimamia haki za watu. Hata Waziri wa Fedha, akija mshughulikieni kwa sababu ni sehemu ya Baraza.

Mhe. Spika, mwisho kabisa niseme kwamba juzi nilihoji kibali walichopewa meli ya *SeaLink* ya kaka angu Bakhresa. Mhe. Waziri. akaandika maneno yako. lakini akawa hana maneno ya kuridhisha. Ninachomwambia Mhe. Waziri. ni kweli sisi ma-*engineer*. lakini na ushahidi wote unaonesha kwamba mmekiuka taratibu za sheria za *ZMA*. Nikawambia kwa nini mmetoa kibali cha kuongeza abiria 700 mpaka 1400 wakati sheria ya usajili wa meli iko wazi? Mtu anamashaka kaamini, kwa nini asiamini kama kuna rushwa. Kwa hiyo, Mhe. Waziri, wacha mzaha, tupate majibu ya kina ambayo yanaridhisha watu, kwa nini mmeongeza abiria kutoka 700 hadi 1400 wakati sheria ipo? Na kama Wawakilishi walikuwa hawana haki ya sheria ile kuipitisha, ni kwa nini ulikuja ukatuomba hapa?

Mhe. Spika, nina maelezo mengi, lakini naheshimu muda wako na yote haya yanaonesha ubadhirifu wa fedha za umma Uwanja wa ndege na mwisho namalizia kwa kusema kwamba sheria ya fedha inasema wazi kwamba manunuzi yoyote, nadhani shilingi milioni 10,000,000 ni kwa ajili ya tenda wametumia hawa jamaa milioni 120,000,000 kwa kununua matroli bili ya tenda, lakini kivipi? Wametoa kidogo kidogo mwaka ule ule ili baada ya hivi miaka 20 lengo ni kwamba wanakwepa utaratibu wa tenda. Serikali ipo…

Mhe. Spika: Bado dakika tano.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, ukimwambia waziri ama jamaa yule ni mkali kidogo, mkali! Pana mkali hapa, jamaa linauma *Inalilahi Wainailayhim rajiun*, maana yake kuna mtu mkali juu ya sheria, nikasema mama wee mtihani. Duh! Kwa niaba yangu na wananchi wa Jimbo la Kiwani na kila Mwakilishi aliye makini bajeti hii nakuimba sana mzee wangu, irudi wakajipange, hawa watu hawawezi kufanya kazi wakatudanganya, siungi mkono. (*Makofi)*

Mhe. Ashura Sharif Ali: Mhe. Spika, ahsante sana, awali ya yote nianze na kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu aliyetujaalia uhai, lakini pia, akatupa na uzima akatuwezesha kuwepo hapa kutekeleza majukumu yetu kwa

maslahi ya Taifa letu, lakini pia, nikushukuru na wewe kunipatia na mimi nafasi hii ya kuweza kutoa mchango wangu mdogo katika bajeti iliyo mezani wakati huu.

Mhe. Spika, niseme kwamba nimpongeze Mhe. Waziri, kwa uwasilishaji wake, lakini pia, niwapongeze watendaji kwa kuhudhuria kwa wingi sana huku juu.

Mhe. Spika, mimi nianze kusema kwamba Wizara hii ya Miundombinu na Mawasiliano ni wizara muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa lolote lile duniani. Nchi ambazo zimefikia maendeleo ya kweli zilifanya kazi kubwa sana katika kupitia Wizara hii ya Mawasiliano na Miundombinu. Ni wizara ambayo ukisema miundombinu, maana yake huwezi kufikia yale ambayo yanahitajika au yanaweza kuzalisha kwa ajili ya uchumi wa Taifa bila ya kuweka miundombinu inayokubalika katika Taifa husika.

Mhe. Spika, niseme kwamba uchumi wa Taifa hili unalega lega mno, ni kweli kwamba serikali yetu imekuwa tegemezi mno kiasi ambacho fedha zetu hazikidhi haja ya ile miradi ambayo tunahitaji tuweze kufikia malengo ya Taifa hili.

Mhe. Spika, niendelee kusema kwamba serikali umefika wakati sasa kama kweli tunahitaji kufikia huko tunakokusudia, ni vyema tukaangalia upya utaratibu wa kujiwekea katika sekta hii ya miundombinu na mawasiliano. Huu ni utangulizi wangu baada ya utangulizi huo, sasa nije katika mchango wangu.

Mhe. Spika, niseme kwamba sisi vyetu ni visiwa, visiwa vyetu tunahitaji kufanya shughuli zetu kwa njia ya kupitia baharini, ikiwa tunataka ikiwa hatutaki, lazima tufanye hilo na hili kwa maslahi hata ya uchumi wetu kupitia watalii wetu, tunahitaji lazima shughuli hizi ziwepo.

Mhe. Spika, kwa masikitiko makubwa sana, natanguliza hili Mamlaka ya Usafiri Baharini napata tabu sana, wizara hii kuweza kuruhusu meli yenye uwezo iliyotengenezwa kwa utaratibu wa kuchukua watu 700, ikakiuka sheria na kuchukua watu 1400 kichume na utaratibu wa sheria za nchi hii. Mimi najiuliza wizara hii mna utaratibu wenu, sheria mnapitisha wenyewe, kwa nini mnatuletea sisi hapa? Kwa hiyo, niwaombe baada ya haya mazungumzo ambayo Waheshimiwa Wawakilishi tunayasema hapa, basi mtangaze rasmi meli hiyo ichukue watu 700, ndiyo uwezo wake. Tumechoka vilio na misiba ambayo makovu na majeraha yake bado wanayo Wazanzibar.

Mhe. Spika, tunasema kwamba tukimalizia maneno haya, meli hii ichukue uwezo wake uliotengenezewa kwa utaratibu unaohusika watu 700, wengine hivi leo walikuwa vizuka ni wajane wameachwa na waume zao, tuna watoto mayatima, tuna watoto ambao wanahitaji kuhudumiwa wamepoteza wazee wao wote wawili, tuna vijana wetu wa shule kadhaa ambao wangelijenga Taifa hili, hawapo na sababu ni usafiri wa baharini. Leo imekuwaje meli iliyosajiliwa kisheria ichukue watu 700, unasema 1400, haikubali na wala haieleweki na nasema kwamba hili na mimi sitaunga mkono bajeti hii kwa sababu kwanza ya hili.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu nigusie hapo hapo utaratibu wa tiketi ni mbovu, jamani inakuwaje una Ofisi na utaratibu wa utoaji tiketi, halafu ziweko mikononi nje, kama tunataka tuuze mikononi hatuna haja ya O,fisi ndio maana yake. Utaratibu uliopo, kwa nini haufuatwi mbona tuna maradhi ya kutofuata sheria sisi jamani?

Mhe. Spika, baada ya hayo ,sasa nije kwenye Shirika la Bandari. Mimi ninachotaka kukisema ni kuuliza kwamba hivi Mhe. Waziri, hizi Bandari nyengine akiacha ile ya Malindi hazitaki, hazina haja, hazina umuhimu kwa Taifa hili? Nimkumbushe Mhe. Waziri, mimi ni mtu kutoka Mkoa wa Kaskazini Unguja ambapo kuna Bandari ya Mkokotoni ambayo ni maarufu na inafanya shughuli zake kila siku, inapakia abiria kuelekea Pemba - Tanga, inatoa abiria kutoka Tanga kuja pale usiku na mchana. Pia, kunafanyika shughuli mbali mbali za kibiashara, kunashushwa vitanda, magodoro, viti, meza na kadhalika,lakini mbona iko vile?

Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Waziri, serikali inasema na kupiga kelele vyanzo vya mapato, fedha ndogo, hawajajipanga kukusanya, ndio maana yake, mimi nasema hawajajipanga na hawajawa tayari, wamekusudia fedha hizi ziingie kwenye mifuko ya wachache watumie na ndio maana imetokea hiyo. Bandari ya Mkokotoni kuna mapato ambayo yanaweza kusaidia kuendesha maisha ya Taifa hili, lakini bado kunafanywa mchezo anayekusanya hajulikani, anayepokea haonekani, Bandari hiyo inakwenda kienyejienyeji tu. Nimuombe Mhe. Waziri, pamoja na kwamba anazungumza sana na Naibu wake, lakini nimuombe waiangalie upya, waziangatie hizi Bandari ndogo ndogo hususan ya Mkokotoni, upakizi wa abiria hapo haueleweki.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, tuwe watulivu tumsikilize Mhe. Ashura Sharif Ali, anaendelea kuchangia.

Mhe. Ashura Sharif Ali: Mhe. Spika, niseme kwamba hapo panapakiwa abiria vyombo vyenyewe havieleweki, hujui wanapakia kiasi gani, ukubwa gani, hicho chombo kina uwezo gani, ilimradi vinapakia wanakwenda na kurudi, basi Bandari ya kienyeji inakwenda hivyo, pengine na hayo madawa ya kulevya na vitu vyengine vinapitia humo. Nataka niseme na makusanyo hapo ndio yanapotea, lakini usalama wa abiria pia sioni kama unachungwa. Nimuombe sana Mhe. Waziri, alifanye hilo.

Mhe. Spika, jengine hili sitaki niulize labda niliguse tu, ujenzi wa Bandari ya Mpigaduri. Hii imekuwa hadithi ya alinacha na mimi naiacha vile vile kama ilivyo, ikiwezekana sawa, haikuwezekana, basi nasema kwamba labda niache hapo, lakini pia, kuna kitu kinazungumzwa hapa hatua za utekelezaji.

Mhe. Spika, wamesema kwamba wao katika utaratibu wao wa utekelezaji kwa mwaka uliopita katika mwaka 2013/2014, Shirika limelenga kuhudumia meli za kigeni 180, lakini ninaacha hizo za kigeni, mimi nakusudia hapa. Aidha, meli za ndani zilizohudumiwa ni 2913, najiuliza, sisi tuna meli za ndani idadi hii? Maana labda niseme kwamba waziri atakapokuja hapa anifahamishe meli za ndani, nimeona hapa katika ukurasa wa 44 kuna meli za ndani ambazo zimehudumiwa hapo zipatazo 2913. Ningependa nifahamishwe na nieleweshwe, meli za ndani ni zipi na meli tulizonazo hapa zile za serikali ni mbili *MV.* Ukombozi na Maendeleo na hivyo vyombo vyengine vya *private* zinafika meli 2913? Naomba nipatiwe majibu haya.

Mhe. Spika, pia, tunasema kwamba kuna utekelezaji wa miradi ya maendeleo, hivi jamani mimi niulize hii miradi ya maendeleo hasa ikitajwa huwa ipi? Kwa sababu hapa naona wamesema kwamba wana matengenezo ya sakafu ya eneo la kuhifadhia makontena Bandarini, hili nalo limekuwa mradi, mbona tunazungumza lugha za kiajabu ajabu mambo ambayo hayapo. Miradi ni ile ambayo inaanzishwa na kuoneshwa fedha zake na utaratibu, lakini mara nyingi nimeona hapa kuna hadithi za alinacha na kuna maneno ya ajabu, kwa sababu ukarabati nao huitwa mradi. Jamani, hapa tulipo ni pengine, wizara hii ni muhimu sana kabisa kwa maendeleo ya Taifa, hivi vitu vya ajabu ajabu ni vitu vya kubahatisha ambavyo havieleweki, mimi napata mashaka kuona kwamba matengenezo ya sakafu nayo pia yanasemwa huo ni mradi umetekelezwa na fedha zimetajwa hapa ni shilingi 164.01 milioni zimetumika jamani, tunadanganyana, tunaambiana ndivyo ilivyo, huu ni mtihani.

Mhe. Spika, tumepeana hadithi, mwisho kabisa kuna uchimbaji wa mchanga katika gati ya Malindi, mradi huu haujaanza kutokana na hali ya kifedha na kwa hivi sasa. Hata hivyo, shirika limekusudia kuutekeleza mradi huo mara tu hali itakaporuhusu. Hali kama haikuruhusu sisi tupitishe nini hapa ikiwa mnatupa hii taarifa, maana yake hauna fedha, sisi wajibu wetu ni kupitisha hizo fedha za miradi mliyoipanga ili mkatumie mkituhadithia sisi, tuwaambieje?

Mhe. Spika, nikiondoka hapo, sasa niende katika mradi wa barabara. Mimi niseme kwamba mara nyingi mtu hufanya tathmini kwanza na hatimaye akajenga, serikali mara nyingi inaingia katika miradi ya ujenzi mizuri tu, kwa ajili ya maendeleo ya Taifa na wananchi, lakini Mhe. Saleh Nassor Juma, asubuhi alizungumza kwamba, ni vyema tukafanya tathmini kwanza tukaona zile gharama tukawalipa wananchi ambao tunawaondoa katika maeneo husika kwa ajili ya majumba yao na mimea na hatimaye sasa ndio tukaanzisha ujenzi.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri, amesema kwamba barabara ya Koani na Jumbi hiyo anasema hajalipa fidia.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, sauti zinapaa, minong'ono imekuwa mikubwa kidogo. Kwa hiyo, inatuharibia mwelekeo na mwenendo wa shughuli zetu. Naomba tuwe watulivu tunaweza tukazungumza, lakini kwa kunong'ona. Mhe. Ashura Sharif endelea.

Mhe. Ashura Sharif Ali: Mhe. Spika, ahsante sana, umenisaidia. Niiambie wizara imeweka hapa huu miradi, lakini fidia za hawa watu wa Koani-Jumbi wengine wamelipwa na wengine hawakulipwa, nyumba zao wengine wamekaa hazikuvunjwa na mpaka hivi sasa zipo. Ni kweli kabisa lazima wakatae hili, maana kuna barabara nyingi zilizojengwa, mimi namshukuru Mwenyezi Mungu, niseme *Alhamdulillah Rabil-alamiin* Bumbwini-Mfenesini ni barabara iliyokamilika ambayo nilikuwa nina kilio cha muda mrefu na ni nzuri sasa, lakini fidia zao baadhi yao mpaka hivi leo hazijalipwa.

Mhe. Spika, sasa hili ni tatizo, kwa mwananchi wa kawaida unapomuondoa katika eneo lake husika asijue pakuelekea na wakalipwa nusu au kutolewa fidia kulingana na wanavyotaka tu, huyo mpe ngapi na huyo ngapi, jamani hatutofika, hizo ni haki za wanyonge na Mwenyezi Mungu hatotuacha kwa hili. Bado wizara wana haki za watu Mfenesini-Bumbwini hawajazilipa, lakini wajue kwamba Jumbi-Koani ni barabara muhimu nayo wamefikiria jambo zuri, lakini zile nyumba thamani waliyopewa na wenyewe wanyonge waliokusanya tofali moja moja wakajenga wakafikia hatua ile jamani hawajatendewa haki, lazima hili lifanywe.

Mhe. Spika, jengine niseme kwamba kuna mradi wa barabara zinazoingia mjini. Sasa niseme kwamba barabara ya kutokea Mkokotoni-Mahonda hadi kuja mjini, sasa hivi imekuwa tatizo, barabara hii ukipita Chaani, Gamba, Kinyasini, kwa kweli sasa hivi hali ni ngumu sana huko, wanaoelekea Nungwi, Matemwe ambako sisi tunakusanya kodi kwa ajili ya wageni wetu, watalii wanaokwenda huko na wakipita maeneo hayo hali ni ngumu sana. Serikali umefika wakati wa kuiona ile barabara na kuianzishia mradi.

Mhe. Spika, mimi nilidhani kwa sababu nimewahi kuiona kwenye bajeti iliyopita, nilijua nitaiona hapa, nimeiona nimeisoma, lakini naambiwa haijapatiwa fedha, bado wanataka watoke nje wakaombe wafadhili. Niiombe sana serikali iiangalie barabara ile ina umuhimu mkubwa na ni barabara ambayo ni kubwa kutoka mjini kuelekea huko Kaskazini, barabara ile ni muhimu sana kabisa wananchi wanapata tabu.

Mhe. Spika, pia, kuna barabara ambayo inatoka Mkwajuni-Kijini, barabara hii tokea enzi ya Nabii Nuhu na Nzi Kibwebwe haijajengwa, huko wanakaa wananchi wengi, watu wanaishi, lakini masikini wanawake wajawazito wakati wa kujifungua wanafika kujifungulia njiani kwa sababu gari haiendi, ama atazaa kwenye gari, ama anaweza kupoteza mtoto wake na yeye mwenyewe. Niiombe saa serikali, nimeona imeingizwa hapa, basi isiwe kubabaishana iwe kweli na kweli waweze kutekeleza ujenzi wa barabara hiyo.

Mhe. Spika, vile vile, kuna barabara ya Muanda ambayo huko kunatolewa mazao mengi sana, ndio nikasema kwamba miundombinu ndio inayoleta uchumi wa Taifa. Sasa barabara hii ni vyema ikafikiriwa nayo, wanazalisha viazi vitamu vingi mno tunavyokula, kuna mikarafuu inazaa karafuu nyingi zinaletwa na ndio uchumi wetu mkubwa, tunapiga kelele sasa hivi karafuu, karafuu zinatokea kule. Kwa hivyo, barabara hii ya Muanda kuja Donge ikaunganisha kuja Mjini ni muhimu sana. Naiomba serikali iiangalie kwa jicho la huruma kabisa ili iweze kujengwa barabara hii.

Mhe. Spika, barabara hii ya Mkokotoni kuna madaraja tena ni ya hatari, kama wanaona masihara kwa vile hawatembei twendeni mkaone hiyo hali ilioko huko ya hayo madaraja, hali ni ngumu madaraja zaidi ya manne, lakini ukipita unafumba macho. Magari yanayopita ni mengi mno kwenda Mkoa wa Kaskazini. Hivyo, pia, niwaombe Waheshimiwa, serikali ichukue juhudi za makusudi hali si nzuri.*(Makofi)*

Mhe. Spika, nikiendelea kidogo niseme niiombe serikali, mimi nasimama kuiomba serikali tu, serikali kwa miaka 50 sasa ya Mapinduzi yetu matukufu tumefanya sherehe za aina yake, lakini umefika wakati wa kuangalia Kiwanja cha ndege cha Pemba, kutokujenga Kiwanja cha ndege Pemba na kuboresha huku kwa kweli kunakuwa hakuleti sura nzuri ile inayosifiwa ya Kimapinduzi na kuleta usawa kwa Wazanzibari wote. Niiombe sana serikali umefika wakati wa kuona sasa tuboreshe Uwanja wa ndege wa Pemba, hadithi za alinacha hebu ziondoke, sasa tufanye kweli, kwenye bajeti watu wanasema, lakini mimi nimeona kwa nafsi yangu nikifika pale huwa napata masononeko makubwa, kulikoni ndege zile zisitue ikifika saa 12 unaambiwa itakuwa ndege hairuki, ndege haitui haipendezi, inaweza kutokea *emergency* Mhe. Rais wetu yuko kule na hakuna aina yoyote ya uwezo huo, tutafanyeje? Ndio swali tunaweza kufanya nini? Imetokea *emergency* ndege haiwezi kuruka na Mhe. Rais yuko kule na watendaji wake.

Mhe. Spika, wananchi ambao wana haki pia, kisiwa kile kina nafasi ya uchumi wa aina yake, watalii wengi kabisa hupita pale *Airport* nao, wanaokataa kupita Bandarini wanapita *Airport*, ule ndio utamaduni wa kusema wanataka kuja Unguja, imetokea haja wanataka kwenda watalii wanakosa safari zao, hatuwezi kufikia malengo. Naiomba serikali kwamba iangalie upya, ijipange, ifikirie na iwazie popote iwe iwavyo, lakini ioneshe dalili na moyo wa huruma na upendo kwa Wazanzibari kuwaunganisha kuona kwamba huduma zao zinapatikana kwa usawa, ili kuondoa manung'uniko, basi *Airport* ya Pemba ni lazima sasa yaonekane mabadiliko ya kweli kupitia serikali yetu.

Mhe. Spika, baada ya kuyasema hayo, niseme kwamba mimi sitaweza kabisa kuunga mkono hotuba hii kwa kuwa kuna mambo naiomba serikali ifanye, lakini pia, kuna mengi niliyaomba kwa miaka mingi, sitaunga mkono mpaka

nipewe majibu ya kuniridhisha, nikipewa majibu ambayo yameniridhisha na kunijenga matumaini kwa maswali yangu, basi nitaunga mkono, lakini kwa sasa hivi siungi mkono nakushukuru.

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Mhe. Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema aliyetujaalia leo kufika hapa tukiwa wazima wa afya na kuweza kutekeleza majukumu yetu. Pia, nikushukuru na wewe kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mhe. Spika, na mimi nimpongeze Mhe. Waziri, pamoja na Naibu wake na watendaji wote wa wizara hii kwa kuweza kutekeleza majukumu ambayo wamepewa katika kipindi cha mwaka 2013/2014.

Mhe. Spika, mimi sitokuwa na mengi ya kusema na mengi kati ya hayo ambayo mengine nilikuwa nimejipangia kusema tayari wameshazungumzwa. Suala la kwanza kabisa ambalo huwa mara nyingi sana nalizungumza katika Baraza hili na ambalo bahati mbaya sana ninakuwa sisikilizwi, lakini nitaendelea kulizungumza hadi mwisho wa kipindi changu cha kukaa ndani ya Baraza hili. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mimi nasimama hapa kwa niaba ya wanawake, wanawake ndio walionichagua kunileta hapa na lazima niwalipe fadhila zao. Kwa hiyo, nikisimama hapa nataka niwatetea zaidi wanawake kwa sababu kila mmoja anatetea cha kwake, mwenye jimbo lake na mimi nasimama hapa kwa niaba ya wanawake ambao wamenichagua.

Mhe. Spika, vitabu vyako vyote vinavyokuja humu nilishaomba katika kipindi cha nyuma kwamba viwe na taarifa inayoelezea kama ni wafanyakazi, basi wangapi wa kike na wangapi wanaume wanaopelekwa kwenda kusoma. Katika ukurasa wa 21 unaoelezea Idara ya Utumishi na Uendeshaji kuna kifungu kinaelezea suala zima la watu ambao wamepelekwa kwenye mafunzo, lakini kwa bahati mbaya sana hatujaambiwa wangapi wanawake waliopelekwa na wangapi wanaume.Vile vile, katika ukurasa wa 22 umeelezea suala zima la watu kupandishwa vyeo katika wizara hii, ambao wamefanya kazi kwa kipindi kirefu, lakini pia, wana utaalamu. Pia, haikuchanganua kwamba ni wangapi wanawake ambao wameweza kufanikiwa kupandishwa vyeo katika wizara hii.

Mhe. Spika, huu sio utawala bora, nasema hivyo kwa sababu tunajua kwamba kuna mambo mengine yanafundikwa chini ya zulia. Sisi tunataka haki zetu, kuna wanawake wanafanya kazi katika mawizara mbali mbali, lakini kwa sababu ya jinsia zao hawapewi kipaumbele katika masuala mbali mbali. Mhe. Waziri, akija hapa anipe idadi ya wafanyakazi wake aliyonao wanawake kama anao, lakini anipe na idadi ya wafanyakazi hao ambao wamepelekwa mafunzoni pamoja na wale waliopata kupandishwa vyeo.

Mhe. Spika, nikiendelea niende katika ukurasa wa 24. Nimpongeze sana Mhe. Waziri, kwa kuweza kufanya ukarabati na ujenzi katika barabara mbali mbali za Unguja na Pemba. Tunafahamu kwamba kazi ni nzito, kazi hizi ni nyingi, lakini vile vile, uwezo wa serikali yetu ni mdogo bado. Kwa hiyo, ujenzi wa miundombinu unategemea sana na uwezo wa uchumi wa nchi ile, lakini bado tuna pungufu ndogo ndogo ambazo zinasababisha kila siku badala ya kwenda mbele tunarudi nyuma.

Mhe. Spika, mimi nataka kuizungumza barabara ya Kisiwandui mpaka kufikia *Wireless.* Mwaka juzi nimeizungumzia barabara hiyo, mwaka jana nimeizungumzia barabara hiyo na leo nasimama tena kuizungumzia barabara hiyo. Leo nasimama zaidi kwa uchungu mkubwa sana kuhusiana na barabara ile. Barabara ile niliahidiwa kwa bahati mbaya sana siku ambayo niliuliza swali hili mwaka jana, siku ile mimi sikupata nafasi kwa sababu ulinituma. Kwa hiyo, nikaondoka nikawa sipo Barazani, lakini nimetizama kwenye *Hansard* sikuona kwamba nilijibiwa, lakini leo nayataka majibu na namwambia Mhe.Waziri, kwamba hapa leo hakitoeleweka, shilingi naitoa.

Mhe. Spika, ile barabara tukumbuke kwamba ni barabara ambayo imo ndani ya Mji wetu wa Zanzibar, mjini kabisa, barabara ile imekuwa ikitumika na gari, lakini ipo karibu na majumba mengi ambayo wananchi Wazanzibari, lakini mimi nilipoomba na nimekuwa nikimwambia sana Mhe. Waziri, barabara ya Kisiwandui/*Wireless,* Mhe. Waziri, akawa ananiambia itafanyiwa kazi. Nikaja nikamuuliza kwa bahati nzuri sana tulipokuwa Dodoma kwenye Bunge la Katiba Mhe. Waziri, alikuwa anakaa nyuma yangu. Kwa hiyo, kila nikigeuka ninamwambia Mhe. Waziri, barabara yangu, ananiambia Mheshimiwa itafanyiwa kazi.

Mhe. Spika, kabla ya kuondoka barabara ile iliparwa watu wakapata tamaa, nimefika pale nyumbani tukafurahi sana pamoja na watu wa pale. Ni mwezi wa nne na jambo baya sana ambalo limejitokeza pale ni kwamba barabara ile

imechimbwa mpaka ikapasuliwa paipu za maji. Leo ukipita pale mbele ya Ofisi ya Walemavu kuna shimo kubwa ambalo linatoka maji, panafuka maji ambayo watu wanayalilia na wanayataka, lakini yanamwagika ovyo.

Mhe. Spika, ile barabara imeharibika vibaya sana. Mimi nimemwambia Mhe. Waziri, hivi sasa naona aibu nikipita pale wananchi wananitegemea, nikipita pale najificha naingia mvunguni kwenye gari yangu, lakini haiwezekani nisiende mimi kule kwetu. Sasa nimemuuliza Mhe. Waziri, akaniambia mkandarasi ambaye amepewa kazi ile kufanya, alikuja akagundua kwamba ile fedha ambayo aliisema ataitumia ni kidogo, kwa maana hiyo kwamba wizara imempa mtu kufanya ile kazi wakati tathmini ya ile barabara wao wenyewe hawaijui.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri, anajua vizuri sana tumezungumza, haiwezekani kwamba leo apewe mkandarasi ambaye kwa sababu tu amesema mimi nitaitengeneza kwa milioni kadhaa ambazo ni kidogo kuliko wengine akapewa na baada ya hapo akagundua kuwa hawezi kufanya kwa fedha zile alizozisema. Hapo pana rushwa, rushwa inanuka hapo, haiwezekani. Nataka maelezo Mhe. Waziri.

Mhe. Spika, nilimuomba Mhe. Waziri, nikamwambia angalau basi tustiri pale maji yasitoke patiwe kifusi. Siku mbili sijenda, lakini sijui nini kimefanyika, lakini leo nasema nataka nijue barabara ile Mhe. Waziri, uniambie lini itatengenezwa. Nakumbuka vizuri sana ile ilikuwa ahadi ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Alikuja pale watu wakamlalamikia na akasema kwamba barabara ile itajengwa, lakini mpaka hii leo umepita mwaka mmoja na nusu hakuna kilichofanyika. Kilichofanyika ni kwamba kumekwenda uharibifu zaidi. Wamekwenda pale wamechimba na wamepasua paipu, sasa maji yanamwagika ovyo. Hilo halikubaliki na nasema kwamba leo Mhe. Waziri, anijibu aniambie kwamba lini barabara ile itatengenea. Sio lini kwa maneno, tumeshachoka na maneno, lakini tunataka barabara ile itengenezwe, kwa sababu nina wasiwasi mkubwa kwamba fedha tayari zilikuwa zimeshatengwa. Haiwezekani barabara ianze, halafu ghafla ikatike, lazima kuna fedha kazipeleka wapi? Mhe. Waziri, utaniambia fedha za barabara ile umezipeleka wapi? Kama unazo kwa nini haitengenezwi?

Mhe. Spika, nitakwenda katika ukurasa wa 32, Idara ya Mawasiliano. Sote tunajua kwamba teknolojia ya mawasiliano ni muhimu katika kukuza uchumi wetu wa nchi hasa katika masuala mazima ya biashara, sekta za elimu, sekta za afya na kila kitu. Wewe mwenyewe ulikuwa shahidi juzi tulipopata semina kutoka kwa Huawei, tuliona duniani wenzetu wanafanya mambo ya ajabu kwa kutumia teknolojia ya mawasiliano. Gharama nyingi ambazo zile Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, wanalalamika hasa katika zile gharama tunazosema kwamba kunakuwa na mikutano, kunakuwa na viburudishaji na kunakuwa na *sitting allowance*. Zile zinaweza kuondoka ikiwa tutapata teknolojia ya mawasiliano.

Mhe. Spika, sasa mimi nashukuru sana na naipongeza serikali kwa sababu kwa kweli wameweza kuanza kujenga mkonga wa Taifa ambao utakuwa unapeleka taarifa mbali mbali katika mawizara, lakini mimi najua wizara hii ndie mdau mkubwa wa *ZANTEL* na kuna mambo ambayo yananisikitisha sana, bado hatujaweza kukaa tukafikiria kuwaondoshea uzito au ugumu wa kiuchumi wananchi.

Mhe. Spika, kuna suala zima la kuweza kuzitumia simu. Mawasiliano ya simu sio kuzungumza watu kuwasiliana kuwa huyu kampigia huyu tu, haitoshi. Wenzetu tunawaona sasa hivi Tanzania Bara bili za umeme, bili za maji, bili za kila kitu zinalipwa kwenye simu, tunawapunguzia wananchi ugumu wa maisha. Mwananchi atoke huku anakokaa Matemwe aje mjini gharama yake ni shilingi elfu sita, lakini leo akiwa na uwezo kwa kushirikiana na *ZANTEL* na naamini mimi *ZANTEL* wanaweza. Kwa sababu *TIGO* wanafanya hivyo, kwa nini *ZANTEL* hawachukui jukumu hili wakatupunguzia ugumu na uzito wa maisha kwa wananchi wetu. Hilo linawezekana.

Mhe. Spika, lakini kama *ZANTEL* Kampuni ambayo inategemewa na inatumika sana hapa Zanzibar. Kwa bahati nzuri kusoma sio tu kwenda skuli, lakini kusoma unasoma, unaonana na watu wengine ukenda sehemu nyengine, ndio maana Wajumbe wako wanakwambia wanataka sana kusafiri wakaone dunia nyengine, wala Wajumbe wako hawakimbilii kutaka kusafiri kwenda nje, hapa hapa Afrika kuna nchi ambazo zina maendeleo kuliko sisi.

Mhe. Spika, sisi tulipata nafasi kwenda Nairobi mwaka huu, tulipokwenda kule nilitia *sim card cheap* ile ya Kenya, mpaka leo napata taarifa mbali mbali kuhusiana na mambo ya chakula bora, hali ya hewa na mengineyo. Hayo yanafanywa na mashirika yao ya simu. Lini sisi tutafika huko. *ZANTEL* wanafanya, lakini wanachokifanya mengi ni matangazo ya biashara. Hatujafikia teknolojia kubwa ile ambayo waliyonayo wenzetu, lakini hata hii ndogo tuliyonayo tuitumie vizuri ili tuwapunguzie ugumu wa maisha wananchi wetu.

Mhe. Spika, nalizungumza hilo sana kwa sababu uwezekano wa hilo kufanyika upo. Mwananchi haiwezekani leo anataka kulipa umeme atoke huko hata kama anatoka analipa mia tano, mia tano *is something* kwa maskini, kwa nini leo wananchi hawawezi kulipa kwa kupitia *ZANTEL?* Suala la kununua kadi lingekuwa halipo, ingekuwa tunatumia mitandao hii ya simu. Kungekuwa hakuna haja watu kukaa barabarani, lakini tumekuwa wagumu kutumia teknolojia, badala yake teknolojia inatumiwa katika mambo ambayo hata hayana faida na wala hayaleti maendeleo.

Mhe. Spika, la mwisho kabisa, mimi nataka kulizungumzia ni suala zima la usalama barabarani. Hili ni jukumu la wizara hii. Kuna barabara nyengine mpya bado zinajengwa, lakini zimekuwa hazijengwi zile sehemu za kuweka gari, ikiwa gari imeharibika au ikiwa gari tuseme daladala inataka kusimama hamna, lakini kikubwa madereva wetu hawa wanaoendesha madaladala utafikiri wanapewa *training* ya kuharibu huo usalama wa barabarani. Wanaendesha gari ovyo, utamkuta mtu amesimama katikati ya barabara kazuia magari mengine huko yeye anapakia abiria.

Mhe. Spika, ningeiomba sana wizara hii na hasa Idara ya Leseni kwanza kuhakikisha kwamba hawa wanaowapa leseni kweli wana akili timamu. Nina wasiwasi sana kwamba wengine hawana akili timamu namna wanavyoendesha magari na wakasababisha ajali katika barabara zetu.

Mhe. Spika, jengine ni kuhusu kusafirisha makontena yanayotoka Bandarini na kwenda katika maeneo ambayo yanahusika. Kwa nini yanasafirishwa mchana kweupe barabara zenyewe mbovu, nyembamba, halafu unaliona gari na kontena linapita. Hivi kwa nini hatufanyi mpango wa kusema kwamba kuna muda maalum wa kusafirisha hivi vitu japo usiku? Lakini ni hatari kwa maisha ya wanadamu, ni hatari ya maisha ya wananchi wa Zanzibar. Mimi naiomba sana wizara ilishughulikie hili ilisimamie inawezekana. Asiyetaka kusafirisha wakati huo akafungulie kontena lake kule kule Bandarini uwezekano huo upo. Nakuomba sana Waziri, ni hatari kwa sababu tumeshaona makontena yameanguka njiani.

Kwa hiyo, tunalisemea hili, sijalisemea mimi peke yangu na kuna Waheshimiwa wengine wamelisemea ni hatari. Tunaomba makontena yasisafirishwe wakati wa mchana ambapo muda huo kuna magari chungu nzima, kuna watoto wanaotoka skuli wanatembea, kuna binadamu watu wazima wanatembea. Kwa kweli ni hatari na tunataka kunusuru maisha ya wananchi wetu.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo, siungi mkono hotuba mpaka nitakapopata majibu. Nakushukuru sana.

Mhe. Spika: Mheshimiwa, tunakushukuru. Muda naona haumtoshelezi Mhe. Omar Ali Shehe, kuendelea kuchangia.

Waheshimiwa Wajumbe, kuna taarifa moja ya kazi na matangazo mawili. Taarifa ya kazi ni kwamba shughuli hii kwa mujibu wa ratiba ya shughuli zetu ilikuwa imalizike leo jioni, lakini wachangiaji tunao wengi mno. Kuna wachangiaji ambao bado hawajachangia na wameomba jumla 23. Ni dhahiri hatuwezi kuwamaliza,lakini badala ya kufanya majumuisho leo jioni, jioni tutaitumia kwa ajili ya kuendelea kuchukua michango. Hata hivyo, hatutaweza kuwamaliza. Nilikuwa natoa shukrani nyingi sana kwa wale ambao walikuwa wanajaribu kusema kwamba mengine yameshazungumzwa. Kwa hiyo, inasaidia katika kuokoa muda. Jioni tutaendelea na michango, lakini nitawaomba kwamba tuokoe muda ili tupate wachangiaji wengi zaidi na wale ambao kwa bahati mbaya hawatapata, waweze kutoa michango yao kwa maandishi. Hilo ni suala la taarifa ya kazi.

Waheshimiwa Wajumbe, kuna matangazo mawili. Moja ni tangazo la Tume ya Uchaguzi. Waheshimiwa Wajumbe, nimepokea katika Ofisi yangu taarifa kutoka kwa Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar ambayo inatuarifu kuwa Tume hiyo imepanga kuweka wazi daftari la kudumu la wapiga kura, ili wananchi wapate fursa ya kufanya ukaguzi na masahihisho ya taarifa zao pamoja na kuweka pingamizi kama zipo kwa watu wasiostahiki kuwemo katika madaftari ya maeneo ya uchaguzi pale itakapohitajika.

Waheshimiwa Wajumbe, shughuli hiyo ya kuweka daftari la kudumu la wapiga kura kuwa wazi itakuwa kwa muda wa siku saba kuanzia tarehe 21 Juni hadi tarehe 26 Juni mwaka huu katika vituo vyote vilivyotumika katika zoezi la kuandikisha wapiga kura wapya na uendelezaji wa daftari la kudumu la wapiga kura kwa Unguja na Pemba. Vituo hivyo ndivyo ambavyo vitatumika kuweka madaftari hayo wazi ili wananchi wapate nafasi ya kwenda kufanya ukaguzi na kuweza kufanya masahihisho na kwa wale ambao itakuwa hata majina yao hayamo, basi pia wataweza kusema. Zoezi hilo litafanyika kwa wananchi kujaza fomu maalum za malalamiko endapo katika ukaguzi wa

madaftari hayo, watagundua kukosekana kwa majina yao, kukosewa kwa taarifa zao ndani ya madaftari au kuwemo watu wasiostahiki kuwemo katika madaftari ya wapiga kura.

Waheshimiwa Wajumbe, taarifa hii inaletwa kwetu ili tuweze kufahamu juu ya kuwepo kwa zoezi hilo, lakini pia, tuweze kusaidia kufikisha taarifa kwa wananchi tunaowaongoza ili zoezi hilo la ukaguzi wa daftari la kudumu la wapiga kura liweze kuendeshwa na liendeshwe kwa ufanisi mkubwa.

Waheshimiwa Wajumbe, nashukuru kuwapa taarifa hiyo, nirudie tu tarehe 21 Juni hadi tarehe 26 Juni ndio zoezi hilo litaanza katika vituo vyote vile ambavyo vilikuwa vinatumika katika uandikishaji wa wapiga kura wetu.

Waheshimiwa Wajumbe, tangazo la pili, tunaalikwa Tamasha la Filamu la Kimataifa Zanzibar, yaani *ZIFF* ambalo Wajumbe wote mnaalikwa na tamasha hilo litaanza kwa Uzinduzi wa Onesho la Mechi ya Ufunguzi wa Kombe la Dunia ambalo litafanyika kuanzia leo saa 3:00 usiku Ngome Kongwe, lakini ufunguzi rasmi wa Tamasha hilo utafanyika siku ya Jumamosi tarehe 14 mwezi huu saa 2:00 usiku pahala hapo hapo Ngome Kongwe. Waheshimiwa Wajumbe wote mnakaribishwa. Tangazo letu hili limeletwa na mwenzetu Mhe. Mahmoud Thabit Kombo.

Waheshimiwa Wajumbe, baada ya taarifa hiyo ya kazi na matangazo hayo mawili, sasa tusitishe shughuli zetu mpaka saa 11:00 jioni.

(Saa 7:00 mchana Baraza liliakhirishwa mpaka saa 11:00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Baraza lilirudia)

Mhe. Spika: Waheshimiwa, majadiliano yanaendelea na kama lilivyoweka ombi langu mapema kipindi cha asubuhi, ni kwamba kila tukitumia muda mfupi kidogo ilimuradi Mhe. Mjumbe awe amechangi vizuri itasaidia kupata nafasi kwa Wajumbe wengi zaidi, kuchangia katika hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano.

Waheshimiwa Wajumbe, majadiliano yanaendelea. Nafasi ya kwanza jioni hii itakuwa ni ya Mhe. Omar Ali Shekhe na atafuata Mhe. Suleiman Hemed Khamis wakati Mhe. Ali Salum Haji anajitayarisha.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwa ni mchangiaji wa kwanza kwa jioni hii. Baada ya kukushukuru, nimpongeze Mhe. Waziri, kutokana na uwasilishaji wa bajeti yake ambayo kaiwasilisha katika lugha ambayo inafahamika vizuri.

Mhe. Spika, tunapozungumza bajeti ya Wizara ya Miunombinu na Mawasiliano, tunazungumza katika muktadha wa kuangalia hali ya uchumi wetu kwa sababu miundombinu ina umuhimu mkubwa katika maendeleo na kukuza uchumi wa nchi yoyote ile. Nchi zote duniani zilizoendelea na zile zinazoelekea kuendelea wamewekeza kwa kiasi kikubwa katika ujenzi wa miundombinu, kama vile Bandari, viwanda vya ndege pamoja na barabara.

Mhe. Spika, sasa ukweli ni kwamba uchumi wetu Zanzibar unaendelea kudorora kwa sababu hasa kutokana na changamoto inayoikabili Wizara hii ya Miundombinu na Mawasiliano. Kwa tathmini yangu, mimi nasema kwamba wizara haiendi vizuri kwa sababu tatu kubwa; Sababu ya kwanza ni sababu ya serikali kuu na hata wakati ninachangia bajeti kuu ya serikali, nilisema kama kuna maneno ya kuyazungumza, basi tunapaswa kuzungumza katika bajeti kuu ya serikali, kwa sababu kadiri serikali itakavyokuwa na uwezo wa kukusanya, ndivyo kadiri serikali itakapokuwa na uwezo wa kutoa fedha za kutosha katika sekta husika na hapo ndipo unapoweza kujenga hoja kwamba ikiwa wizara haikupewa fedha, unataraji kitu gani kitokee.

Mhe. Spika, jambo la pili, ni tatizo la serikali kuu vile vile katika suala zima la kutokuweza kuitekeleza ile sera yake ya *Public Private Partrnership (PPP)*. Ni ukweli kwamba nchi zote duniani zilizoendelea na zinazoelekea kuendelea katika suala zima la miundombinu, serikali haijipigi kifua *by hundred percent.* Nchi zote duniani takriban katika sekta hii ya miundombinu sasa hivi, sekta inayoongoza huwa si serikali bali ni *private* hizi *Companies,* ndizo zinazojikita katika ujenzi wa miundombinu na vitu vyengine.

Mhe. Spika, leo kwa upande wa Zanzibar, serikali inataka kuchukua kila kitu. Hili haliwezekani, serikali haina uwezo huo. Ni kupitia mpango huu pekee, ndipo unapoweza kwa kweli kuimarisha miundombinu hasa ya barabara,

viwanda vya ndege pamoja na sekta nyengine. Kwa hivyo, hili bado sipeleki shutuma wala tuhuma kwa wizara, bali ni tatizo la serikali kuu, kwamba bado hakujawa na umuhimu wa kuipa nguvu sekta binafsi, ama kuifungulia milango binafsi katika kuekeza kwenye maeneo hayo, lakini jambo la tatu ambalo kwa mtizamo wangu ndio linalochangia ni tatizo, sasa mimi niseme labda ni mambo ya uzembe na kutokuwa na vipaumbele katika wizara husika, kwa sababu hata pale unapokuwa na kitu kidogo, basi inapaswa kile kidogo unachopewa kukitumia kwa umakini au kile kidogo unachopewa kukitumia katika kuangalia vipaumbele ufanye nini.

Mhe. Spika, hivyo, katika maeneo haya matatu, nadhani ndio yanayopelekea tukawa tuna tatizo kubwa katika Wizara hii ya Miundombinu na Mawasiliano na ndio sababu ya Wajumbe kwa kweli kuweza kuwa ni wakali mno katika uchangiaji wa bajeti.

Mhe. Spika, bajeti ya mwaka 2014/2015, mimi sitaki niingie ndani wala sitaki niichambue chochote, kwa sababu yake ni ile ile tu, bei ya pilipili hoho kwamba hamna kitu. Nimejaribu kufanya utafiti baina ya bajeti ya mwaka jana ya 2013/2014 na bajeti hii ya 2014/2015, nimefanya utafiti mdogo tu. Kuanzia ukurasa wa kwanza mpaka nikafika katikati. Kama ukifanya tathmini utaona kilichotokea hapa, kuna kitu kinachoitwa "*copying and paste"*. Walichukua bajeti ya mwaka jana, wakafuta maneno yale yale ya kumi na mbili, kumi na tatu, wakatia kumi na nne na kumi na tano.

Mhe. Spika, hata mpangilio huu wa bajeti takriban mtiririko huu ndio ule ule uliomo kwenye bajeti ya mwaka jana, hakuna kilichobadilika. Ukianza kusoma hapa utaona ni vile vile kila kitu ni kile kile. Kwa hivyo, tatizo pengine kama wanavyosema wenzangu inawezekana ikawa ni rangi tu ya kitabu kwamba mwaka jana kimekuwa ni cheusi, mwaka huu kimekuwa na *cream*, sijui rangi gani. (*Makofi*)

Mhe. Spika, hivyo, kwa ufupi ninataka niseme kwamba sitaki nijikite yaliomo ndani zaidi katika kufanya uchambuzi kwa sababu hakuna. Mimi ni mwaka huu wa nane katika Baraza hili na hadithi zilizomo humu ni tangu zile za mwaka 2005, tulipoanza kuingia katika Baraza hili, ni zile zile. Barabara ya Ole/Kengeja, sijui barabara ilichotoka, pengine ni ile barabara ya nyumba mbili, hadithi yake ndio imekwisha humu haionekani tena. Hilo limekamilika.

Mhe. Spika, hivyo, kwa kweli mimi sitaki nijikite sana katika kufanya uchambuzi kwa sababu hamna kipya sana ambacho kitakuwa ni tofauti na bajeti ya mwaka jana na katika ku-s*ave* muda wako, lakini kwanza ninataka nianze na suala la *ZMA*.

Mhe. Spika, Mamlaka hii ya Usajili wa Meli, nilisema hapa katika bajeti kuu kwamba kuna nchi zinategemea uchumi wake katika suala hili la usajili wa meli. Nikitaja mfano katika Kisiwa cha Malta kwamba uchumi wao unatokana na suala zima la usajili wa meli basi. Mwaka jana Baraza lako baada ya kazi kubwa liliagiza, likamuigiza Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwamba tunahitaji kujua yaliyotokea *ZMA* Dubai, ili Mkaguzi akafanye ukaguzi. Taarifa tulizonazo ni kwamba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kafanya kazi yake. Matarajio yetu ilikuwa ripoti ile iletwe. Jana niliwasiliana na Mhe. Waziri, anayehusika na wizara hiyo ya Mdhibti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, jibu lake akaniambia kwamba serikali haikuona haja ya kuleta ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali katika Baraza. (*Makofi*)

Mhe. Spika, ninataka niseme maneno yangu hapa, serikali yetu tunaisifu sana, lakini inawezekana serikali yetu inataka sasa kukiuka masharti na misingi ya utawala bora. Tunahitaji ripoti ya *ZMA* iletwe hapa Barazani. Serikali haiwezi ikafanya vitu hivi vya kiajabu ajabu. Mabunge yote duniani ama Afisi zote za Wadhibiti na Wakaguzi Wakuu zinafanya kazi ya ukaguzi, ama iwe ni ukaguzi wa kawaida au ni ukaguzi kaguzi hizi maalum (*Special auditing).*

Mhe. Spika, ripoti zote za *Special auditing* zinaletwa katika Mabunge. Kwa hivyo, hakuna sababu yoyote, kilichotokea pale ni serikali kama kuna tatizo lolote ni serikali, ndio iliyofanya vile. Ni wajibu wetu sasa kama chombo cha wananchi kuweza kujua kwa niaba ya wananchi, kuweza kujua tatizo lililotokea ni lipi. Haiwezekani serikali hiyo hiyo ikafanya kosa na serikali hiyo hiyo ikajihukumu, haiwezekani. (*Makofi*)

Mhe. Spika, tuna imani kubwa na serikali na tunaomba tena kwa mara ya pili, kwamba tunaomba ripoti ya ukaguzi maalum iliyofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali iletwe katika Baraza ili Wawakilishi wa wananchi wajionee na wananchi baadae wajue nini kilichotokea, vyenginevyo tofauti na hilo hatuwezi tukakubali na kwa kweli itakuwa ni serikali kuzidi kukiuka misingi hii ya utawala bora ambayo tumeitangaza kwamba serikali

itafuata misingi ya utawala wa bora.Kwa hivyo, naomba tena kwamba ripoti ile ya *ZMA*, pamoja na ripoti nyengine ziletwe katika Baraza ili Wawakilishi waendelee kuziona.

Mhe. Spika, jengine ni suala la usalama katika Viwanja vya ndega, pamoja na Bandari. Katika hili kwa kweli tunashukuru kwamba kuna mitambo hii ya *CCTV* imewekwa. Ni matarajio yetu inafuatwa, lakini tatizo ambalo limejitokeza hasa katika kiwanja chetu cha ndege, kuna kesi ya mpiga kura wangu katika Jimbo la Chake Chake ilitokea karibuni. Alisafiri pale na baada ya kusafiri alidondosha bahasha yenye dola elfu tatu na mia tano, bahasha ile iliekewa mguu. Kijana anayeitwa Karim alipofuatia ilionekana na majibu aliyopewa ilionekana kwenye *CCTV*, kweli kijana kapita pale na nini, lakini alipokaa *CCTV* kwa maelezo aliyopewa kwamba haikuonekana. Hii inaleta shutuma kwamba wafanyakazi wa *Airport* bahasha hii waliichukua.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri, jambo hili uliripotiwa na leo tunataka tulifuatilie kwa sababu kwa tokeo kama hili, kwa kweli linaichafulia heshima yetu. *Airport* ni pahala ambapo panatakiwa pawe na usalama na watu waliopo pale wanatakiwa wawe ni waaminifu. *Airport* hawapiti tu watu wa Unguja na Pemba, *Airport* hupita wageni mbali mbali. Suala kama hili likitokea, ni kuitangaza nchi yetu vibaya. Kwa hivyo, tunaomba Mhe. Waziri, naomba utakapokuja utuelezee ni hatua gani zilizochukuliwa katika kuhakikisha kwamba kijana yule Mzanzibari yule amepata haki yake.

Mhe. Spika, lakini katika hilo hilo, kwa kweli haipendezi. Bandari zetu sasa hivi ukipita pale, unachakuliwa, watu wanachukua mabegi yale wanachakua nguo za ndani. Si kitu kizuri kwa kweli, kwa nini mule kwenye Bandari hamuweki mitambo ambayo kwa kweli tukenda na wakati kuliko kupekuapekua mizigo ya watu? Vitu vyengine ni hatari kuonekana na watu wengine, ni aibu. (*Makofi*)

Mhe. Spika, tunaonekana sisi tupo katika karne ya 16 na wakati tupo kwenye karne ya 21. Bandari nzuri imejengwa pale. Leo ku-*search* mtu, maana yake mpaka umtawanyie nguo zake zote. Huo si ustaarabu tunaotaka na vile vile *Airport* ya Pemba tatizo hilo lipo kwamba lazima watu wakupige sasambure. Hatuna utaratibu huo na wala hatutaki utamaduni huo.

Mhe. Spika, jengine ni tatizo la ujenzi wa barabara. Katika kitu ambacho kinakula fedha nyingi ni ujenzi wa barabara, lakini kinachoonekana tumefeli ni katika ujenzi wa barabara, kuna barabara kama nilivyoeleza mwanzo zinachukua muda mrefu katika ujenzi wake. Tumeshuhudia barabara ya Amani/Mtoni ni hadithi ya kila siku, Wete/Meli-Tano ambapo munasema Wete/Chake Chake ambapo mimi siamini ni Wete/Chake Chake, ni Wete/Meli-Tano ni barabara ambayo ishachukua muda mrefu.Barabara ya Wete/Gando na Wete/Konde kwa kweli zimechukua muda mrefu. Hili linatuathiri sana kiuchumi, kwa sababu kama tulivyosema mara nyingi kwamba takriban suala hili kunakuwa kuna faini katika kukaa kwake na tulitaja hapa kwamba kila siku wizara ama serikali inatakiwa ilipe faini kiasi gani, tulilieleza hapa, ingawa Mhe.Waziri, yeye hatambui, lakini hili tulilieleza.

Mhe. Spika, yote hii ni kwa sababu ile ile kama Mhe. Hija Hassan Hija, alivyosema ni kukiuka masharti yaliomo sheria yetu ya fedha na manunuzi. Unapoanza kukiuka masharti ya sheria ukachukua wakandarasi wabovu waliokuwa hawana uwezo, ndio tatizo linalotokea katika barabara hizo tunazozizungumza.(*Makofi*)

Mhe. Spika, naomba sana tuwe makini sana na Waheshimiwa Wawakilishi, tuwe makini sana kwenye suala hili, lakini mbali ya kutaka barabara hizi zitengenezwe, tuna tatizo la hata hizo barabara tunazojengwa hazikidhi viwango, ni barabara mbovu. Waheshimiwa Wajumbe, ninawaomba sana tuzingatie sana suala la ujenzi wa barabara. Katika hili tuzidi kumuomba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ajaribu sasa kufanya ukaguzi katika eneo la barabara. Tunafungiwa kwenye ngulai, tunapigiwa ngulai. Barabara zinazojengwa sio ziliomo kwenye mikataba iliyoelezwa. Haiwezekani kwamba barabara kama tunapewa bure, kama ikiwa ni bure ni sawa, bure haina gharama, bure chochote tu hata kibovu, lakini ikiwa ni suala kwamba tunakopa au ikiwa ni suala ambalo barabara hizi tunazijenga kwa fedha kwa walipa jasho, haikubaliki kujenga barabara ndani ya mwaka mmoja, ikawa barabara haifanyi kazi, haikubaliki. (*Makofi*)

Mhe. Spika, Waheshimiwa, hilo...

Mhe. Spika: Una dakika tano.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, namuomba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ajielekeze katika hilo.

Mhe. Spika, jambo jengine katika suala la barabara ni suala la utunzaji wa barabara. Hebu Mhe. Waziri, utakapokuja utueleze mipango yako, kwa sababu hoja si kujenga, hoja ni namna gani wizara inasimamia katika kuhakikisha kuwa barabara zinatunzwa.Wenzetu Bara kule wameeka mezani katika kuhakikisha kwamba magari hayazidishi uzito. Leo hapa takriban ukitembea utaona magari yanazidisha uzito na yanatuharibia barabara.Wizara katika hili, Mhe. Waziri, naomba utakapokuja uniambie wizara yako ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba gari zinazopita katika barabara zetu ni zile ambazo ziliruhusiwa kwa mujibu wa viwango vinavyokubalika.

Mhe. Spika, jengine ni suala la kwamba wizara hii kadiri tunavyoizungumza wizara, tunazungumza na mashirika yaliomo ndani ya wizara. Tuna tatizo la kimsingi ndani ya serikali kwamba mashirika haya hadi sasa kama Mhe. Waziri, alivyoeleza kwamba hayatoi gawio lake katika serikali, hiyo acha na Mhe. Waziri wa Fedha mwenyewe atajua nini afanye, lakini tuna tatizo la kuweza kujua kama Wawakilishi kuweza kujua fedha ziliomo katika mashirika zinatumikaje na hoja yetu ya msingi ni kwamba Wawakilishi wawe na *access* ya kujua bajeti ya mashirika. Leo kwa kweli inakuwa ni mali ya watu wachache. Waheshimiwa Wawakilishi, hatufanyiwi haki, hatufanyi haki kama hatujui bajeti zinazoendesha katika mashirika ili tukajua kama shirika linakwendaje, hatuna uwezo huo. Naomba na serikali katika eneo hili waliangalie ili angalau na Baraza hili nalo liwe na fursa ya kuweza kujua.

Mhe. Spika, jambo jengine ni suala la ajali za barabarani. Katika jambo moja linalotusumbua ni ajali za barabarani. Hili kwa bahati mbaya kwamba serikali haina uwezo wa moja kwa moja kuliingilia, kwa sababu chombo chenye mamlaka ni taasisi ya Muungano ambayo sidhani kama Serikali ya SMZ ina uwezo wa kutoa amri moja kwa moja katika taasisi hii, lakini naomba serikali iwe makini sana, ajali barabarani zinaendelea kutuangamiza hasa katika hawa wenye vespa "tako moja" sijui au wadudu gani.

Mhe. Spika, wana tatizo hawa. Nchi inakuwa haina nidhamu watu wanajiendeshea tu vyombo vilivyokuwa havina utaratibu. Leo utapita mjini hapa, muache kama kijana anataka kuchukua aende Makunduchi huko kwenye barabara, muache aende akafe peke yake, lakini leo katikati ya mji unamkuta kijana kwa kweli mambo ya kihuni na nchi ina uongozi huu. Naomba sana mambo ya ajali barabarani hizi hasa kwa hawa mavespa, serikali ijaribu kuangalia ili tunusuru maisha ya vijana wetu pamoja na wengine ambao hawana hatia. (*Makofi*)

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo naomba nilizungumzie kuhusu kuwa tuna tatizo hapa la *ZANTEL*. Nilikuwa na mengi sana, lakini naomba kwa muda wako wa dakika zako tatu. Naomba niseme kwamba *ZANTEL* ni *proud* yetu Wazanzibari, ndio taaisisi pekee ambayo sisi tunaweza kujivunia, lakini ilielezwa hapa katika bajeti ya mwaka jana kwamba aliletwa *SO* hapa na *Etisalat* na lengo tukasema kwamba huyu alikuwa na njama maalum ya kuja kuiua *ZANTEL*, hapa kuja kuihamisha, tulisema suala hilo. (*Makofi*)

Mhe. Spika, leo *ZANTEL* ina *default* ya dola milioni mia moja katika taasisi hizi za Kimataifa. Tukisema ni *ZANTEL* ,maana yake tunakusudia ni fedha za serikali kwa sababu na serikali ina *share* katika *ZANTEL*. Tunaiomba serikali, namuomba Mhe. Waziri, atakapokuja atupe maelezo maalum katika suala la *ZANTEL*. Vipi serikali inalijua suala hili na vipi serikali imeliingia kati suala hili? Tunalihitaji kulijua kwa sababu dola milioni mia moja, ndani yake ni fedha zile za serikali ambayo kama ni deni, basi ni sehemu ya deni, basi serikali itakuwa inadaiwa ama serikali itakuwa inakosa mapato katika deni hilo ambalo *ZANTEL* itakuwa ni *default* ambao wanatakiwa walipe katika Makampuni ya mwisho.

Mhe. Spika, naheshimu nina mengi sana, lakini mwisho naomba nimuulize Mhe. Waziri, barabara yangu ya Msingini kwa sababu Dkt. Mhe. Mwinyihaji Makame alikuja akaniambia hapa kwamba barabara ile tayari ipo kwenye *pipe line*. Sasa naomba Mhe. Waziri, utakapokuja uniambie mkakati ambao utauchukua wa haraka sana kuinusuru ile barabara ili walau basi watu wa Msingini waweze kupita kama walivyopita kama miaka ya nyuma.

Mhe. Spika, leo sitozungumzia Bandari ya Wesha na *Airport* kwa sababu ninajua hadithi ni ile ile ingawa Mhe. Waziri na wewe katika Bandari ya Wesha na wewe ni mdau, lakini umeisahau.

Mhe. Spika, ninakushukuru. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana. Naomba sasa nimkaribishe Mhe. Suleiman Hemed Khamis, afuate Ali Salum Haji na baadae Mhe. Fatma Mbarouk Said.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Spika, na mimi nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuweza kutoa mchango wangu katika Wizara hii ya Miundombinu na Mawasiliano. Maelezo yangu yatakita kwenye kumbukumbu ambayo yatamgusa kila mtu, yatamgusa Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano na Waziri wa Fedha, kwa sababu hapa ni lazima yapatikane mashirikiano ya kutosha ili kuendeleza suala letu. Kwa hivyo, utakuta masuala mengi yamevia kutokana na kukosa mahitaji maalum. Kwa hivyo, nataka nianze kwenye kuonesha ule ushahidi kwamba mara hii tumepata bajeti ya kitoto na ni bajeti iliyokuwa haina msingi na ni bajeti ambayo kumbukumbu zake ni za nyuma, hakuna kipya hata kimoja kilichofanywa kwenye maelezo ya hotuba ya Mhe. Waziri. Katika maombi ya fedha ya mwaka 2013/2014 takriban maelezo ni yale yale. Ukiyasoma maelezo ya mwaka 2013 na ya 2014 utayakuta ni yale yale, isipokuwa kuna matatizo ya maombi tu ya kifedha, lakini utakuta kauli ni zile zile inayosema kwamba wizara imeweza kuidhinisha matumizi kwa bajeti iliyopita ya mwaka jana ya 2013/2014 bilioni 20. Katika bilioni hizi 20 za mwaka jana ndio bilioni 5.192 kwa ajili ya kazi za kawaida na bilioni 14. 90 zimeombwa kwa ajili ya kazi za maendeleo. Ukitizama bajeti ya mwaka huu ambayo ni 2014/2015 utakuta ni 14 bilioni badala ya bilioni 20, zimetoka bilioni 20 zikaanguka mpaka bilioni 14.077 kwa ajili ya matumizi ya wizara kwa mwaka huu 2014/2015 na bilioni 5. 677 kwa ajili ya kazi za kawaida na bilioni 8.40 kwa ajili ya kazi za maendeleo.

Mhe. Spika, utakuta mara hii Mhe. Waziri, hakupata bajeti kama ile ya mwaka jana, mwaka jana ilikuwa bilioni 20 na mwaka huu bilioni 14, sasa tutegemee nini hapa Mhe. Waziri, zile adhabu ambazo tuliziona mwaka jana na mwaka juzi na mwaka huu si zitakuwa zile zile, ikiwa kero tulizoziona mwaka ule na mwaka huu, si zitakuwa vile vile? Kwa hivyo, ushahidi unaonesha kuwa bajeti hii bado haijawa nzuri kwa mwaka huu.

Mhe. Spika, vile vile, nataka nizungumzie mambo ambayo mengine waliyataja ambayo nina wasi wasi kwamba mambo hayo mengine hayatoweza kufanywa, kwa mfano hapa wamesema kwamba kuna barabara ambayo itatengenezwa Ole-Konde, dhamira ni kufanya *maintenance* kidogo ambayo *periodic maintenance* ya barabara ile, lakini inaonesha urefu wa barabara hii kilomita 12.3, sijui nayo kama itatengenezwa, ni hadithi za ndani ya vitabu ambazo zinajirejea kila siku na maelezo ni yale yale, wala sidhani kwamba hii itafanywa, kwa sababu hizo barabara kubwa *main roads* zimeshindikana, siamini, lakini wamesema barabara hizi zitatengenezwa kutokana na mfuko wa barabara *UUB*, lakini na hiyo ahadi iliyotolewa kwa kufanya hiyo *maintenance* ya barabara hizi, zidhani kama nazo zitatengenezwa. Hayo ni maneno tu yamesemwa, tunayadhibiti na tutayachukua ili tuone kama kweli wizara hii itatekeleza hizo *maintenance* kama alivyoahidi katika maelezo yake.

Mhe. Spika, katika masuala ya mradi wa barabara tatu za Kaskazini ambayo inagharamiwa kwa mkopo kutoka Banki ya Kiarabu kwa maendeleo ya Afrika *BADEA*, ambao ndio hawa wanaochangia vile vile. Pia, na Mfuko wa Maendeleo ya Saudi Arabia *SAUDI FUND*, pamoja na fedha za serikali, michango hii bado inaonesha kwa kipindi kilichopita ilikuwa hali ni hiyo hiyo na kipindi hiki ni hiyo hiyo, ambayo inasema kwamba barabara za Kaskazini ukitizama ukurasa wa 8, unasema kwamba mradi huu unaogharamiwa kwa pamoja baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Benki ya Kiarabu *BADEA*, Mfuko wa Maendeleo wa Saudi Arabia unazijumuisha barabara za Wete-Konde kilomita 15 na Gando.

Mhe. Spika, ukitizama na kitabu cha pili kina maelezo haya haya. Kwa hivyo, huyu waziri yeye alikuwa hana haja ya kutuletea tena kitabu kipya, bora angetuletea kile kile cha mwaka jana tukaendelea na shughuli tukakizungumzia basi. Kwa sababu maelezo yaliyomo humu kwenye kitabu hiki cha mwaka jana na maelezo yaliyomo kwenye kitabu cha mwaka huu ni yale yale, hata *comma* na *fullstop* ziko vile vile hazijabadilishwa. Kwa hivyo, hapana chochote kilichofanywa mambo ni yale yale yanajirejea.

Mhe. Spika, sasa pamoja na hayo kwa ujenzi wa barabara ya Konde, kwa kweli mimi nataka nimuambie Mhe. Waziri, pamoja na Waziri wa Fedha, Bandari, barabara pamoja na Uwanja wa ndege, mambo haya yako karibu sana na macho ya watu. Kuna mambo mengine yamejificha, lakini mambo ya barabara, Bandari na Viwanja vya ndege, kwa sababu hawa ndio wanaotumia barabara, Bandari na ndio wanaotumia Uwanja wa ndege. Sasa mambo yake yakiazimiwa kufanywa yafanywe ili watu wayaone. Waangalie harakati za magari, hivi sasa kelele zimekuwa nyingi, mara gari ziko hapa na hizi ziko hapa. Harakati hizi zinazokwenda kwa kweli watu haziwaridhishi kwa sababu ni moja katika macho ya wananchi. Kwa hivyo, Bandari, Uwanja wa ndege, pamoja na sehemu nyengine ziko katika macho ya watu, tukifanya jambo tutafanya jambo la ukweli.

Mhe. Spika, kwa hivyo, miradi hii kwa kweli imezorota kwa kiasi kikubwa sana. Sasa tunasema hali ni ngumu kwa barabara hii ya Konde-Wete, barabara yetu ya Konde imekaa zaidi ya mwaka mzima haikutengenezwa,

ilitengenezwa kwa mara ya mwanzo ilikuwa nzuri, imekatika katikati, halafu imepigwa na mvua imeharibika barabara yote. Sasa hivi ndio wanaanza kuianza tena upya. Mimi nina wasi wasi Mhe. Waziri, kwamba hizi barabara hasa hii ya Konde kama itamalizika, kwa sababu hawa watu wa Kampuni ambao ni huyu *MECO,* yeye huyu katika kuendesha miradi yake, kwa sababu hapa Unguja alikuwa alipewa barabara akatengeneza na Pemba akapewa barabara tatu, alipewa Wete-Gando, Wete-Konde na Wete-Chake. Hizi barabara zote takriban hazikufanywa au zimefanywa nusu.

Mhe. Spika, Wete-Chake haikufanywa chochote, iliyofanywa nusu ni Konde-Wete na Wete-Gando. Kwa hivyo, kwa muda wa miaka yote tangu mwaka 2009, barabara hizi zimeanza kutengenezwa, angalia leo tuko mwaka gani, kwa kilomita 15 tu na barabara zote ni kilomita 15, isipokuwa barabara ya Wete-Chake ndio kilomita 22. Kwa hivyo, sisi hapa tumekaa kwa muda mrefu, watu wamepata maradhi makubwa sana kwa kipindi ambacho zinatengenezwa barabara zile, watu wamepata maradhi ya kifua kikuu kwa kutokana na vumbi la muda wa miaka miwili au mitatu, lakini barabara haijesha.

Mhe. Spika, vile vile, kuna watu ambao walivunjiwa majumba yao, wengine hawajamaliziwa kulipwa, kuna wengine nyumba zao zimepasuka bado hawajalipwa. Humu hatujaona chochote kwa watu ambao walipewa fidia zao. Kwa hivyo, suala hili limekuwa gumu na limekuwa zito. Mimi wasi wasi wangu ni kwamba hizi barabara zitashindwa kumalizwa, kwa sababu fedha aliyonayo haiwezi kumaliza kazi zake na niseme tu kwa ufupi kwamba kama mnataka barabara hii ya Konde imalizwe, basi nataka kusema kwamba alipwe fedha zake ambazo anadai ambazo bado hajalipwa. Anadai dola milioni 2,962,221 ambayo alikuwa akidai.

Mhe. Spika, pia, anadai pesa zilizokuwa zimebakia za Mazizini-Fumba, hizi nazo bado hajalipwa mpaka leo shilingi milioni 913,874,631, hizi bado hajaliwa, pamoja na pesa nyengine milioni 346,535,845, pia pesa hizi hajalipwa. Kama fedha hii hatolipwa huyu Kampuni hii, basi kuna uwezekano kwamba barabara ile ya Konde ambayo tunaitegemea imalizike, basi haiwezi kumalizika kwa muda huu mpaka pesa hizi zilipwe, kwa sababu na yeye amekopa pesa benki anahitaji kurudisha, hizo pesa alizolipwa za barabara ya Konde amelipa na bado anadaiwa mapesa chungu nzima huko benki. Kwa hivyo, ikiwa hapa serikali haitomlipa hizi pesa zake, basi kuna uwezekano barabara hii hapo ilipofikia pengine isiweze kutiwa lami, nina wasi wasi huo mkubwa sana. Nataka nimuulize Mhe. Waziri, una hakika kwamba barabara hii mara hii itamalizika, maana yake Mishanzo ndio inaendelea hivi sasa. Je, barabara hii ya Konde itamalizika.

Mhe. Spika, barabara ya Gando hata kuguswa haijaguswa iko vile vile tangu ilipoanzwa imetiwa kifusi imeachwa vile vile na hiyo ya Konde ina kifusi, haijafanywa chochote hivi sasa ndio wanaanza tena upya kuifanya kazi hiyo na barabara ambayo ni ya Wete-Chake nayo pia kuguswa haijaguswa. Sasa waziri tunafanya nini kwenye masuala haya, katika kipindi kile kilichopita na kipindi hiki barabara hazijaguswa na hizi kelele sio za Pemba tu, mpaka hapa Unguja barabara zote kwa kipindi cha miaka miwili. Bajeti iliyopita mwaka jana kulikuwa na zogo hapa kwa bajeti hii. Wajumbe wote walikuja juu hakuna kilichofanywa na barabara zote ni mbovu. Kwa hivyo, nasema na hapa inawezekana na kipindi hiki hakuna kitakachofanyika.

Mhe. Spika, mimi nasema pamoja na kushirikiana na Mhe. Waziri, suala hili tulihakikishe kwamba mara hii angalau barabara hiyo moja ya Konde imalizike. Pia, nataka nishauri kuwa hapa tuna wasi wasi wa aina ya barabara iliyotengenezwa za Finya-Pandani, Pandani-Mzambarauni, ambapo katika utengenezaji wa barabara hii tuna wasi wasi kwamba ile lami yake iliyotiwa sio lami ya ambayo ni *standard*. Kwa hivyo, Mhe. Waziri, nakuambia kabisa na mimi natoa sababu zangu kabisa nasema tusije tukatiliwa lami kama ambayo iliyotiwa njia ya Mzambarauni-Pandani Finya, hatuitaki lami kama ile, ile ni lami hafifu na nyinyi mtaiona baada ya muda mfupi itakavyoharibika na halafu inasababisha ajali chungu nzima kutokana na ule muundo iliyotengenezwa barabara ile. Hilo pia nilitaka niliseme.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo ya barabara tatu ambazo Mhe. Waziri, nilitaka nimuulize. Je, ni lini hasa barabara hii ya Konde-Wete itamalizika, hilo swali langu moja, lakini swali la pili, nataka kidogo nizungumzie katika Bandari hizi mbili, Bandari ya Wete na Bandari ya Mkoani. Kwa kweli inasikitisha na kwa muda ambao Bandari hizi mbili, Bandari ya Mkoani na Bandari ya Wete zimeachwa kwa muda mrefu bila ya kushughulikiwa na tulikuwa tuna mategemeo kwamba angalau Bandari ya Mkoani ni nzuri kidogo itafika mahala pazuri, lakini mpaka sasa hivi Bandari ya Mkoani bado iko katika hali iliyokuwa sio ya kuridhisha. Kwanza kwa hali ya hewa ambapo ikinyesha mvua, basi ina maana watu wote watarowa na vitu vyao vyote walivyochukua vitarowa, kwa sababu hakuna pahala pa kujificha mvua, hilo ni kosa kubwa sana.

Mhe. Spika, jengine ukitizama katika hii Bandari ya Wete ambayo haijafanyiwa matengenezo yoyote, ambapo kuna uwezekano wa kuwa Bandari ile inawakosesha raha watu, meli kutoka hapa kwenda mpaka Wete na Wete zikaenda Tanga. Hivi sasa ni matatizo makubwa, watu wanategemea biashara zao kutoka Tanga, kama unavyotegemea Dar-es-salaam-Unguja na Tanga-Pemba. Kwa hivyo, inakuwa ni mashaka makubwa sana kwa sababu hakuna utaratibu wa meli zinazofanyakazi.

Mhe. Spika, baada ya bandari hizi mbili kuzizungumzia. Pia, nataka nizungumzie juu ya hii *MV*. Maendeleo ambayo ni meli ambayo tunaitumia kila siku...

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, una dakika tano.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Spika, haya ahsante. Meli hii ya *MV*. Maendeleo kwa kweli hairidhishi katika usafi wa ndani. Namuomba Mhe. Waziri, meli hii ya *MV*. Maendeleo iangaliwe kwa vizuri sana, maana yake watu wanapata maradhi mule ndani, meli ni chafu sana. Kwa hivyo, nakuomba Mhe. Waziri, ile meli iangalie bwana, watu hawahishughulikii kwa usafi, meli ya zamani, lakini utunzaji ni mdogo katika meli ile.

Mhe. Spika, jengine ambalo nataka nilizungumzie kwa mujibu wa dakika zangu ambazo zilizobakia ni suala zima la Kampuni ya *ZANTEL*. Awali *ZANTEL* ilikuwa ndio watu wa Unguja walikuwa wanaitegemea sana kwa muda miaka yote, lakini leo katika Kampuni iliyokuwa ni mbovu kabisa, basi ni hii ya *ZANTEL*, pamoja na kuwa sisi sote tuliokuwemo humu kwenye Baraza tunatumia hii Kampuni ya *ZANTEL*. Sasa hivi Kampuni ya *ZANTEL* imeanza kushindwa na kwa sababu watu wamesema muangaza mbili, basi moja humponya.

Mhe. Spika, yule bwana wa *ZANTEL* alikuwa yeye ndio *permanent* kwa hapa Zanzibar, kaona labda hapa hapati na ukifanya tathmini idadi ya watu ambao walio wengi ni Zanzibar kuliko huko anakokwenda, huko anakokwenda hawezi kupata kitu kwa sababu yeye kaelemea Dar-es-salaam na mamlaka yake na mambo yake yote kapeleka Dar-es-salaam, hawezi kuipiku *VODACOM*, hawezi kuipiku *TIGO* hata siku moja. Kwa hivyo, yeye ni tiro tu, ni sifuri, badala ya kushughulika na hapa Zanzibar, akaiwezesha vizuri Zanzibar, tukapata mawasiliano mazuri. Leo mawasiliano ya *ZANTEL* hapa Zanzibar haipatikani, badala yake unaambiwa ikiwa unataka upeleke ujumbe wa sauti, hii ni Kampuni gani tena ya ujumbe wa sauti.

Mhe. Spika, lakini ukiigusa *AIRTEL*, basi tayari ina *full network*, lakini ukienda kwenye *ZANTEL*, *network* hakuna, ukienda kwenye *TIGO full network*, ukienda kwenye *ZANTEL*, hakuna, ukitaka peleka ujumbe kwa njia ya sauti, tunakwenda wapi na Kampuni hii na hao watu wameshahama hapa, wako Dar-es-salaam, ule urafiki umeshamalizika, wameshaitupa hasa hawana habari na hii Zanzibar.

Mhe. Spika, kwa hivyo, hasa Zanzibar sisi *ZANTEL* inakufa. Je, Mhe. Waziri, unatuambia vipi kwenye Kampuni hii ambayo tumeianzisha sisi zamani ndani ya mikono yetu na hii ni yetu, lakini hali ya sasa hivi ya Kampuni sio nzuri, haina *network*, haifurahishi na ukitaka sasa labda uwe na *line*s mbili utie *ZANTEL*, utie na *AIRTEL* ili upate angalau mnara wa *AIRTEL* upate kuzungumza, bila hivyo kwa kutegemea *ZANTEL* peke yake, basi utaambiwa hapatikani, kila wakati hayupo, msubiri kidogo, tumia sijui sauti na mambo chungu nzima. Kulipisha tu, hujapiga simu umeshaambiwa shilingi mia umeshakatwa, hujazungumza naye mtu, basi umeshakatwa shilingi mia au mia mbili.

Mhe. Spika, kwa hivyo, tunamuomba Mhe. Waziri, hii Kampuni watuambie kama wanaitaka na kama hawaitaki, hapa yako Makampuni mengi tutajiunga, maana yake wao wameshatukimbia hawapo hapa wako Dar-es-salaam na mambo yao wanafanyia huko huko, lakini hawapati kitu huko, watapata tabu bure, hawatoki mbele ya *VODACOM* na *TIGO* hawatoki warudi huku huku Zanzibar. Kwa hivyo, kama wanataka tuendelee mwambie atengeneze Kampuni yake iwe nzuri au na sisi tutatoka tutaingia kwenye Kampuni nyengine, simu zetu zote tutapeleka kwenye Kampuni nyengine, kwa sababu hii haitusaidii kitu sasa hivi. Kuna *TIGO* zipo tele, *AIRTEL* ziko ukigusa tu.

Mhe. Spika, kwa sababu muda wangu ni dakika tano uliobakia na mimi nakushukuru, naunga mkono, lakini haya yangu yote niliyomwambia Mhe. Waziri, ayachukulie hatua na tuone maendeleo katika nchi yetu. Ahsante sana.

Mhe. Spika: Ahsante sana, kwanza nimkaribishe Mhe. Ali Salum Haji, baadae Mhe. Fatma Mbarouk Said na hatimaye Mhe. Salmin Awadh Salmin.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Spika, ahsante na mimi nichukuwe fursa hii adhimu kukushukuru kuweza kunipatia fursa hii ya kuweza kutoa angalau machache katika Wizara hii ya Miundombinu na Mawasiliano.

Mhe. Spika, mimi leo nitazungumza katika hali ya unyonge sana, kwa sababu tumeshapiga kelele sana na tumeshazungumza sana katika wizara mbali mbali, lakini wakati mwengine unakuta mambo ndio hayo hayo na Waswahili wanasema; "muungwana ni vitendo". Sasa sioni haja ya kuendelea kupiga makelele nikaumiza kichwa katika mambo ambayo huoni mabadiliko yake kwa haraka sana.

Mhe. Spika, kwanza nianze kwa kutoa pongezi, niwapongeze ndugu zetu wa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa ujumla ambayo iko chini ya Mhe. Waziri mahiri, kaka yangu Mhe. Rashid Seif Suleiman na Naibu Waziri wake pamoja na watendaji wake wakuu, kwa namna wanavyojitahidi katika kufanyakazi katika wizara hii. Mimi nasema naipongeza na naangalia zaidi jitihada na mafanikio. Kuna watu wanasema kwamba panapo mafanikio, basi na kasoro haziwachi, kasoro kweli zipo na faida pia zinaonekana.

Mhe. Spika, nataka kuangalia maeneo mawili tu ambayo yameonekana yana jitihada katika wizara hii. Eneo la kwanza nilipongeze Shirika la Bandari kwa namna wanavyopiga hatua katika kuleta mabadiliko kwenye taasisi yetu. Mabadiliko katika uendeshaji wa kazi, lakini mabadiliko katika masuala mazima ya kukuza uchumi au kuongeza mapato katika kitengo kile.Vile vile, nimpongeze Mhe. Rais kwa kufanya ziara ya ghafla tu juzi na kujionea mwenyewe hali halisi ya maendeleo katika bandari yetu.

Sasa niseme tu pamoja na jitihada ambazo anazozifanya na changamoto alizokuwa nazo na ile changamoto kubwa ambayo Mhe. Rais ambayo ameiona ya ufinyu wa eneo unaotokana na wingi wa makontena. Hivyo, niwaombe tufanye jitihada katika kufanikisha yale ambayo Mhe. Rais amewashauri, ili bandari yetu iweze kufanyakazi na hatimae tukisubiri Bandari yetu ya Mpigaduri, kwa ajili ya kutanua wigo katika suala zima la wafanyabishara wetu.

Mhe. Spika, katika suala zima la barabara naomba niseme tu, kwamba ninaipongeza serikali kwa jitihada inazozifanya na nilikuwa najaribu kuumiza kichwa na wakati mimi nimezaliwa katika miaka ya 1960's na *references* mbazo ninazo, kwamba nilikuwa nikitaka kwenda Makunduchi lazima nikalale kwenye gari na halafu siku ya pili ndio nije mjini. Lakini tunashukuru hivi sasa ukiniambia niende Makunduchi dakika 25 au 30 na kwenda na kurudi.

Kwa hivyo, naipongeza kwa jitihada za karibuni tu, katika ujenzi mzima wa barabara. Kwa mfano, juzi tu tumeshuhudia barabara tofauti zimekuwa katika hali nzuri kama vile barabara ya Dunga/Amani, Tunguu/Kinyasini, Paje/Makunduchi pia Uroa/Kiwengwa. Hata hivyo, barabara za Kwahani kutoka sheli mpaka Mwembenjugu na Kutoka Kwalamsha mpaka Kwajumapweza nashukuru. *(Makofi)*

Niseme kwamba panapo mafanikio na changamoto hazikosi na nimesema mwanzo na changamoto nitakuja kuzieleza baadae na kuwataka wenzetu watafute namna zaidi ya kuweza kubadilika kuona hali halisi ya namna gani wanarekebisha. Kwa kweli tunajua sote kwamba tatizo la nchi yetu ni ufinyu wa bajeti. Kwa hiyo, hata tukiendelea kutoa lawama na sio kusema tu hata kama tutawashikia mikwaju kama fedha hakuna hakuna, kitu ambacho kinaweza kufanyika katika hali ya uharaka kabisa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, pamoja na yote ambayo nimejaribu kuyazungumzia katika suala zima la pongezi. Nataka nimuombe Mhe. Waziri pamoja na timu yake akiwemo na Mkurugenzi wa Barabara (UUB) kupitia kwako Mhe. Spika, kuna tatizo ambalo linaniumisha kichwa kwa muda mrefu; watu wanasema kwamba usitake neema na baada ya kupata ikawa karaha, mimi niliomba ujenzi wa barabara Mikunguni/Mwembenjugu na barabara nashukuru imejengwa.

Mhe. Spika, lakini barabara ile ina historia yake, yaani barabara ile kabla ya kukarabatiwa ilikuwa na matuta, sasa matuta yale yameondoshwa na idara wakati wa kufanya ukarabati, sasa huwa ninapata kigugumizi na nimeshawahi kuuliza na kusema sana na nikijibiwa naambiwa peleka maombi. Mhe. Spika, juzi nilimnukuu Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria alisema kwamba "Jambo lolote linapokaa kwa muda mrefu na hata kama halikuwa katika sheria, suala hilo inakuwa tayari ni sheria".

Mhe. Spika, naambiwa labda Mwakilishi wako miaka yote hakuomba na haya matuta yaliekwa karibu miaka 13 au 14 na Mwakilishi aliyepita hata kama Mwakilishi hakufuata taratibu kama yamedumu kwa muda mrefu na yamesaidia jamii katika eneo lile ah! Kuna sababu gani ya kutokuyarejesha.

Sasa ninaomba sana kwamba matuta yale yarejeshwe, kwa sababu kutokuwepo matuta yale kumeshaua watu wengi sana, kwani kutoka kwenye barabara mpaka kwenye nyumba kuna baadhi ya maeneo hata mita moja haifiki, na wanaoathirika zaidi ni watoto wadogo na wala sipendi kumzungumza sana Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano maana yake aliwahi kumtolea mfano Mhe. Jaku Hashim Ayoub kuhusu kima na watu na alisema kwamba wale kima hawanaakili.

Kwa hivyo, namuomba aelewa kwamba kuna barabara kubwa watu wazima ndio wanaozitumia sana, lakini barabara zetu za maeneo ya ndani zinatumiwa zaidi na watoto wadogo, yaani mtoto mdogo anatoka ndani ya nyumba anashindwa kuangalia kama vile umri wa miaka mitatu au minne. Sasa mimi nafikiri wale huwa sawasawa na hao kima ambao hawataki yeye, kwa sababu watoto wadogo pia hawana akili. Hivyo, ni vyema awasaidie watoto wadogo na ndio hasa wanaogongwa.

Mhe. Spika, tayari nimeshuhudia matukio mawili ambao wananchi wangu walitaka kuchukua hatua mikononi nikawazuia, pia ilitaka kuchomwa pikipiki nikazuia, kuna mtu alitaka kukatwa miguu kama alivyomkata mwenzake nikazuia na hali hii ya kuzuia itakuwa mpaka lini. Kutokana na hali hiyo, naomba matuta yarejeshwe, kwa ajili ya kuwanusuru wananchi wa Mwembebeni katika barabara yao ambayo wamesaidiwa na idara yetu.

Vile vile kuna saula la hizi barabara ambazo zinazofanyiwa matengenezo; barabara ya Koani/Jumbi na mwenyewe hayupo hapa na nilitembelea Jumapili iliyopita na Mhe. Mussa Ali Hassan kwa ajili ya kwenda kuangalia jamaa zake wa jimbo lake.

Katika kitabu chake Mhe. Waziri ameeleza namna alivyoitengeneza ile barabara katika hatua za awali, lakini ninamuomba aende akatembelee katika siku mbili hizi. Kwa kweli ile kuzisafisha imekuwa kero kwa wale wananchi. Barabara hivi sasa kama ukitaka kwenda kwa gari ndogo, labda utafute baskeli vyenginevyo kwa gari huwezi kufika. Mhe. Spika, haya ndio yale mapungufu, tufanye jitihada kwa hawa mafundi wetu, ili kuharakisha hizi kazi kwa lengo la kuondosha usumbufu.

Mhe. Spika, katika suala la barabara nataka nimalizie kwa barabara Mfereji wa Wima na Kwabiziredi. Kwa kweli barabara hii imekuwa na mtihani mkubwa na zinaleta kadhia pamoja na kwenye kitabu tumeona kwamba kuna mpango huo wa kufanywa utanuzi. Kwa hiyo, zaidi tunaomba jitihada Mhe. Spika, kwa sababu tunajua mfuko wetu ni mwepesi sana, lakini jitihada zinahitajika kwa kushirikiana na wafadhili wetu, ili tuone tunafikia hatua gani.

Nikiendelea na mchango wangu Mhe. Spika na ninazungumza kwa haraka haraka nataka nizungumzie suala zima la *Airport*. Waheshimiwa Wajumbe wengi wamezungumzia na kila mjumbe amesema na vyake. Lakini kweli mapungufu ya *Airport* yako mengi sana na mimi mwenyewe kadhia imeshanifika na nikapambana sana.

Kwa hivyo, nadhani niiombe wizara kupitia kwako Mhe. Spika, na tunawaomba sana lakini inafika pahala unaomba na kuchoka. Mhe. Spika, ni vyema wafanye maamuzi magumu katika suala zima la Uwanja wa Ndege, kwa ajili ya kuondosha usumbufu kwa wananchi wetu wanaosafiri na wale wanaowasili. Katika uwanja wetu limekuwa ni tatizo sugu na viongozi wengi wameshateseka pamoja na kuadhirika.

Kutokana na hali hiyo, naomba juu ya kutafuta namna ya jitihada katika kulisaidia lile eneo na nimetembea juzi nimekuta vile vibango angalau usishushe abiria hapa katika lile eneo ambalo tulikuwa tukipiga kelele vimeshaondoshwa tunashukuru kwa hilo. Pia si vibaya kuwapongeza baada ya kuona mandhari ya uwanja wa ndege wetu imeanza kubadilika. Sasa ndio ninaposema kwamba panapomazuri na mabaya hayakosi.

Zaidi ambalo nataka kulizungumzia Mhe. Spika, lenye kutupa ugumu na kutupa mashaka ni suala zima la usalama katika eneo leo ya uwanja wa ndege. Kwa kweli wengi wamezungumza lakini na sisi bado tunapata kigugumizi katika suala la mabegi ya madawa ya kulenywa nayavyoingia ndani. *(Makofi)*

Sasa ikiwa mtu anafika kupitisha mabegi sijui usalama wa wananchi uko katika hali gani na unapata mashaka, kwa sababu watu wengi wamezungumzia *CCTV* lakini ah! *CCTV* ni sehemu moja, labda tuulizane hakuna walinzi wa kuangalia au pengine hizo mashine, maana mtu kapita na begi bila ya kupitishwa kwenye mashine, kwa sababu unaweza kujiuliza mambo mengi. Mhe. Spika, tunaomba tuletewe ripoti ya watu walioingia na mabegi hatua zilizochukuliwa na mpaka hatua zilizofikia, kwa ajili ya kuweza kujiridhisha.

Nikiondoka hapo Mhe. Spika, sasa naomba nizungumzie kuhusu Idara ya Leseni. Mhe. Spika, samahani kidogo kabla ya kuingia kwenye Idara ya Leseni kuna jambo nimeliacha na leo limenikaa na roho sana. Waswahili wanasema kwamba ukitaka kuona raha ya jambo, ulifanye mwenyewe na kuna misemo mingi tu.

Mhe. Spika, jana ulipokuja ulituasa sana katika suala zima la nidhamu katika Baraza lako na hususan kuhusu suala la mahudhurio. Vile vile ulisema kwamba sisi mara nyingi tunawanyoshea watu vidole katika kuibana serikali katika matumizi mabaya, lakini kumbe sisi wenyewe Wawakilishi nidhamu haiko vizuri.

Kutokana na hali hiyo, kuna suala ambalo linamgusa kiongozi na ni Mwakilishi wa Baraza lako hili tukufu na wala sina haja ya kumtaja jina, ambae anahusiana na Kampuni ya *ZAT* ya Uwanja wetu wa Ndege. Baada ya utafiti wa kina na ufuatiliaji ninayo taarifa kwamba Kampuni ya *ZAT* hailipi ipasavyo mapato katika uwanja wetu wa ndege katika kuhudumia eneo lile. Sasa kama sisi tunapiga kelele watu kulipa kodi lakini kama sisi wenyewe tunakwepa kodi, hili ni tatizo. *(Makofi)*

Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri wa Fedha kupitia kwako Mhe. Spika, wakati wa kuja kufanya majumuisho anipe maelezo ya kina katika ulipaji kwa Kampuni ya *ZAT*, tunaidai kiasi gani na kwa muda gani na pia nimtake lini kampuni hii itatulipa, ili serikali iweze kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Mwenyezi Mungu huwa anampa mtihani mwanadamu kwa kumtizama imani yake. Kwa mfano, Nabii Ibrahim alipewa mtihani na Mwenyezi Mungu wa kumchinja mwanawe, lakini kwa ajili ya imani na utiifu kwa Mwenyezi Mungu, aliweza kuchukua hatua na Mwenyezi Mungu alimsamehe na kumwambia achinje mnyama na sisi tunaweza kunyosheana vidole wenyewe kwa wenyewe. *(Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu sasa naomba nizungumzie kuhusu Idara ya Leseni. Mhe. Spika, kwenye idara hii ninayo mambo mawili tu nataka niwasaidie ndugu zangu.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, unazo dakika tano.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Spika, nitamaliza juu ya msitari dakika zako.

Jambo la kwanza kwa Idara ya Leseni ni kuwataka kusimamia ipasavyo. Mhe. Spika, kumekuwa na kawaida kwa maafisa wa Idara ya Leseni kuingia kwenye magari kutizama zile gari ambazo hazifiki mwisho wa *route*, ambazo zinawatesa wananchi wetu na hususan wagonjwa na wajawazito na zaidi ni *route* ya kufika Hospitali ya Mnazimmoja.

Sasa zoezi hili Mhe. Spika, linakuwa halina utaratibu mzuri, kwa sababu utaratibu wake wakati mwengine unafika miezi mitatu na hata sita ndio wanakuwa wanafanya siku moja. Kwa hivyo, kuhusiana na suala hili nawaomba kupitia kwako Mhe. Spika kwamba wajipange katika hili, ili kuondosha wale wakorofi.

Jambo jengine Mhe. Spika, nakwenda haraka haraka katika suala zima la hizi gari ambazo tunazipa leseni. Kwa kweli hapa Zanzibar hivi sasa Mhe. Spika huijui gari ya abiria, gari ya mizigo wala gari ya *private* na hivyo tunapata mashaka. Matokeo yake hivi sasa ajali zimekuwa nyingi ambazo si za lazima na hususan katika hizi gari zetu za aina ya *carry* ambazo zimeingia hivi sasa na vinachukua vijana wengi kama vile kupeleka kwenye michezo ikiwemo mpira wa miguu na imekuwa zinasababisha ajali nyingi za mara kwa mara.

Kwa hivyo, ninawaomba kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba tunapotoa leseni kwa gari zetu tuwe tayari kuzifuatilia, ili kuona kwamba wanafuata yale masharti walioruhusiwa.

Mhe. Spika, jengine kwa sababu ya muda wako kuna suala hapa nataka nilizungumzie tena ninayo *document* na nitampa Mhe. Waziri kwa ajili ya kuiangalia na kuweza kumsaidia katika suala zima la kuanzisha Skuli ya Usalama wa Barabarani. Kwa mfano, kule Dar-es-Salaam kuna Skuli ya Usalama wa Barabarani, lakini skuli ile mara nyingi tunawapeleka madereva wetu wa viongozi na wala madereva wetu wa kawaida huwa hawapati mafunzo katika suala zima la usalama barabarani na kupelekea kutokufahamu na kutokutii sheria.

Kutokana na hali hiyo, ninaomba kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba wizara hii na *document* nitampa Mhe. Waziri kwa ajili ya kuiangalia, ili baadae aone namna gani na sisi Zanzibar tunaanzisha hiyo skuli.

Mhe. Spika, la mwisho ninayo *hansard* hapa na wala sitoisoma hata kidogo kwa kujali muda wako Mhe. Spika. *Hansard* yenyewe ni Ripoti ya Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi iliyosomwa tarehe 3 Februari, 2014, ambayo aliulizia juu ya mapato kutoka Taasisi zetu za Muungano ikiwemo *TCRA, TPDC, TCAA*. Hivyo, nataka kujua, ili Mhe. Waziri wa Fedha atakapokuja ataweza kutusaidia, labda wamefikia hatua gani katika kuona kwamba Zanzibar na sisi tunanufaika katika mapato haya ya mashirika yetu matatu, ambayo tunaungana nayo katika suala zima la mawasiliano.

Baada ya kusema hayo, Mhe. Spika naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja na ninaomba tumuidhinishie Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano fedha kwa ajili ya kwenda kufanyakazi kwa utulivu. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, sasa naomba nimkaribishe Mhe. Fatma Mbarouk Said, afute Mhe. Salmin Awadh Salmin na baadae Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi, wakati Mhe. Asha Bakari Makame anajitayarisha.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Mhe. Spika, ahsante na mimi kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia machache katika bajeti hii ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Kwanza nimshukuru Mhe. Waziri, Mhe., Naibu Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kutuwasilishia bajeti hii. Mhe. Spika, kama kawaida siku zote huwaomba wenzangu kwamba tuisome, tukosoe, tutoe mawazo yetu na baadae tuipitishe bajeti hii. *(Makofi)*

Mhe. Waziri, ametuonesha kwamba wizara hii inazo taasisi mbali mbali na zote zinahitaji kupata fedha kwa ajili ya kuendesha mambo yake tofauti. Mhe. Spika, niseme kwamba nitakuwa tofauti kidogo na wenzangu, kwa sababu kuna miradi hii ya barabara, kwenye ukurasa 9 kuna mradi wa barabara Wete/Chake Chake, Ole/Kengeja, pia kuna mradi wa barabara zinazotoka mjini Unguja na zote hizi wenzangu wamesema kwamba kuna marejeo pengine ya miaka mitatu.

Mhe. Spika, nadhani ni haki yao kufanya hivi ikiwa miradi hii haikutimizwa, ingekuwa ni jambo la ajabu sana kutafuta miradi mingine bila ya hii kuikamilisha. Kwa kweli kwa upande wangu naona ni jambo la busara kwanza kuonekana kwamba hizi barabara ambazo zimo katika mpango huu zinakamilika.

Nikiendelea na mchango wangu naomba kumuuliza Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, kwa sababu na mimi ninayo barabara ndogo sana ambayo imo ndani ya Ilani ya Uchaguzi na mpaka leo hii bado haijatizamwa. Vile vile niliwahi kuuliza swali siku moja, lakini sikupata jibu na niliambiwa iko chini ya Baraza la Manispaa na imo kwenye Ilani ya Chama changu cha Mapinduzi.

Kwa hivyo, ninamuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, wakati atakapokuja hapa anieleze kwa usahihi zaidi kwamba barabara hii nimuendee nani, ili iweze kujengwa kutoka Amani Fresh kuelekea Mboriborini.

Mhe. Spika, idara zote hizi pamoja na wizara nzuri na mimi nitasema kwa ufupi tu kwa kuokoa muda wako Mhe. Spika na matatizo ambayo tumeyaona, kwamba miradi mingi ya barabara haikukamilishwa. Hali hii ni kwamba serikali yenyewe ndio ilikuwa inaisimamia miradi hii ya ujenzi wa barabara hizi pamoja na misaada ya wahisani, lakini bila ya kuwa na nguvu sisi wenyewe, yaani tukawa na nguvu ya *revenue* ama keki ambayo tunaikusudia ikiwa ni ndogo hatutoweza kufanya lolote na itabakia tu kuwa ni miradi ambayo itakuwa haitekelezeki.

Ninaiomba serikali kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba kile kidogo kinachopatikana, kikatumika kwa ufanisi zaidi tena kwa uwazi pamoja na uwajibikaji mzuri, ili tuweze kukamilisha hizi barabara ambazo tumezitia kwenye kitabu hiki.

Sasa naomba nizungumzie Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara ambayo iko kwenye ukurasa wa 24 kuhusu Sekta ya Usafiri wa Nchi Kavu. Mhe. Spika, naomba kunukuu kidogo;

Ukurasa wa 24 kuhusu Sekta ya Usafiri wa Nchi Kavu, unaeleza hivi:-

"Katika kipindi cha mwaka 2013/2014 Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kupitia Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara na Idara ya Usafiri na Leseni imeendelea kuimarisha miundombinu ya barabara na huduma za usafiri wa barabara kwa kuendeleza kazi za ujenzi na utunzaji wa barabara, madaraja na kusimamia usalama wa barabarani".

Mhe. Spika, hili ni jambo zuri tena ni la msingi kabisa. Hata hivyo, kama nilivyosema kwamba hizi barabara mbazo zinajengwa ziwe na kiwango kile ambacho kinakubalika katika masuala ya utendaji mzuri wa hizi barabara, kwa sababu kama walivyotangulia kusema wenzangu kwamba barabara hizi zinakuwa hazina viwango. Kwa hivyo, naomba kupongeza kwa hicho kidogo ambacho wanakifanya tuwape moyo, ili waweze kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

Nikienda ukurasa wa 29 kuna Idara ya Usafiri na Leseni ambayo tayari nimeshaizungumza. Lakini kuna sekta ya mawasiliano ukurasa Nam.31 kwamba sekta ya mawasiliano imeendelea kutoa mchango mkubwa katika ukuwaji wa uchumi na huduma za kijamii katika nchi yetu na inajumuisha utoaji wa huduma za mawasiliano kwa njia ya posta, simu na huduma za teknolojia ya habari. Ni kweli Mhe. Spika, kama alivyosema mwenzangu Mhe. Mgeni asubuhi hii ni ya kupigiwa mfano na ni lazima twende na wakati ambao dunia imeshasonga mbele na kwa sababu na sisi ni sehemu ya dunia basi ni lazima tufike huko ili kurahisisha mambo.

Hii teknolojia ya habari nafikiria inarahisisha mengi, hata juzi kwenye semina tuliona namna gani hata hilo tatizo la sasa hivi mara nyingi tunasema kwamba Wizara ya Elimu hasa kwamba haina walimu wa sayansi, kwa hivyo tukitumia teknolojia hii ya habari kuna hii *Education* ambayo pia inaweza ikasomeshwa moja kwa moja bila ya kuwepo mwalimu. Kwa hivyo na hii na mimi nasema Serikali ijitahidi kutumia teknolojia hii ili kurahisisha mambo yake.

Mhe. Spika, kuna sekta ya usafiri wa anga; ukurasa wa 35 mpaka 36 ambayo ina mamlaka ya viwanja vya ndege ambavyo vile vile ni muhimu ni lazima viwe na *standard* viwanja hivi na lazima viwe vya kimataifa na kwa sababu nimeona kwamba kuna matatizo mengi, hata *ex-ray machine* ni mbovu, kwa hivyo ningeomba mamlaka hii ikatizamwa kwa jicho la huruma na sio jicho la huruma tu kwa sababu maeneo haya yote yanatusaidia katika kukuza pato la taifa letu.

Kwa hivyo Mhe. Spika, hili Mhe. Waziri wa Fedha pia alitizame suala hili kuhusu kuipa ile pesa ambayo itatosheleza ingawaje alinijibu katika kipindi kilichopita kwamba haiwezekani pesa hizi wakaachiwa, na kwa sababu kuna hospitali labda wao watakuwa hawana makusanyo nikaona kwamba ni vizuri basi yakatizamwa yale mambo muhimu itasaidia.

Mhe. Spika, kuna usafiri wa baharini kuna shirika la meli na uwakala na Shirika la bandari vile vile ni mashirika muhimu, na vile vile ni kwamba mimi najenga kidogo mashaka kwa mashirika haya kwamba yanakuwa muda mwingi baada ya kwenda mbele tunarudi nyuma, maana yake mimi nilitegemea labda kama mashirika haya yanakwenda kibiashara basi na meli mbili kwa kweli haisaidii.

Sisi tulitaka siku moja tusikie meli zetu zipo za kutosha lakini leo tuna meli mbili na moja ni meli ya mafuta ambayo imekodiwa, nimeona kwenye kitabu humu, lakini vile vile kama tunakwenda kibiashara basi siku moja tujaalie kwamba tutakuwa na meli hata kama hapa kwetu zitakuwa hazina kazi za kufanya tunaweza kuzikodisha na zikafanya hiyo kazi. Mimi ningefurahi sana.

Mhe. Spika: Waheshimiwa wajumbe Mheshimiwa anaendelea kuchangia nadhani tungemsikiliza ingekuwa vizuri zaidi kama tunazungumza tuzungumze kwa kunong'ona.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Mhe. Spika, ningefurahi sana siku moja tukaona kwamba shirika la meli lina meli nyingi zaidi tusiwe na meli mbili na meli zenyewe zimeshachakaa, lakini hata hivyo kama ni kibiashara basi tuweze kuzitumia meli hizi hata kwa kuzikodisha nje; zitafanya kazi katika Afrika ya Mashariki na kwengineko ili tukalikuza hili shirika. Lakini tumelikuta shirika linakuwa mali zake za mpito yaani *current assets* na dhima za mpito zinakuwa kama zitakuwa hazina uwiano basi Mhe. Spika, ni kwamba suala hili kwa kweli shirika hili litakuwa haliwezi kujiendesha kwa faida.

Mhe. Spika, vile vile tuna Shirika letu la bandari ukurasa wa 43; Shirika la bandari lina jukumu la kutoa huduma za uingizaji na utoaji wa meli katika bandari za Unguja na Pemba ufungaji na ufunguaji wa meli kwenye gati. Uangalizi wa alama za kuongezea usafiri wa meli minara na maboya, uteremshaji na upakiaji wa bidhaa kwenye meli. Kwa kweli Mhe. Spika, hii ni kazi nzito na ngumu lakini vile vile inahitaji fedha nyingi, Mhe. Spika, vile vile linahitaji kujiendesha kwa faida. Kwa hivyo ningependa sana vyombo hivi na hasa haya mashirika vinataka kujiendesha wenyewe kwa hivyo ningependa sana wakawa wawazi na wawajibikaji. Tunajua kwamba sasa hivi Mkurugenzi aliyekuwepo pale anastahili sifa kwa kazi hizi kuziendesha vizuri.

Mhe. Spika, baada ya yote haya niseme kila kitu kinatakiwa uwajibikaji zaidi. Barabara zetu kama nilivyosema mwanzo kwamba zinahitaji bila ya kusema kwamba tunakwenda kwengine na ingekuwa ni jambo la kuchekesha kusema kwamba tunakwenda kwenye mradi baada ya njia zile ambazo tumezitaja huko nyuma, na tukaenda na barabara nyengine, kwa kweli ingekuwa ni vichekesho.

Tutizame mikataba kama inatekelezeka na wakandarasi nao vile vile kama walivyosema wenzangu; kwamba mkandarasi awe na viwango vile vile, tukichukua mkandarasi kwa kusema tuchukue mikataba yao kutokana na bei zao na thamani zao, kwa kweli tutapata barabara ambazo hazina viwango.

Mhe. Spika, vile vile tatizo jengine ambalo limejitokeza ni kwamba Serikali yenyewe inaanzisha miradi mingi lakini kile kinachopatikana ni kidogo. Kwa hivyo tufanye juhudi za makusudi ili pale tunapotia mikataba na hawa wakandarasi basi tuwe na pesa ili tusicheleweshe na kwa sababu hii kuchelewa chelewa pia inaipa hasara Serikali.

Mhe. Spika, baada ya hayo niseme naokoa muda wako naunga mkono bajeti hii mia kwa mia ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kadiri ya hali ilivyo inaonekana kuna wajumbe wapatao kumi hawatapata nafasi ya kuchangia nategemea watakaopata nafasi ni pamoja na Mhe. Salmin Awadh Salmin, Mhe. Asha Bakari Makame, Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi, Mhe. Kazija Khamis Kona, Mhe. Abdalla Mohammed Ali, Mhe. Machano Othman Said, Mhe. Salim Abdalla Hamad, wengine watakaopata kesho ni pamoja na Mhe. Waziri wa Fedha, na Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano, kwa hivyo wale ambao sikuwataja nasikitika sana kwamba ni vigumu kupata na Mhe. Mahamoud Mohammed Mussa atapata nafasi. Nasikitika sana wale ambao sikuwataja kwa kweli muda uko finyu sana na ningeomba radhi watumie nafasi ya kutoa maelezo yao na michango yao kwa maandishi haya, nashukuru.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rashid Seif Suleiman; Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano na Muwakilishi wa Jimbo la Ziwani.

Mhe. Spika, mimi sina maneno mengi katika bajeti hii kwa sababu bajeti hii nilipoipitia na nikaiona haina tofauti na ile ya mwaka jana, kwa hivyo bajeti hii nimeshaichangia tokea mwaka jana kwa hivyo leo nitachangia tu baadhi ya maeneo.

Mimi kwanza nije katika shirika la Bandari la Zanzibar kwanza nimpongeze Mkurugenzi wa Shirika la bandari kwa kazi nzuri anayoifanya ya kushughulikia masuala ya bandari, lakini pia kuwashughulikia wafanyakazi wake wa bandari.

Mhe. Spika, baadhi ya wananchi ambao tunawaongoza katika maeneo yetu huwa wanatupa tupa mambo wakati mwengine, sasa hawa miongoni mwa wananchi waliomo jimboni mwangu ni wafanyakazi wa Shirika la bandari na wamenambia bwana tunamshukuru sana Mkurugenzi wetu anafanya kazi vizuri na zaidi kwa kuongeza maslahi yao, jambo ambalo mashirika mengine wanashindwa kufanya hivyo wanajivutia wao wenzao wanawasahau. Sasa huyu wa bandari yeye amewajali sana wafanyakazi wake mpaka kufika pahala kusema wanamshukuru kwa kuongeza maslahi jambo ambalo mara nyingi tunasema kwamba mashirika haya ambayo yanajitegemeya, pale ambapo wanakuwa na uwezo wa kuwaboreshea wafanyakazi wao hayo maslahi yao basi wafanye hivyo. Kwa hivyo tunampongeza na tunamshukuru kwa kuweza kuboresha maslahi ya wafanyakazi wa shirika la bandari na sasa kidogo hali zao zimekuwa nzuri, jambo ambalo zamani tulifikiri halitowezekana kumbe linawezekana kabisa.

Mhe. Spika, nije katika Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara UUB; Idara hii ina majukumu makubwa sana ya kutengeneza barabara zetu zile nyengine mpya tunazowapa na kuzifanyia matengenezo zile za zamani ambazo kila

wakati zinakuwa zinaharibika na zinafanya mashimo na mambo mengine mengine, wamekuwa wakijitahidi pamoja na malalamiko ya hapa na pale hayaachi. Kwa sababu kila mmoja anataka eneo lake liwe zuri na huo ndio wajibu wetu.

Sisi wajibu wetu kuangalia maslahi ya wananchi kila mmoja anataka mambo mazuri katika maeneo yake na huo ndio wajibu wetu. Lakini kwa kweli wanafanya kazi, wanajitahidi lakini wana tatizo moja Mhe. Spika, hili Serikali bado haijalitafutia ufumbuzi. Tatizo la vifaa katika taasisi hii mwaka jana nilizungumzia juu ya jambo hili kwamba Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara vifaa vyake vimechakaa ni vya muda mrefu, magari yamekuwa mabovu, zana zake nzito pia zimekuwa mbovu na matengenezo yake yanakuwa na gharama kubwa.

Vifaa hivi kwa kweli Mhe. Spika, vimechakaa na kwa kweli kunahitaji mkakati wa kisawa sawa kuona tunawapatia vifaa vya kutengenezea barabara vile vipya ambavyo wanaweza kufanya kazi za uhakika, wapate zana mpya, wapate magari ya kutosha hapo sasa nadhani itakuwa tunapata wakati mzuri wa kuwalaumu pale ambapo hawatoweza kutimiza wajibu wao.

Mhe. Spika, tumekuwa tukisikia malalamiko mengi sana juu ya wenzetu hawa lakini kwa kweli wana matatizo makubwa; matatizo kama haya yalikuwepo shirika la bandari wakati fulani huko nyuma ucherewesha ji wa makontena, kufunguliwa tulikuwa tukilalamika, mpaka pale Serikali kwa makusudi ikachukua dhima ya kutafuta vifaa kama *crane* na mambo mengine; jambo ambalo limewasaidia sasa yale malalamiko katika bandari yamekuwa hayapo. Kontena zinatolewa kwa wakati.

Sasa na hapa kwenye idara hii kama Serikali haitofanya mkakati wa makusudi ikafumba macho na kutafuta zana zile ambazo ni mpya sio kama hizi zilizochakaa chakaa za muda mrefu, basi lawama zitakuwa nyingi na malalamiko yatakuwa mengi, kwa sababu kila unapokwenda unaambiwa *bulldozer* mbovu, imeharibika, iko kwenye matengenezo. Magari mabovu yamechakaa kwa hivyo mimi niiombe sana Serikali kwa kweli iweze kupitia Wizara ya Fedha, Waziri hayupo lakini wafanye mkakati wa makusudi kuona wanapatiwa vifaa vile vya kisasa vya kufanyia kazi, ili haya matatizo tuliyokuwa nayo ya barabara yaweze kutatuka.

Mhe. Spika, eneo jengine ni eneo la miradi ya ujenzi wa barabara kwa kweli eneo hili nalo linaonekana lina matatizo, miradi hii mingi inakuwa inazungumzwa humu kila bajeti inayokuja inatajwa miradi ya barabara na ndio maana waheshimiwa wajumbe wamekuwa wakilalamika. Kila siku stori hiyo hiyo mradi wa Ole/Kengeja, mradi wa Muyuni/Matemwe mradi wa wapi na wapi lakini hakuna linaloonekana na linalomalizika, kwa hivyo tumekuwa na mashaka juu ya utekelezaji wa miradi hii.

Sasa Mhe. Waziri hebu aje atueleze ni mradi gani hasa alioweza kuutekeleza katika miradi hii, kwa sababu kila siku ni hadithi za miradi lakini hatuoni mwisho, kwa hivyo tumekuwa na mashaka juu ya utendaji hasa katika haya Makampuni pengine kuna matatizo ya ufungaji wa mikataba kwa sababu inasikitisha kuona kwamba kila siku tunazungumzia miradi hii. Kila siku miradi hii lakini hatuoni utekelezaji wa hatua ya mwisho juu ya miradi hii.

Mhe. Spika, kwa mfano mradi wa ujenzi wa barabara ya Matwemwe/Muyuni na ule wa Barabara ya Mkwajuni/Kijini ambayo ni barabara ya muda mrefu sana; wananchi wa kule wamekuwa wakilalamika sana juu ya barabara hii, lakini kila ukicha unaambiwa sijui mradi wa *ADB* sijui mradi wa *World Bank* kila siku imekuwa stori hiyo kwa hiyo.

Sasa Mhe. Waziri hebu uje utueleze kwa sababu bado kila siku ukisoma kwenye kitabu unaambiwa bado tuko kwenye *feasibility study* tunaita upembuzi, mpaka Waheshimiwa wajumbe wengine wanauliza huu upembuzi yakanifu ndio nini, kwa sababu kila ukicha mradi unaambiwa uko mwaka jana, mwaka juzi ulikuwa upo kwenye upembuzi yakinifu, mwaka jana uko kwenye upembuzi yakinifu, mwaka huu upo kwenye upembuzi yakinifu, sasa tunashindwa kufahamu huu upembuzi yakinifu inaonekana ni kichaka cha kujifichia utekelezaji hakuna lakini unaambiwa uko kwenye upembuzi yakinifu.

Sasa huu upembuzi yakinifu mpaka lini Mhe. Spika, wananchi wanalalamika barabara mbovu, barabara hii hata kwenye ilani ya Chama cha Mapinduzi mwaka jana waliahidiwa wananchi wa Kijini kwamba barabara yao itatengenezwa, lakini kila siku upembuzi yakinifu mkopo kutoka *ADB*, hebu tuelezeni kuna tatizo gani.

Mimi wakati mwengine Mhe. Spika, nimekuwa na mashaka juu ya utaalam kwa sababu hii miradi kukwama pengine hatuna wataalam, wakati mwengine unasema wataalam wapo, au tatizo lipo kwenye utekelezaji katika uwajibikaji. Sasa tumekuwa na mashaka juu ya mambo haya ambayo kila siku tunakwenda nayo hayamaliziki. Barabara hii tokea wakati Dr. Shein anaizungumza na kabla ya Dr. Shein hata wakati wa Dr. Karume alikuwa anaizungumzia barabara ya Kijini/ Matemwe lakini kuna nini barabara hii haitengenezwi? Kila Rais anayekuja anaizugumzia barabara hii na utapata majibu kwamba kuna mradi, kuna mradi, kuna mradi huu *ADB*, kuna mradi sijui wa nini. Wananchi wa kule wamekuwa wakilalamika hawajaona barabara hata siku moja.

Kwa hivyo tunasema Mhe. Waziri mambo haya ya kufanya ubabaishaji kwa wananchi hayafai. Tunapozunguzia kitu na utekelezaji kionekane, wananchi waone tunatekeleza kitu gani kuliko kupata maneno, kila wakati maneno. Kwa hivyo barabara ya mradi wa Matemwe/Muyuni tunahitaji ifanyiwe matengenezo, mwakani tukijaaliwa hatutaki tena *story* hii tunasema kabisa hakuna msalie mtume. Mwakani tukijaaliwa hatutaki hadithi juu ya barabara hii ya Matemwe/ Muyuni, tunataka utekelezaji wake.

Mhe. Spika, eneo jengine ambalo nataka kuzungumzia juu ya fidia kwa watu walioathirika na upanuzi wa viwanja vya ndege. Bado kuna malalamiko ya wananchi juu ya fidia ya wananchi ama wavunjiwa au wametakiwa waondoke katika upanuzi wa viwanja vya ndege. Nataka Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho, kwanza atupe orodha ya wale watu ambao hawajapewa fidia katika upanuzi wa viwanja vya ndege na atueleze kwa nini mpaka leo hawajapewa pesa zao. Hilo tunalihitaji kwa sababu wananchi bado wanalalamika. Wengine mmewapa nusu nyengine mumezibakisha mpaka leo kwa nini? Muda umekuwa mkubwa, uje utueleze ni wananchi wangapi tena na majina yao ni kiasi gani wananchodai na kwa nini hawajapewa pesa zao mpaka leo.

Eneo jengine Mhe. Spika, juu ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege. Kumekuwa na malalamiko mengi juu ya uwanja wa ndege na namna ya huduma zinavyotolewa katika viwanja vya ndege. Mkurugenzi anajitahidi kuufanyia matengenezo na utahisi pamekuwa na mabadiliko, mabadiliko yapo lakini tatizo la Mkurugenzi wa Uwanja wa Ndege ni kutokuheshimu viongozi sasa hii ni kasoro moja kubwa sana ya kiutawala. Huwezi kuendesha taasisi kama ile ambayo inahudumia watu ikiwa wananchi pamoja na viongozi ukawa wewe hujali viongozi wewe unaona labda pale mkubwa ni Rais peke yake. Lakini Rais hayuko peke yake kiongozi katika nchi hii, Rais ana wasaidizi wake.

Sasa unapofika pahala kama huwaheshimu wale wasaidizi wa Rais hili ni tatizo, lazima ajirekebishe. Mkurugenzi lazima ajirekebishe na hii inatupa mashaka kwamba hata wale wafanyakazi wake anawaambia hakuna mtu mwengine hapa, hakuna Mwakilishi, hakuna, Waziri, kwa sababu hata wale wafanyakazi wa chini zile *treatments* zao hazijali viongozi. Hata ukimwambia mimi fulani anakwambia sisi hapa ni moja, huwezi kuongoza taasisi hii kama hivi kwa kuona kwamba labda kiongozi ni fulani mwengine humjali, hatuwezi kwenda kwenye utaratibu huo. Nchi lazima iwe na viongozi na viongozi lazima waheshimiwe katika nchi hii. Haiwezekani nchi isiwe na heshima ya viongozi. Kwa hivyo wafanyakazi wake inaonekana na wao anawa-*treat* katika utaratibu huo mpaka inafika pahala gari ya Mhe.Waziri inakwenda inafungwa, wawakilishi wana malalamiko mengi. Analoambiwa juu ya viongozi hakubali imekuwa kama ule uwanja wa ndege ni wa kwake, haiwezekani ni hata siku moja.

Kwa hivyo Mhe. Waziri mrekebishe Mkurugenzi wako juu ya utovu wa nidhamu kwa viongozi. Sisi hatuwezi kukubali, sisi ni watu tuliochaguliwa na wananchi, tunaheshimika tunatakiwa tuheshimiwe na hakuna nchi iliyokuwa haina viongozi. Viongozi lazima waheshimiwe. Tunaheshimiwa Bara tunapokwenda na nchi nyengine itakuwa katika ardhi yetu katika nchi yetu. Kwa hivyo Mhe. Waziri ninakwambia mwambie Mkurugenzi wako ajirekebishe awe na nidhamu, awe na adabu juu ya viongozi, ajue nani mkubwa nani mdogo pamoja na kupewa dhamana katika uwanja isimfanye kukosa adabu kwa viongozi wake.

Jengine Mhe. Spika, kuhusu ongezeko la abiria katika meli ya *Sealink* ambayo imezungumzwa hapa ambapo kwa kweli tulikuwa hatuna taarifa. Mimi mwenyewe nilikuwa sina taarifa. Baada ya kusikia maswali na majibu juzi ambayo yalikuwa yakijibiwa kwamba meli imeongezwa idadi ya watu kutoka 700 mpaka 1500. Kwa kweli mimi nimeshtushwa sana Mhe. Spika, na nimeshtushwa kutokana na kumbukumbu za ajali zilizotokea nyuma. Hivi Mhe. Waziri unatwambia ndio umeshasahau mara ile mpaka unaruhusu na unatetea kitu kama kile? Mimi sikutegemea kama Mhe. Rashid alipokuwa akijibu maswali jana angetetea tatizo lile la kuongezwa abiria wa meli mara mbili ya wale waliokuwepo.

Hivi kweli inaingia akilini au inajengeka hoja kwa mtu wa kawaida chombo kimetengenezwa kwao kwa abiria 700 unaongeza hadi 1500, inaingia akilini? Hivi kuna hoja ya kulijibu Baraza hili juu ya uovu huu na matendo

yaliyofanyika juzi. Meli zimezama hapa watu wamekufa wamepoteza maisha wengi, leo unakwenda kuongeza idadi ya abiria katika meli lengo lenu ni kitu gani, tamaa gani hii hebu tuache tamaa jamani katika kuongoza maisha ya watu. Roho ya binaadamu si kitu cha mchezo. Zanzibar hapa tulikuwa katika huzuni kubwa sana dunia nzima, halafu juzi tu watu wanafariki wanauwawa maelfu kwa maelfu unakwenda kuongeza meli *capacity* kuliko vile ilivyo mara mbili.

Mhe. Spika, katika hili halina majibu, halina utaalamu, halina mbadala wala mjadala wala halina hoja juu ya suala hili. Kama meli imetengenezwa kwao inabeba abiria 700 umewaongeza mpaka 1500 hakuna maneno, abiria wale Mhe. Waziri uwafute uirejeshe meli ile katika hali ya kawaida. Wanaoumia ni ndugu zako, wanaokufa ni ndugu zetu, wanapoteza maisha kwa tamaa zetu. Hatuwezi kufanya tamaa kwa sababu ya kuwauwa watu. Meli imetengenezwa kwa abiria 700 huwezi kuongeza watu mpaka kufika 1500, wale sio mbuzi, wala si mizigo, zile ni roho za binaadamu.

Juzi juzi tumeshuhudiza hapa meli zinazama. Hivi meli kama ile ikienda ikapata taharaki kule ikizama utakuja kuliambia nini Baraza hili? Mhe. Waziri hatukubaliani na hoja ya aina yoyote. Hatukubaliani na jibu la aina yoyote, lolote hatukubaliani nalo hilo tunakwambia. Meli imewekwa na *capacity* abiria 700, uwarejeshe. Hatutaki kuwa wauwaji, hamuwezi kuwaua watu hivi hivi kama kuku, kama mbuzi kwa tamaa zenu; hilo ninakwambia Mhe. Waziri.

La mwisho Mhe. Spika, namalizia kuna babara za *feeder roads*, iliyoko katika Jimbo la Magomeni nimuombe sana Mhe. Waziri. *Feeder road* iliyopo Magomeni ambayo inatoka katika barabara kuu ya Magomeni inakwenda katika barabara ya Amani. Hii ni *feeder road* lakini ni barabara kubwa, ni njia kubwa ambayo huwezi kupita usipishane na magari mengine na sasa hivi hali yake ni mbaya sana. Nimejaribu kumuomba Mkurugenzi wa Mfuko wa Barabara kwamba barabara ile au *feeder road* ile itengenezwe tokea mwaka jana akanambia bajeti zile *proposals* za Idara ya Njia tayari zimeshapelekwa kwa hivyo tusubiri katika mwaka huu wa fedha. Na mwaka huu wa fedha ndio tayari umeshafika.

Kwa hivyo ninamuomba Mkurugenzi wa barabara kupitia kwa Waziri, katika barabara za ndani ambazo zitatengenezwa *feeder road* hii nayo iwekwe katika mpango utakaotengenezwa kupitia fedha za UUB. Kwa sababu ni njia kubwa inatumika na sasa hivi katika mvua za juzi imeharibika sana, haiwezi kupitika. Nimeona humu kwenye mipango mnatengeneza barabara za *feeder road* nyingi tu Mikoani, wapi, kwa hivyo na hii kutokana na ombi langu ambalo nililipitisha tokea mwaka jana iingizwe katika mpango wa barabara za *feeder roads* ambazo zitasaidiwa na mfuko wa barabara, yaani zile za UUB, hilo ndio ombi langu Mhe. Spika.

Baada ya maelezo hayo niliyoyatoa nadhani Mhe. Waziri atatoa maelezo ya kutosha yatakayowezesha kuweza kuipitisha bajeti hii, mimi sina tatizo na bajeti ikiwa Mhe. Waziri atatoa maelezo mazuri na zaidi katika eneo la uongezaji wa abiria katika meli, atoe maelezo ya kuwatoa watu aliowaingiza katika meli. Sina tatizo tutaipitisha bajeti hii ili aweze kwenda kuendelea na shughuli zake.

Mhe. Spika, ninakushukuru. Ahsante sana. *(Makofi).*

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi jioni hii kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri. Pia Mhe. Spika, nimpongeze Mhe. Waziri kwa kutuwasilishia hotuba yake katika Baraza lako hili tukufu na kusaidiwa na watendaji wake wote, ninawapongeza Mhe. Spika.

Mhe. Spika, mimi nitakuja katika ukurasa 26 na nitaanzia na barabara yangu Mkanyageni/Kangani. Mhe. Spika, waswahili husema, kila muamba ngoma huwa anavutia kwake. Na mimi Mhe. Spika, naanza kuvutia kwanza kwenye barabara yangu hii ya Mkanyageni/Kangani. Mhe. Spika, barabara hii imekuwa ni kilio kikubwa sana cha wananchi wetu na mimi mwenyewe.

Mhe. Spika, suala hili limekuwa mno kwa kuanzia mwaka 2005 niko Baraza kongwe mpaka hii leo barabara hii iko mdomoni kutengenezwa na mpaka hii leo Mhe. Spika, bado barabara hii inashindwa kutengenezwa.

Mhe. Spika, nije katika kitabu cha 2012/2013 kinachosema kwamba mradi huu umepangwa kutekelezwa mwaka wa fedha 2012/2013 baada ya kukamilika kwa barabara ya Mgagadu/Kiwani na unagharimiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, mradi una lengo la kujenga barabara inayoanzia Mkanyageni/Kangani yenye urefu wa

kilomita 6.5. Lakini vile vile wakasema kwa mwaka wa fedha 2012/2013 jumla ya shilingi 100,000,000 zimeombwa kutoka serikalini kutengenezewa barabara hii.

Sasa niseme Mhe. Waziri hii barabara iliombewa shilingi 100,000,000 pesa hizi hazikupatikana kutengenea barabara hii au pesa hizi zimekwenda wapi. Lakini vile vile mwaka 2005 pesa hizi ziliombewa shilingi 50,000,000 kutengenezewa barabara. Pia barabara hii Mhe. Spika, haikutengenezwa, nimuulize Mhe. Waziri fedha zile zilifanywa nini?

Vile vile Mhe. Spika, nikija katika kitabu cha 2013/2014 kinachosema mradi huu una lengo la kujenga barabara inayoanzia Mkanyageni hadi Kangani. Hapa Mhe. Spika, shilingi 50,000,000 ambazo ziliombwa vile vile nimuulize Mhe. Waziri fedha hizi hazikuwahi kupatikana au fedha hizi zilikwenda wapi mpaka kufika hadi barabara hii hadi hii leo bado haijatengenezwa.

Mhe. Spika, pia nije katika ukurasa wa 55 kifungu cha 4 unaosema ujenzi wa barabara ya Mkanyageni Kangani ambao una urefu wa 6.5 na mfadhili SMZ. Lakini nikija kwenye bajeti nakutia 0 na nikija kwenye ruzuku ya mkopo nakutia 0. Jee, ninajiuliza Mhe. Spika, barabara hii kweli ina nia ya kujengwa wakati ya kuwa huku kuna ziro na huku inaambiwa barabara hiyo itajengwa. Vile vile niseme kuna barabara ya Mjimbini/Tondooni na vilevile kuna barabara Mtadoda hizi zote ni barabara ambazo Mhe. Spika, kwa kweli sasa hivi hazipitiki. Lakini nikisema zaidi barabara hii ambapo imo kwenye bajeti ya Mkanyageni/Kangani Mhe. Spika, kwa kweli ni tatizo.

Kwa sababu mvua zinaponyesha yule mtu akishakuwepo pale Kangani kuelekea huko alikokusudia anajitwika mizigo kichwani hakwendeki. Mhe. Waziri nimeshamuomba kwa sana alau kifusi, nishachoka. Mimi mwenyewe kifusi mara ngapi nimeshatia. Lakini kwa kweli Mwakilishi hawezi kujenga barabara, kwa hivyo Mhe. Waziri alau nilimuomba kifusi anisaidie lakini hadi hii leo kashindwa alau kile kifusi. Ninamuuliza Mhe.Waziri barabara hii itamalizika lini.

Pia nije katika barabara ya Ole ambayo Mhe. Naibu Waziri asubuhi nilimuuliza swali langu na akanijibu sikuridhika kwa kweli, lakini nikasema wakati ya kuwa hii leo Wizara ipo nitabidi nilichangie kidogo. Mhe. Waziri nilimuuliza kwamba hii barabara itaanza lini na siku zote barabara hii iko katika bajeti, lakini akanambia kwa kweli barabara haiko kwenye bajeti isipokuwa bajeti ni mara hii. Lakini nilimuuliza Mhe. Waziri wategemea hii barabara itamalizika kwa ilivyopangiwa na ikiwa haikumalizika Mhe. Waziri atakuja kutwambia nini? Kwa sababu barabara nyingi huwa zimo katika mpango lakini inapofika mwaka mwengine inakuwa barabara ile haikutengenezwa. Sasa ninamuuliza na hii anaahidi kwamba barabara hii itamalizika na ikiwa haikumalizika ataliambia nini Baraza lako hili.

Mhe. Spika, nije katika kiwanja cha ndege Unguja, mara nyingi suala la viwanja vya ndege Unguja huwa ninalichangia sana inapotokea bajeti na huwa ninalipigia kelele sana kuhusu kiwanja cha ndege Unguja.

Mhe. Spika, kuhusu usafiri pale watu wanaposafiri hupita pale na wakapekuliwa lile ni tatizo kubwa sana na kitendo cha aibu kikubwa sana kuwa mtu mzima na akili yake anapita pale anaanza kupapaswa kichwa mpaka maziwa, mpaka chini, mpaka miguuni; hili ni tatizo kubwa sana Mhe. Spika. Na huu si utaratibu kabisa wala mtu yule hatambuliwi kama anawekwa kwenye alau kibanda angalau sehemu ya kujificha, inakuwa pia hajifichi anapekuliwa pale pale.

Mhe. Spika, hili ni tatizo kubwa sana na hiki ni kitendo cha aibu kwa sababu wanaotupekuwa ni watoto wadogo ambao tunawazaa anampapasa mtu mama yake au baba yake anamuanzia kichwani mpaka miguuni, hili ni tatizo Mhe. Spika, kwa kweli ninamuomba Mhe. Waziri aliangalie sana tatizo hili. Ule upekuzi wa pale angalau pajengwe kibanda cha kujifichia mtu anapopekuliwa. Mhe. Spika, kwa kweli utaratibu kama huu umepitwa na wakati tutafute vitu ambavyo vinaweza kumpekua mtu akaweza kujulikana kwamba ana kitu cha kupekuliwa. Lakini sio kupapaswa Mhe. Spika. Hili ni tatizo tafuteni mashine za kuangalia na ndio mara nyingi tunasema Mhe. Spika, madawa ya kulevya yanapita pale kutokana na kuwa hapana mashine ya kupekulia. Leo mtu ana kitu tumboni utampapasa utakijua kama kimo, ninamuomba Mhe. Waziri aliangalie suala hili sana kuhusu upekuzi uliopo pale.

Mhe. Spika, sasa nije kwenye kiwanja cha Pemba; kuhusu suala la Kiwanja cha Pemba hii sijui ni bajeti ya ngapi ambayo pia huchangia kuhusu suala la Kiwanja hiki cha Pemba ambacho kimeahidiwa kitawekwa taa. Hebu nimuulize Mhe. Waziri taa hizi ni taa za aina gani, ambazo zitaweza kuwekwa katika kiwanja cha ndege. Hadi hii

leo taa hizo zinawekwa wala hazikamiliki. Ninamuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa katika majumuisho yake atueleze hizi taa zitawekwa lini.

Mhe. Spika, nije katika sekta ya usafiri wa anga, mimi nataka kujua tu kuhusu hizi ndege zetu ambazo zina rubani mmoja mmoja, je, Mhe. Waziri mna uhakika gani wa usalama wa wananchi katika ndege hizi. Lakini pia Mhe. Spika, nimuulize Mhe. Waziri hizi ndege kwa mwaka huwa zinakaguliwa mara ngapi?

Mhe. Spika, nije katika Idara ya Usafiri wa Nchi kavu. Idara hii ya usafiri wa nchi kavu ina jukumu kubwa sana la usafiri. Hii inakuwa ni vyombo vya moto, sana huwa ndio vinavyosafiri lakini ningeomba sana kuliangalia suala la magari na kutafutia *stand* ya kuwekwa magari. Hili limekuwa ni tatizo kubwa Mhe. Spika. Watu wetu wanadhalilika, watu wetu wanahamanika na tukiwaangalia hawa ni wananchi wetu ambao wanategemea serikali yao; hawana ajira, ajira zao wametegemea kuendelesha magari yao ili wapate ajira na kula na watoto wao.

Leo Mhe. Spika, watoto hawa wamegeuka paka; paka anapozaa mpaka atimize vifungu 7 ndio aweze kuchukua mtoto wake kumtoa nje. Sasa na hawa leo wanawekwa hapa, leo wanawekwa pale na kesho kutwa hapa, hii ni idhilali Mhe. Spika, kwa kweli watu wetu wanateseka sana. Ninamuomba Mhe. Waziri hili aliangalie sana kuhusu watu wetu na vyombo hivi vya moto.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Spika, kwanza na mimi nichukue nafasi hii nikushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi hii kwa kujadili wizara ambayo ni muhimu sana katika mataifa yote, maana mawasiliano na miundombinu ni wizara muhimu.

Mhe. Spika, kwanza nitatoa pongezi maana nisigeuke kinyonga, kwani kila kizuri hakikosi ila. Kwanza nichukue nafasi hii niipongeze sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa jinsi ilivyojitahidi katika kujenga njia. Mimi niseme Mhe. Spika pamoja na yote lakini serikali imejitahidi sana kupitisha njia sehemu mbali mbali.

Pia nitoe pongezi maalum kwa njia ya Mtambwe, niishukuru sana serikali kwa njia ya Mtambwe kwa kweli *Alhamdulillah* maana sasa hivi Mtambwe hatuna shida ya maji, hatuna shida ya umeme, hatuna shida ya barabara. Hivyo niishukuru sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa vifaa hivyo kutufikia.

Mhe. Spika, lakini mimi kidogo naomba wenzangu watanisamehe, mimi nasema nimpongeze sana mfanyabiashara Bakhresa. Kwa kweli Mhe. Spika, tusisahau hisani wala fadhila. Ndugu Bakhressa ni mtu pekee ambae analeta vipando vya baharini, na ametusaidia sana hasa sisi kisiwa cha pili, lazima hilo nilizungumze wazi. Mimi simtii makosani kwa hii meli ya *Sea Link*. Makosa wanayo wizara tusimtie mtu makosa ambayo hanayo, yeye ni mfanyabiashara na kapewa maelekezo maana tumevunja sheria sisi wenyewe Wizara ya Mawasiliano, Mheshimiwa.

Kwa hivyo, namuomba ndugu Bakhressa asiwe na wasi wasi lazima haki yake tumpe, kwa kweli anatusaidia sana. Mhe. Spika, ameiweka bandari yetu utafikiri sijui kitu gani, maana yake bandari imepoa na bado anawajibika kuitengeneza bandari. Kwa hiyo, nimuombe ndugu Bakhresa kupitia chombo hiki, kwamba kule Wete ile bandari yake atuonee huruma. Mhe. Spika, enzi za kale bandari ya Wete ndiyo iliyokuwa bandari kuu kwa Pemba, kwa hiyo namuomba atuonee huruma atutengenezee kidogo angalau na wale wafanyabiashara na wao waweze kufanya mambo hayo kupitia chombo hiki.

Vile vile Mhe. Spika, sasa nije katika uchangiaji wangu, niunge mkono kwa yale wenzangu ambayo wamezungumza kuhusu habari ya kusachiwa. Kwa kweli ni aibu hasa sisi akina mama, akina mama tunafanyiwa mambo ambayo si mazuri. Hilo niunge mkono tu.

Jambo jengine niseme kuhusu nidhamu ya *Airport*, *Airport* ya Unguja; nidhamu yake ni ndogo waheshimiwa. Mimi ni juzi tu nilisafiri nikapita pale nikaingia wakaniambia mama nipe tiket, nikamwambia tiketi imetiwa kwenye simu, lete nione, nikamwambia huniamini? Sikuamini nakwambia lete nione kama hukuleta husafiri hapa. Nikamwambia *wallahi* nitasafiri mimi hapa, mimi hapa nitasafiri sasa tutashindana mimi na wewe, kusafiri au kutosafiri. Maana nasema ule ukweli maana saa nyengine wanatufanya mpaka sisi viongozi tunakuwa tunajibu vyengine na mimi si mtu wa kuchukua madaraka mikononi mwangu Mhe. Spika, maisha yangu yote, lakini mtu akinifanyia upuuzi na mimi namfanyia upuuzi. Nikamwambia mimi nitasafiri hapa, husafiri akawaambia wenzake hana ruhusa ya kusafiri huyo, nikamwambia nataka mtu aniguse, lakini nitasafiri. Wale vijana wengine wananijua vizuri tena wakamwambia huyo ni mheshimiwa, sina mheshimiwa, uheshimiwa wake huko huko.

Heshima hakuna Mheshimiwa niunge mkono maneno aliyoyazungumza Mhe. Salmin Awadh. Kwa hivyo, sisi pamoja na yote lakini heshima ni kitu cha bure kwa bahati wale vijana wengine wakaniambia mama Asha lete mizigo yako, nikapeleka mizigo yangu ikapekuriwa ikesha mimi nikasafiri. Sasa na mimi nayazungumza hapa makusudi, hilo moja.

Mhe. Spika, jengine mimi sijui niseme wizara hii ina ulemavu gani, wizara hii sijui ina nini kila waziri anayewekwa akifika pale anabezwa bezwa, anabembelezwa mambo hayawi, maana nasema kweli mimi Mhe. Spika. Jamani kulikoni hii wizara mawaziri mna nini, ewe Mwenyezi Mungu tusaidie hii wizara ipate waziri mwenye kujua namna ya kuendesha hii wizara. Wizara hii kila anayewekwa pale akishakukaa siku mbili ya tatu anajiona yeye ndiyo basi.

Tatizo Mhe. Spika, hatuwajibiki ipasavyo waziri unatakiwa utembee katika sehemu zako mbali mbali siyo ukae ofisini tu, na wewe uangalie mambo utembee na utizame. Mimi namsifu sana Mhe. Haji Omar Kheir, mtu lake mpeni. Mhe. Haji Omar Kheir si wizara hii aliyopewa tu, wizara zote mtu hamdanganyi na ndiyo inavyotakiwa. Kwa hivyo, nawaomba mawaziri mupitie baadhi wengine wanapitia lakini waliokuwa hawapitii wapitie sehemu zao za kazi ili wanapokuja hapa tukiwaeleza watupe maelezo sahihi. Mhe. Spika, nasema hapa patachimbika, patachimbika kwa *Airport* ya Pemba.

Mhe. Spika, kila bajeti, kila suala likiulizwa mimi na *Airport* ya Pemba, lakini la kunisikitisha Mhe. Waziri sasa hivi hayupo, lakunisikitisha ni hivi karibuni tuliliuliza suala hili na Mhe. Waziri akatwambia usiwe na wasi wasi Mhe. Asha mambo yote tayari, taa zitatiwa hata wiki haitimii zitakuwa tayari. Matokeo yake mpaka leo. Sasa mimi pamoja na maelezo mazuri ya Mhe. Waziri wa Fedha kwa sababu waziri muhusika katudanganya hapatoshi kesho hapa; hapatoshi mpaka anihakikishie au serikali kuu ichukue dhamana kwa sababu wenzangu wamechangia inaweza ikatokea *emergence* yoyote jamani Pemba hakuna taa basi bora tubandike ile mishumaa ya *birthday* ile mikubwa au tuiache mienge ile ya kuingia mashimoni tuiweke pale. Lakini kwa kweli jamani *Airport* ya Pemba hairidhishi Mheshimiwa.

Jengine Mhe. Spika, na mimi niseme barabara ya Kijini kwa kweli barabara ya Kijini Mheshimiwa mimi toka niko Mkoa wa Kaskazini “A” nilikuwa Katibu Msaidizi Mkuu wa Chama cha Mapinduzi barabara hii wananchi wanailalamikia tokea mwaka 1985 nilipokwenda mimi. Barabara hii wananchi wanailalamikia na ukiangalia kwa kweli wanawake ndiyo wanaopata shida maana wengine wanajifungulia njiani . Mheshimiwa namuomba sana Mhe. Waziri tena sana Mhe. Naibu Waziri uyachukue haya barabara ya Kijini kwa kweli iko hali mbaya sana, na kule nako kuna wananchi jamani hebu tuwaoneeni huruma.

Sasa Mhe. Spika, namwambia Mhe. Waziri ameshaingia sasa hivi patachimbika hapa kuhusu habari ya *Airport* ya Pemba.

Mhe. Spika, kwa sababu watu wamezungumza mengi lakini nizungumze suala moja, namuomba sana Mhe. Waziri atakapokuja hapa aje anipe kuna fedha za kigeni pale *Airport* zinazokusanywa na *Shipping Cooperation* kupitia kitengo chake cha uwakala. Kwa hivyo, nataka aje anieleze kila mwaka wanapata kiasi gani? Umenisikia Mhe. Waziri kila mwaka mnapata kiasi gani naomba hili uje unieleze Mhe. Waziri, maana hapa nina hakika nyengine zinaingia mifukoni. Kwa hivyo, suala hili nataka nije nielezwe.

Mhe. Spika, mimi nasema Uwanja wa Ndege Zanzibar, Mheshimiwa wenzangu wameulalamikia sana na mimi itabidi lazima niulalamikie kwa sababu Uwanja wa Ndege ule ni muhimu kwetu maana yake Uwanja wa Ndege wa Zanzibar uko hali ile huo wa Pemba ndiyo hausemeki, wala ndege hazitoweza kutua Pemba. Lakini niseme tu kwamba niiombe Serikali na Mhe. Waziri wa Fedha ule uwanja muna kazi kubwa sana, mna kazi kubwa sana mpaka uwanja ule ukaweza kukaa vizuri kama *Airport* ya kimataifa.

Kwa hiyo, nikuombe na niiombe serikali iache kila ilichonacho sasa hivi ule Uwanja wa Ndege kwa kweli tuushughulikieni, ni aibu. Maana yake kwanza nasikia hayo mabasi yanayotakiwa tu pale basi moja sijui dola laki moja na ngapi sijui, mjipange vizuri ili ule uwanja umalizike maana mapato tunakosa mapato mengi sana pale. Nikuombe sana Mhe. Waziri wa Fedha.

Mhe. Spika, la mwisho niseme tu kwamba mawaziri mushirikiane namna ya utendaji kazi, kwa sababu kila wizara inamgusa waziri mwengine, na nalisema hili kwa makusudi. Kwa sababu juzi hapa tulipitisha bajeti nasikitika

kwamba husimama waziri mmoja tu, mimi siwasemi nawaambia kweli na nyinyi wenyewe mnanisikia. Angalau mawaziri musimame musaidiane kujibu zile hoja, kama Waziri wa Mawasiliano na Miundombinu hapa hapatoshi kesho basi mkimuacha hivyo kazi kwenu, na baadhi ya miundombinu na nyie mnahusika.

Kwa hivyo, kila mwenye kuhusika amsaidie, atoe ufafanuzi wake ili kuweza na yeye kusaidiwa katika haya mambo ya miundombinu, maana yake miundombinu pale pana maji, pana umeme sasa musimuachie Waziri tu Miundombinu kwa sababu ndiyo miundombinu peke yake, mumsaidie.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo lakini namuonea huruma, sipitishi hiyo bajeti, namuonea huruma kwa sababu yeye alipokuwa *backbencher* alikuwa mkali mno, sasa rungu kapewa yeye linamshinda! Kwa hivyo, mpaka nipate maelezo ya kina ndio nipitishe bajeti, si hivyo siipitishi bajeti n'go. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Kazija Khamis Kona: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuchangia bajeti hii ya Mhe. Waziri wa Miundombinu. Mhe. Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujaalia leo hii kuwa katika hali ya uzima na afya na kuendeleza majukumu yetu kama tunavyojipangia.

Mhe. Spika, pili nimpe pole Mhe. Waziri kwa kazi ngumu aliyokuwa nayo na pia nimuombee dua kwa Mwenyezi Mungu amfanyie wepesi ili atekeleze majukumu yake kama ipasavyo.

Mhe. Spika, mimi kwa kuanzia naanzia na Mradi wa Barabara zinazoingia Mjini Unguja. Mhe. Spika, mradi huu umejumuisha njia inatoka Bububu/Mahonda hadi Mkokotoni kuna siku hapa niliuliza suala nikaambiwa kwamba njia hii iko katika mshauri elekezi, tayari sijui ishalipiwa dola mia moja. Sasa Mhe. Spika, naomba hapa ufafanuzi wa hali ya juu kutokana na njia hii halafu pia kitabu chake Mhe. Waziri kinaeleza juhudi za kutafuta fedha za ujenzi wa barabara hizi zinaendelea na hadi kufikia mwezi Machi 2014, hakuna fedha iliyopatikana kutoka kwa wafadhili kwa ajili ya mradi huo. Sasa sijui Mhe. Waziri amejipanga vipi katika njia hizi na hasa katika maeneo yale yenye madaraja.

Mhe. Spika, sasa mimi nimuombe Mhe. Waziri hapa kama bado hawajampata huyo mfadhili basi tuyaangalie yale madaraja, Mheshimiwa madaraja yako hali mbaya sana, tena yanahatarisha maisha halafu sisi hapa tunajinadi uchumi wetu unatokana kwa asilimia kubwa kwenye utalii. Leo utalii unampitisha kwenye daraja kama lile anapiga picha anaenda kueneza kwao, kweli tutapata watalii wengine waje katika nchi hii, au huyo mtalii keshakuja mara ya kwanza kweli atakuja tena anaiona hatari ile, mimi nitatumbukia muda wowote.

Kwa hiyo, hapa Mhe. Waziri lazima wizara yake ifanye jitihada ya aina yoyote na ifanye mbinu ya aina yoyote ili madaraja yale yajengwe. Mhe. Spika, kama hakuna uwezo basi tutafute namna yoyote ili tuweze kuyaziba yale madaraja ili yasiwe wazi kama vile. Mhe. Spika, kila siku pale panatokea ajali Mhe. Spika.

Mhe. Spika, mimi nataka Mhe. Waziri aje aniambie ana mpango gani atakaoufanya ili madaraja yale angalau yaonekane na sura sura, ili yaweze kuridhisha kidogo kwani yako katika hali mbaya madaraja.

Mhe. Spika, na mimi niendelee na mchango wangu barabara hiyo hiyo kuna eneo lile Jimbo la Chaani barabara hiyo imechimbwa chimbwa sana na hatuoni matengenezo yake yanavyoendelea. Sasa Mhe. Waziri aje aniambie watayakamilisha matengenezo ya barabara ile.

Mhe. Spika, baada ya kuondoka hapo na mimi niende katika barabara ya Kijini kwa sababu na mimi Jimbo la Matemwe ni langu, watu wa Kijini mimi ni wananchi wangu. Kwa hiyo, na mimi natoa msisitizo zaidi Mhe. Spika kwa nini sisi kule kila maendeleo ni mafupi hasa kule Kijini, ukiangalia kituo cha afya kibovu, ukiangalia miundombinu ya maji hakuna, ukiangalia barabara haisemeki, yaani kila kitu sisi kule tumewekwa nyuma.

Sasa namuomba Mhe. Waziri atuhakikishie barabara ya Kijini inatengenezwa tena isiwe katika miradi, washauri waelekezi sijui wanashauriana nini huko kisichomaliza barabara ikapata kujengwa, tutafutieni fedha mtujengee barabara ile na wananchi wa Kijini nao wanachangia katika nchi hii, njia ikiwa mbovu watachangia nini?

Mhe. Waziri naomba na hili aje anitosheleze kwa hali ya juu. Sasa hivi njia ile imetiwa kifusi na sasa hivi ishachimbika yote, wenzangu wanasema hapa ina mashimo kwa hiyo tuyazibe mashimo yale ili wananchi nao wajisikie.

Mhe. Spika, kwa kweli wananchi wa Kijini mimi nasema itakuwa wanaonewa, kila Rais anayetaka kugombea anakwenda kule anaomba kura anaweka ahadi njia ya Kijini nikipata itatengenezwa, mbona haitengenezwi. Mhe. Waziri hapa aje anieleze vya kutosha.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo sina mchango mkubwa, nakushukuru.

Mhe. Abdalla Mohammed Ali: Mhe. Spika, na mimi nakushukuru baada ya magharibi kunipa fursa ya kuchangia wizara hii, isipokuwa tu nitakwenda haraka haraka kwa sababu Mwenyekiti wa Wenyeviti ameniomba katika dakika zangu 20 nimpatie japo dakika 10. Kwa sababu kaja na nondo na saruji na yeye apate kujenga leo. Kwa vile ni Mwenyekiti nitajitahidi nitumie dakika 10 na yeye apate dakika 10.

Mhe. Spika, labda mimi nianze na Bandari ya Mkoani. Ni muda mrefu sasa bandari ile ipo lakini maendeleo yake ni madogo sana. Ni miaka miwili tu iliyopita nyuma ilikuwa katika bandari ile pamefanya ziwa au Wazungu wanasema *lagoon* lilitengenezwa. Lakini nashukuru mwaka jana idara iliona umuhimu na ikalikarabati, kwa hiyo hivi sasa haijambo bandarini panapitika, lakini bado ile bandari ni ndefu kutoka wanakokaa abiria mpaka ukafika kwenye meli. Sasa ningeiomba wizara ikaliona hilo kwamba hivi sasa kuna umuhimu wa bandari ile kuipatia viziba jua na viziba mvua, kwani hata zile meli zinazokuja kushusha mizigo nazo wakati mwengine zinachelewa kwa muda wa masaaa matatu kusubiri mvua ipite ndio wapate kushusha mizigo yao.

Kama hilo haliwezekani basi wangefanya utaratibu kama ule wa *airport*, wakatafuta japo mabasi yakawepo pale yakachukua abiria kutoka jengo la abiria wakawafikishia melini. Hilo litakuwa ni busara sana, kwani wananchi kidogo wanateseka hasa wale ambao walio na watoto wakati wa mvua huwa wanapata shida. Kwa hiyo, ningeiomba wizara ikaona hivi sasa kwamba upo umuhimu huo na kwa vile ile bandari hivi sasa inazidi kukua kwa sababu vyombo vinavyotia nanga pale vinakuwa ni vingi sana.

Mhe. Spika, nikitoka katika suala hilo niende sasa katika hizi barabara, wengi sana wamezungumzia barabara. Mimi kidogo niseme tu kwamba nashukuru katika sehemu moja inayoitwa Wambaa, serikali imeona kwamba labda tuweke kipaumbele ya kuitengeneza ile barabara. Hivi sasa ipo kama alivyosema mwenzangu japo imesizimwa kwa mikono lakini *Alhamdulillah*, wananchi kidogo wanapata kupita. Lakini ni kwamba barabara ile mara nyingi huwa nafikiria zinakusudia zifike kwa wananchi na wananchi wafaidike na zile barabara.

Mhe. Spika, la kushangaza ni kwamba barabara hii imefika katika eneo ambalo karibu kilomita mbili haitumiki, kwa sababu lile eneo ambalo wanakaa wananchi halikufikiwa na barabara ile imepita sehemu nyengine ya pwani ambako kuna hoteli lakini Mzungu wenyewe ambae amewekeza kule alikuwa hana shida ya hii barabara. Kwa hiyo, naiomba wizara pia ione kwamba hivi sasa upo umuhimu wa sehemu ile kuifikishia barabara japo ya kifusi kidogo kidogo ili wananchi na wao wafaidi matunda, tukizingatia kwamba eneo lile linazalisha karafuu kwa wingi sana katika kisiwa chetu cha Pemba.

Mhe. Spika, sasa nije usafiri wa baharini, nilikuwa nina mawazo kwamba serikali labda sekta hii ilikuwa inataka kuiachia sekta binafsi na baada ya matukio ya kuzama kwa meli, nafikiri wameona sasa ipo haja ya serikali kujiingiza katika sekta hii. Nashukuru pengine baada ya miezi 12 labda meli inayotarajiwa kufika itakuwa imefika hapa. Labda niseme kwamba tunamshukuru sana mwekezaji ambaye amewekeza katika sekta hii na amejitahidi kiasi kwamba usafiri hivi sasa kwa kisiwa cha Zanzibar au kuondoka Unguja kwenda Dar es Salaam upo *Alhamdulillah*, kila saa au kila masaa mawili upo usafiri huo.

Kwa kisiwa cha Pemba nafikiri kwa muda wa miaka 20 iliyopita ilikuwa hakuna usumbufu kama huu, ilikuwa boti zipo lakini kwa vile yeye amefanya *monopolization* ya biashara hii imekuwa yeye ndiye anayemiliki ile bahari pale hakuna vyombo vyengine. Kwa hivyo, yeye ametuwekea lile berenge, mimi nasema ni berenge ambalo linatumia karibu masaa manane au tisa kufika kisiwani Pemba. Nafikiri upo umuhimu hivi sasa wa kuona kwamba usafiri wa haraka kisiwani Pemba na Unguja unahitajika, leo hakuna hata boti moja inayosafiri baina ya kisiwa cha Unguja na Pemba, kuna watu ambao wana matatizo wanakuwa wagonjwa wanahitajika waje hospitali katika kisiwa hiki au waelekee Dar es Salaam hawapati huduma hiyo.

Kwa hivyo, tushauriane na huyu ambaye hivi sasa amewekeza katika sekta hii basi atusaidie ili tupate usafiri wa haraka baina ya visiwa hivi viwili, kuna wengine wagonjwa, kuna wengine wendawazimu hawawezi kukaa muda

mrefu katika maberenge yale. Kwa hiyo, wanahitajika waje katika kisiwa hiki kupata huduma haraka haraka hawana uwezo wa kwenda katika *anga tour* kule *airport.* Kwa hivyo, wao wanahitaji wapitie bandarini na usafiri wao ni wa haraka. Sasa huyu mtu hivi sasa kama kule amekuweka nyuma turudie ule utaratibu wa zamani uliokuwepo miaka 20 iliyopita asiturudishe nyuma tena, zile boti ziwepo kila leo, wasafiri wapo na wanahitaji huduma hii kwa hiyo atupatie haraka.

Mhe. Spika, nije kidogo katika Shirika la Meli, wamesema hapa katika ripoti zao kwamba Shirika la Meli ndilo moja wapo linalochangia katika mapato yao na wametueleza kwamba wana meli mbili moja ya Uhuru na hii ya Ukombozi. Meli ya Ukombozi wanavyotwambia kwamba imekodishwa na *GAPCO*, lakini katika mapato yao wametuonesha tu kwamba wamefikia asilimia 79. Sasa mimi wasiwasi wangu hawa ambao hii Meli ya Ukombozi iliyokodishwa katika Shirika la *GAPCO* na wao hawakufikia lengo? Kwani wao ninachokijua kwamba wana mkataba, hata wao nao hawakufikia lengo na mkataba wao ukoje na wanatakiwa walipe vipi kwa mwaka au kwa mwezi hata kiasi kwamba yale mapato yasifikiwe.

Mhe. Spika, katika hili nimejifunza jambo moja, kwamba leo Meli ya MV. Maendeleo ilikuwa haitembei baharini inakaa karibu masaa 8 au 10, lakini hifi sasa inatembea vizuri baada ya kufanya hiyo programu waliyoiweka na nafikiri wametafuta mtaalamu bingwa. Sasa inavyoelekea kwamba shirika hili halina mtaalamu wa kiwango hicho na kesho kutwa baada ya miezi tunatarajia sisi nchi hii kupata meli.

Je, wao itakapofikia wakati huo tutakuwa tuna mtaalamu wa kuweza kuendesha meli hii? Hatutakuwa tunasuasua tena baada ya miezi miwili meli hii ambayo tunaitarajia kufika ikawa haiwezi kutembea tena kwa masafa yanayotarajiwa? Sijui wana mpango wowote wa kusomesha wataalamu wazalendo kuondokana na yule mtaalamau ambae anatoka Kenya ambae hivi sasa anaiendesha meli hii.

Jengine ni kwamba shirika hili kwa muda mrefu lilikuwa linasuasua, hapa serikali ilituletea *reform and structuring* ya Shirika la *ZSTC*. Mimi nina wasi wasi kwamba meli hii itakapofika kama tutalikabidhi shirika hili hili lililopo ambalo kwa muda wa miaka yote limeshindwa kuzalisha chochote nina wasi wasi watashindwa, sijui serikali ina mpango wowote na kama mwaka jana walitugusia kwamba wanataka kuleta *reform* ya Shirika la Meli. Je, mpango ule serikalini bado upo na utaendelea kuwepo, na tutaletewa hapa ili tuupitishe kwa ajili ya ufanisi wa shirika hili.

Mhe. Spika, nafikiri Mhe. Mwenyekiti ameniomba, kwa hiyo kwa leo naona nimalizie hapa. Nakushukuru.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Abdalla Mohammed Ali sasa nimkaribishe Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa na kutokana na maombi hayo maalum muda utakaobaki utakuwa ni wa Mhe. Hamza Hassan Juma.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, namhakikishia tu Mhe. Hamza Hassan Juma, Mwenyekiti wa Wenyeviti kwamba muda utabakia na atachangia *Inshaallah*.

Mhe. Spika, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe mwenyewe binafsi pamoja na Mhe. Waziri, Mhe. Naibu Waziri pamoa na watendaji wote kwa ujumla. Baada ya shukurani hizo mimi naomba kuzidishia tu kuchangia, kwa sababu mchago mkubwa nilikwishatoa katika maelezo ya hotuba ambayo imesomwa hapa na makamu na mambo mengi yapo na tayari wajumbe ambao walichangia walizungumzia vizuri sana na mengine wameyazidishia.

Mimi kwa upande wangu nilikuwa naongeza nguvu zaidi katika suala zima la barabara ya *Wireless*. Barabara hii ni barabara ambayo iliombwa na viongozi wetu wakuu wa serikali na ni ahadi hii. Sasa kinachosikitisha ni kuona kwamba pamoja na kuwa ni ahadi barabara hii imechukua muda mrefu sasa, lakini kubwa ambalo naliomba ni kwamba inaonekana huyu mjenzi wa hii barabara uwezo wake kidogo una matatizo. Ningeliiomba wizara ikamshughulikia mjezi huyu na ikiwa inawezekana basi ni vyema akafutiwa uwezo wa kuweza kutengeneza barabara hii na baadae akatafutwa mjenzi mwengine, na akaweza kujenga barabara hii na ikakamilika kuliko ambavyo ahadi za kila siku zinavyoendelea.

Mhe. Spika, kati kati hapa nilifuatwa kama kiongozi wa jimbo kwa ajili ya kutoa mashirikiano juu ya ujenzi wa barabara hii, kutokana na ujenzi wa ile ofisi ya walemavu pale ili wale watu watoe mashirikiano na ile barabara iweze kuanza kujengwa, kama ilikuwa ndio kikwazo kwa upande wao. Bahati nzuri niliwafuata wale Ofisi ya Walemavu tukawaomba na tukakubaliana, sasa ikawa ile sababu ambayo ilikuwa wao wanasema kwamba ndio

kikwazo ikawa imekamilika lakini bado tunapigana danedane katika suala zima la ujenzi wa barabara ile. Ningeliomba sasa, kupitia Baraza lako hili tukufu wale wajenzi wanaonekana uwezo wao ni mdogo kwa hiyo, ni jambo jema wakanyang'anywa na barabara ile kupewa watu wengine wakaweza kuijenga na ikakamilika hususan ilivyokuwa fedha zake tayari zipo zimetengwa kwa muda mrefu.

Nikiondoka hapo nakuja katika kijitabu chetu hiki ambapo kuna mambo ambayo nahisi yamesahauliwa. Namuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atusaidie. Nilipokuwa nakiangalia kitabu hiki katika ukurasa wa 48 mapato na matumizi ya shirika. Hapa ninasifu sana kutokana na juhudi kubwa na nzuri ambazo wenzetu Shirika la Meli wamezifanya pamoja na Shirika la Bandari wamekusanya vizuri mno, kiwango ambacho mimi nina hofu hata tukiwa na meli yetu sijui kama tutaweza kufikia kiwango kama hiki. Kwa hivyo, kwa utaratibu huu ningeliomba meli yetu mpya itakapokuja utengenezwe utaratibu mzuri wa kuhakikisha kwamba mapato yatakayokusanywa yawe ya uhakika.

Mhe. Spika, kinachonisikitisha baada ya hapo ni huku katika ukurasa wa 90 mpaka 94. Huku kumezungumziwa suala la meli zilizosajiliwa nchini kupitia *Tanzania Zanzibar International Register of Shipping*. Kuna mtiririko wa meli za nje ambazo idadi yake zinaweza kufika hata 62, zimezungumzwa humu zikiwemo na *turnage* zake, lakini nikiangalia mapato ambayo yako hapa kama ni mapato na matumizi kwa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, sidhani kama haya mapato ya usajili wa meli yatakuwa yameingizwa katika mapato hayo. Sasa kama itakuwa yamo Mhe. Waziri atakapokuja hapa nitamuomba anisaidie na kama hamna basi nitaomba atusaidie maelezo ni kwa nini ikawa mapato hayo hayakutiwa.

Nikiondoka hapo sasa ninakwenda katika suala zima la miradi. Wizara hii ya Miundombinu na Mawasiliano ni wizara moja kubwa sana na ina majukumu na mambo mengi sana, lakini ukiangalia vile vile na idadi ya miradi ambayo inapelekwa katika wizara hii ni mingi. Mimi nahisi kwa mawazo yangu umefika wakati sasa tuangalie uwezekano wa kupunguza baadhi ya miradi ndani ya wizara hii, ili waweze kupewa miradi ambayo inaweza kwenda sambamba kuhusiana na pato halisi la nchi yetu.

Mhe. Spika, leo asubuhi nilikuwa nikimsikiliza hapa Mhe. Waziri wa Fedha alivyokuwa akitoa takwimu zake. Takwimu za ndani katika mwaka 2011 zimetoka kutoka asilimia 106 mpaka tukafikia asilimia 87, lakini tukiangalia asilimia za wahisani sasa kwa mwaka huu pale mwanzo nilikuwa sikusikia vizuri, lakini kwa mwaka huu tuko kwenye asilimia 53. Asilimia hii 53 ya misaada ya wafadhili ni kiwango kidogo sana ina maana wanatufahamisha kwamba tuelekee kujitegemea wenyewe kwa kipato chetu ambacho tunakikusanya.

Sasa ukiangalia kwa mfano, kwa mwaka huu wizara hii ina miradi 10, miradi hii ukiangalia kwa kipato ambacho tunakipata hatuwezi kutimiza miradi yote 10 matokeo yake ndio pale tunakwenda kukamata kila mradi kidogo kidogo na miradi inakuwa haikamiliki. Ningeliomba sana ni bora tukawa na miradi mitatu, minne au mitano lakini ni miradi ambayo itakuwa inatekelezeka na serikali inaweza ikahimili kutimiza miradi hiyo.

Mhe. Spika, baada ya hapo kama nilivyosema mwanzo mimi sina mchango mkubwa sana katika hili isipokuwa kwa kumalizia wajumbe walikuwa na maombi yao kwa hizi taarifa ambazo zinasomwa na Wenyeviti wa Kamati, hususan katika bajeti ukiachilia mbali ile ripoti kubwa ambayo inakuja kwa mwaka mzima. Hizi kamati za kibajeti zinapokuja kutoa ripoti zao wajumbe wanaomba kitengenezwe kitabu maalum ili zile ripori za kamati zote waweze na wao kuzipata na waweze kuzifanyia kazi ili michango yao iweze kuwa mizuri zaidi.

Baada ya maelekezo hayo mimi naunga mkono hotuba ya bajeti ya wizara hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii na mimi nitajitahidi kama nilivyogaiwa mimi na mwenzangu nimgaie vile vile.

Mhe. Spika, mimi naanza kwa kutokuiunga mkono hotuba hii ya bajeti na sitoiunga mkono, nina sababu zangu na nitazieleza. Kwanza natangaza naondoa shilingi katika mshahara wa Mhe. Waziri kwa sababu ameshindwa kusimamia majukumu yake.

Mhe. Spika, nazungumza hivi kuna kilio cha muda mrefu tumekuwa tukikizungumza hapa Barazani kuhusu matendo ya udhalilishaji, vile vile ubadhirifu unaofanywa katika Mamlaka ya Uwanja wa Ndege. Sasa Mhe. Waziri

tumemwambia sana anaitikia lakini mwisho anakiri mwenyewe kwamba Mkurugenzi wake wa Mamlaka ni mkaidi na hasikii. Sasa kama ingelikuwa kuna kubadilishana mawaziri tungelimuomba Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akatuletea Dkt. Harrison Mwakyembe angalau miezi 6 tu katika wizara hii. Naamini haya yaliyomshinda Mhe. Waziri basi Dkt. Mwakyembe angeliyaweza.

Mhe. Spika, kwa sababu ushahidi tumeuona, tuliona kule Tanzania Bara kulivyokuwa kuna matatizo katika Shirika la Bandari, lakini Dkt. Harrison Mwakyembe aliamua kumwambia Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano, mimi Mkurugenzi huyu hanifai, sasa aidha mimi au yeye. Sasa Mhe. Waziri hebu na wewe fanya hivyo, udhalilishaji mpaka waziri mwenyewe anadhalilishwa hapo Kiwanja cha Ndege. Sasa leo Mhe. Spika, bado hapa Mkurugenzi wa Mamlaka anafanya nini. Tumezungumza muda mrefu huyu Mkurugenzi ni Mkurugenzi wa Mamlaka, sio Mkurugenzi wa Kiwanja cha Ndege. Alikuwa akae wizarani kule amwachie Meneja wa Uwanja wa Ndege afanye kazi pale.

Mhe. Spika, tulianza kuzungumza kuhusu suala la kufungwa gari ya Balozi wa Oman, imefungwa mara tatu, mpaka Wizara ya Mambo ya Nje wakaja wakaichukua gari pale, aibu. Lakini leo Mhe. Spika, mpaka wananchi wa kawaida Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali mkewe yumo ndani ya gari, gari imefungwa pale pale. Lakini isitoshe, Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, Mhe. Bihindi Hamad Khamis anakuja kupokea wanamichezo wake amezuiliwa nje. Mhe. Spika, nchi gani iliyokuwa haina nidhamu, haina heshima. Lakini baya zaidi huyo waziri anayetutafutia pesa ambaye pia katika huo Uwanja wa Ndege unaojengwa sasa hivi yeye ndie mhangaikaji mkubwa kutafuta fedha, imefika pahala aibu. Mimi kuna rafiki yangu mmoja yupo Dubai, siku hiyo tupo Dodoma kwenye Bunge la Katiba ananitumia kwenye *whatsapp* gari ya Waziri wa Fedha imefungwa mnyonyoro.

Mhe. Spika, leo hii nchi ina nidhamu gani. Mhe. Spika, langu lile ndio uso wa Zanzibar. Mtu akija pale anatakiwa aone sura ya Zanzibar. Sura ya Zanzibar ndio ile. Mimi nadhani tumeshasema sana na nakuomba sana Mhe. Spika, umuombe sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa sababu tutataka kufanya maamuzi magumu kama walivyosema wenzangu. Tunataka kufanya maamuzi magumu awepo. Kwa sababu kuna maamuzi mengine waziri naamini hawezi kuyatolea ufafanuzi. Lakini tunaamini Kiongozi wa Shughuli za Serikali ambae ndie Kiongozi wa Baraza hili, yeye naamini anaweza akatutolea maamuzi.

Mhe. Spika, tumeona kazi zinazofanywa Uwanja wa Ndege bustani ipo nzuri sana. Mhe. Spika, mimi sina chuki na mtu na ukurugenzi bado anaweza akapewa lakini sehemu nyengine sio pale, kwa sababu pale ameshindwa kazi. Mimi nadhani akipewa ukurugenzi wa Manispaa kwa kweli kazi ingelimfaa sana. Kwa sababu ukiangalia bustani zilizokuwepo Uwanja wa Ndege sasa hivi zinapendeza. Kwa hiyo naamini akipewa ukurugenzi wa Manispaa kule mji wetu utapendeza kwa bustani.

Vile vile hata zile gari ambazo zinapaki maeneo mabaya hasa daladala kule Darajani nafikiri angelikuwa anazifunga tairi siku zote naamini wangelifuata nidhamu. Lakini kwa Uwanja wa Ndege pale sipo. Kwa hiyo Mhe. Spika, Mkurugenzi huyu mimi nafikiri ameshindwa kazi.

Sio hilo tu Mhe. Spika, pia kuna ubadhirifu Mhe. Hija Hassan Hija aliuzungumza na mimi nataka niuzungumze. Katika hili siku zote tunazungumza Serikali haina pesa ubadhirifu upo mwingi. Kuna barua hapa ya tenda ambayo ilikuwa inasema *invitation for quotation* iliyoandikwa tarehe 3/4/2014 na ikatiwa saini na Mkurugenzi wa Mamlaka kwa ajili ya ununuzi wa *x-ray machine*.

Kuna barua vile vile hapa ambayo imeandikwa tarehe 2 mwezi wa 4, barua ya kuomba ile tenda imeandikwa tarehe 3, barua ya kujibu kupokea tenda tarehe 2. Kwa hiyo ina maana kuna mazungumzo yalikwisha kufanyika mwanzo. Mhe. Spika, huo ndio ufisadi wenyewe. Mhe. Spika, ufisadi ni kuzifisidi fedha za umma kwa sababu kuna taratibu za tenda.

Sio hilo tu Mhe. Spika, hapo Uwanja wa Ndege kuna ndugu yetu mmoja amewekeza pale tayari watendaji wa Mamlaka ya Uwanja wa Ndege wamemfuata na tayari kuna pesa wameshachukua, na walimuahidi kwamba *x-ray machine* atasambaza yeye. Sasa baada ya kusikia tenda zimetoka mambo ndio kama haya hadharani.

Mhe. Spika, mimi nadhani kama haya maneno ninayosema sio sahihi nitaomba uunde Kamati Teule iende ikafuatilie kadhia ya ununuzi wa *x-ray machine* waangalie tenda na utaratibu uliopatikana. Vile vile tumfuatilie na yule ambaye

walimchukulia pesa zake. Na leo nasema nikimaliza tu kusema hapa wakamrejeshee pesa zake kabla Kamati ya Baraza haijenda.

Mhe. Spika, sio hilo tu, tunapozungumza vitu sisi hatumwonei mtu choyo. Lakini kuna vitoroli hivi, hivyo ambavyo mnavyoambiwa ukifika pale na gari yako kama hukupeleka kwenye vitoroli vya bosi kubwa basi gari yako inafungwa mnyororo. Mhe. Spika, utaratibu Mkurugenzi wa Mamlaka amepewa mamlaka ya kununua chini ya mamlaka yake si zaidi ya milioni 50. Lakini hapa kuna milioni 120 vimenunuliwa vitoroli. Kwa utaratibu wa kukimbia sheria wananunua leo milioni 40, baada ya mwezi milioni 40, yaani ujanja ujanja mwingi pale Mamlaka ya Uwanja wa Ndege. Sasa hili pia Mhe. Spika, haya ni matendo ambayo hayapendezi.

Pia *x-ray machine* iliyokuwa imeharibika tayari kuna watu tuna taarifa wameshapewa karibu milioni 16 kuna kampuni kutoka Bara. Kwa hiyo ile kazi haijafanyika milioni 16. Sasa fedha zimeshatoka tunaomba zirudishwe halafu baadae tuangalie huu utaratibu wa hii *x-ray machine* uko vipi.

Mhe. Spika, sasa hivi wafanyakazi wanalalamika vikao vya bodi vimekuwa vingi na vikao vyenyewe vinaanza saa nne hadi saa sita na nusu vikao vimemaliza. Sasa mimi nadhani sio jambo zuri sana.

Jengine Mhe. Spika, nilizungumza mapema tokea bajeti ya mwaka juzi na mwaka jana kwamba Mkurugenzi aamue moja. Aidha, awe Mkurugenzi wa Mamlaka ya Uwanja wa Ndege, au aendeleze lile hanga alilolikodi. Mhe. Mwanasheria Mkuu nilim-*quote* vizuri na *hansard* ninayo. Mwaka jana alisema kwamba walipewa agizo juu huko baada ya malalamiko ya Baraza na Mkurugenzi akajikubalisha kwamba ameamua kubakia kwamba ni Mkurugenzi wa Mamlaka lakini hanga amelirejesha.

Mhe. Spika, mimi naomba sana kwanza ni aibu viongozi wa Serikali kudanganywa, mpaka Mwanasheria Mkuu pia kadanganywa. Mhe. Spika, mpaka hii leo majadiliano yote anafanya mwenyewe Mkurugenzi. Ingawa ameliondoa jina lake lakini kampuni amewaachia watu. Lakini Mhe. Spika, hii ndio *conflict of interest.* Mhe. Spika, huwezi kuwa Mkurugezi wa Mamlaka halafu umewekeza hapo hapo. Leo hii kampuni ya *AEROTECH* ambayo Mkurugenzi wa Mamlaka ndio kampuni yake wanadaiwa mpaka na *ZRB.* Leo kweli ataweza kusimamia mapato ya Shirika. Mhe. Spika, mimi nafikiri kuna mambo mengi, hata vile vibanda vinavyojengwa pale kama hujatoa chochote hupati kitu. Mhe. Spika, mimi nina wasiwasi hata hiyo *apron* inayojengwa hapo kama kwamba hizi sio dili za watu tutakwenda vipi.

Kubwa zaidi Mhe. Spika, kuna huyu Mfaransa ambae amekuja kuwekeza katika mradi huu wa kufundisha marubani. Nimezungumza sana suala hili, huyu amefika pahala amekwenda, amepanda, ameshuka mpaka kwa Makamu wa Pili wa Rais ameshafika kikwazo kipo kimoja tu, Mkurugenzi nae anataka kuufanya mradi kama ule. Kuna huyu *captain* Robert m-*South Africa* wa hii kampuni ya *HISCO* msituone tunasema tunajua mengi. Huyu yeye ndio mwenye dili zote na Mkurugenzi. Hayo mambo yote aliyofanya kuhusu ununuzi wa *x-ray machine.*

Sasa hivi Mkurugenzi ameshaanza kutafuta ma-*plot* anataka kuanzisha kiwanja cha kutulia helikopta. Wakati yule Mfaransa anataka kuweka kiwanja cha kufundishia marubani, tena kiwanja chenyewe kipo katika ule ukanda mgumu siku zote watu wanapokufa, ukanda wa Nungwi, ambapo yeye ndege zake zina uwezo mpaka wa kutua baharini. Yakitokezea majanga ana uwezo wa kuruka akaenda pale mara moja kusaidia.

Mhe. Spika, kule Nungwi na kwengineko wakitokezea hata wagonjwa wa *emergency* usiku ana uwezo wa kurusha *charter* yake akawaleta uwanjani wakakimbizwa hospitali, anazuiwa kwa ubinafsi. Hoja zangu hizo ndio zinazonifanya kwa kweli nikose imani kabisa. Maana yake sio kama namchukia mtu ndio maana nikajaribu kupendekeza kwamba ile sehemu ambayo mnahisi ana uwezo nayo basi apelekwe kule naamini mji wetu utakuwa mzuri.

Mhe. Spika, nikiendelea katika mchango wangu hoja zilizobakia ni za kawaida kabisa. Katika suala zima la Jimbo langu la Kwamtipura mimi namshukuru Mhe. Waziri kile kibarabara changu cha Shaurimoyo mpaka Kilimahewa kule wamekijenga robo. Kwa kweli nawashukuru, mtu anapofanya vizuri lazima ashukuriwe. Kwa hiyo naomba kupitia Mfuko wa Barabara wametwambia pesa bado wanazo basi angalau mtumalizie. Tumeangalia takwimu ya sensa kibarabara kile kinatumiwa na wakaazi hawapungui watu 22,000. Kwa hiyo kwa kiasi fulani kibarabara kile pamoja na kwamba nyinyi mmekijenga mmekiona kidogo lakini mimi kimeweza kunisaidia sana.

Mhe. Spika, pia nilikuwa naomba suala la meli. Mhe. Spika, hata mimi nina masikitiko makubwa na lazima Mhe. Waziri aje atupe maelezo ya kutosha, na ndio maana tukataka mpaka Makamu wa Pili wa Rais kesho awepo kwa sababu kuna maamuzi mazito tunataka kuyafanya. Tunaweza tukazuia bajeti kwa mambo ambayo Serikali inaweza ikayatolea maamuzi.

Suala la kuzidishwa idadi ya abiria kutokufuata ile *original* iliyotakiwa. Nadhani hilo suala hata mimi sitokubaliana nalo, nitaungana mkono na wenzangu katika kuhakikisha kwamba suala hili linarekebishwa.

Jengine Mhe. Spika, kule Pemba tumepata malalamiko. Unajua sasa hivi sisi tunatangaza tu *PPP* wafanyabiashara washirikiane na Serikali. Lakini Mhe. Spika, wanapotokea wafanyabiashara kutaka kushirikiana na Serikali hatuwapi *support*. Leo *crane* ya Pemba bandarini imekufa karibu mwaka mmoja na nusu. Leo kuna mzalendo anataka kuwaazima *crane* kwa njia ya kuwakodisha ili wananchi wale waweze kuteremsha mizigo yao kwa utulivu. Mpaka leo Mheshimiwa anaingizwa huku anatolewa huku. Sasa Mhe. Spika, hebu atwambie Mhe. Waziri je, wanapenda wananchi wetu wapate tabu, au ndio hii kazi ya bandari na kazi ya usafiri sasa hivi akitaka mtu mmoja tu ndio yeye hao wengine wote wawe hawana sauti. Mhe. Spika, mimi nafikiri hili kwa kweli sio jambo zuri, naomba tuwatendee haki wenzetu wote ambao wanahitaji kutusaidia.

Pia Mhe. Spika, katika hii *route* ya daladala ya kutoka Bububu mpaka Mnazi Mmoja, wananchi wangu wa Shaurimoyo, Saateni, pamoja na Chimbuni wanalalamika kwamba zile daladala kule inakuwa hazifiki mwisho.

Mhe. Spika, la mwisho kabisa nilikuwa naomba sana kila mtu anasema lake kuhusu suala la Bandari yetu ya Zanzibar. Mimi naomba sasa hivi tunategemea huko mbele uchumi wetu Zanzibar utakuwa kwa haraka, idadi ya mizigo itaongezeka. Kule bandarini kusifanywe miundombinu yoyote, isipokuwa labda yale mabanda yaliyokuwemo yavunjwe ili kuweka kontena *terminal*. Kwa sababu nasikia Serikali ina mpango wa kuyaleta makontena huku Kisauni.

Mhe. Spika, ukiangalia sasa hivi *freight* kutoka Dubai mpaka hapa, meli kutoka Dubai mpaka Bandari ya Mombasa wanalipa dola 1,400, kwenda Dar es Salaam dola 1,700, kuja Zanzibar dola 2,400. Sasa leo Mhe. Spika, ikiwa makontena yatakuja kuwekwa Kisauni basi meli zitachelewa kupakua na kupakia mizigo itasababisha zaidi ucheleweshwaji wa meli.

Mhe. Spika, baada ya hayo naona unaniangalia kwa sababu mimi nilisaidiwa, ili na mimi siku nyengine nije nisaidie. Kwa kweli siungi mkono bajeti hii na nitamuomba sana Mhe. Waziri ajitahidi sana kukubaliana na ushauri wetu kwamba hebu atusaidie tumpate Mkurugenzi ambaye atakayeweza kufanya kazi wananchi wote wakaridhika. Mhe. Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako moja kwa moja nianze na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Zanzibar. Mhe. Spika, katika uwanja ule kuna vijana wetu wamejiajiri kwa kuhudumia ndege za kampuni mbali mbali. Mhe. Spika, kwa masikitiko makubwa hivi karibuni kulitokea tukio la kutuhumiwa kuingizwa dawa za kulevya. Kwa sababu hiyo Mkurugenzi Mkuu kwa kina aliona kuwa amehusika kwa hiyo alizuia kile kitambulisho chake cha kufanyia kazi pale. Kwa hiyo baadhi ya Wazanzibari walinyang'anywa vipande vyao, walikwenda kujitetea. Lakini taarifa niliyopewa na hao wanaohusika wenyewe wanasema kwamba Mkurugenzi Mkuu huyu hakuwarejeshea vitambulisho vyao na hawakuajiriwa tena.

La kusikitisha zaidi alisema Wazanzibari tunajua wanatutia aibu kwa hiyo kuanzia leo asiajiriwe Mzanzibari yeyote kufanya kazi hapa. Vijana hao watatu wanatoka katika Kampuni ya *Auric Air*, wawili katika Kampuni ya *Coastal*, na wawili *ZAT*. Na akaagiza kuwa waagizwe vijana kutoka Mwanza waje waajiriwe.

Mimi nilipopata taarifa hii niliendelea na uchunguzi na taarifa niliyoletewa ni kwamba pamoja na kuwa wanaofanya kazi katika kiwanja cha ndege kile walizungumza na Mkurugenzi abadilishe ule uamuzi wake wa kuwadharau Wazanzibari hakukubali, lakini mwisho wa *Auric Air* tayari wameshaajiriwa vijana wapya wawili kutoka Mwanza.

Mhe. Spika, mimi ni Mzanzibari na Rais wetu Marehemu Mzee Abeid Amani Karume baada ya Mapinduzi alisema tumechoka kuonewa, kudharauliwa na kunyanyaswa. Kitendo hiki cha kuwakataa Wazanzibari na kuwaingiza watu kutoka Mwanza ni kitendo kinakwenda kiukabila na mimi napingana nacho moja kwa moja. Kwa hili namuomba kwa sababu najua Mhe. Waziri huyu hamuwezi wala hathaminiwi na Mkurugenzi huyu. Kwa hili namuomba Mhe.

Rais moja kwa moja kuwa nchi hii hatutaki ubaguzi, ni nchi yetu wenyewe, huyu Mkurugenzi ama awajibike au arekebishe makosa yake. Na Mhe. Waziri akitaka majina nitampa moja baada ya moja na wenyewe atakutana nao. Hilo ni moja.

La pili Mhe. Spika, nashukuru kuwa Serikali kujitahidi kutafuta wafadhili na kupata matengenezo ya barabara za vijijini katika Mkoa wa Kaskazini Pemba, barabara ambazo zilifadhiliwa na Wamarekani katika mfuko wao wa Changamoto ya *Millenium*. Katika barabara hizo tulibahatika kupata barabara ya Bahanasa, Daya, Makongeni na Uondwe yenye urefu wa kilomita 13.6. Mhe. Spika, katika utengenezaji wa barabara hiyo kampuni hii ya *H Young* ambayo ndio iliyokuwa ikitengeneza barabara, ilibidi ichimbe kifusi katika sehemu ya Mto Mkuu. Na ili magari yao makubwa kufika kule ilibidi ile barabara iliyokuwepo iparwe na halafu wakachimbe hicho kifusi.

Mhe. Spika, kabla ya hapo barabara hii ilikwisha kutumia jumla ya shilingi milioni 70 kutoka ufadhili wa *TASAF* na tayari ilikwisha kutiwa kifusi, lakini kwa sababu hiyo kifusi kile kiliondolewa moja kwa moja kwa ahadi kuwa baada ya kumaliza kazi kifusi kile kitarejeshwa. Nasikitika mpaka leo barabara zimemaliza na mradi umeshakabidhiwa na Mhe. Rais ameshazindua rasmi barabara ile imeachwa kama ilivyo imekufa na imeshagharimu fedha nyingi. Mhe. Waziri analijua hili na yeye mwenyewe alisema kuwa atalishughulikia. Naomba Mhe. Waziri anipe jibu kuhusu barabara hii ya Bagamoyo/Matuuni/Kele itafanyiwa marekebisho lini wakati ilivurugwa kutoka hali iliyokuwa kutokana na matengenezo ya barabara hizo nilizozitaja.

La tatu, kwa ufupi Mhe. Spika, tumeona kuwa kuna matengenezo ya meli mpya ya mizigo na abiria ambayo inatengenezwa kwa mfuko wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Katika maelezo meli hii kutia saini tu baina ya Kampuni na Serikali ilikuwa ni tarehe 10/07/2013 ni kiasi mwaka mzima hivi sasa. Kilichoendelea ni kukamilisha kazi za usanifu na uandaaji wa michoro ya meli hiyo. Jengine ni uzinduzi wa zoezi la ukataji wa vyuma vya meli hiyo yaani *steel cutting* na yalikuwa ni mwezi wa Machi, 2014 hivi juzi. Na kwa kazi ya utiaji wa mkuku inakadiriwa kufanyika ifikapo 2014 ambayo ndio mwaka huu na ujenzi unatarajiwa kumalizika 2015.

Mhe. Spika, meli hii Serikali kwa makusudi iliamua kuitengeneza kutokana na athari kubwa zinazojitokeza. Kulizama watu wakafa msiba mkubwa na Serikali ikaamua kufanya hivi. Lakini kwa utaratibu huu unaoelezwa hapa mimi sina tamaa kabisa kuwa meli hii itamalizika kwa karibuni. Naamini mwaka wa uchaguzi 2015 utapita na huko tunakokwenda huenda mambo haya yakazidi kuchelewa. Ninavyoomba Mhe. Waziri anapotueleza atueleze kitu tufahamu. Angesema tu kazi inaendelea na ikimalizika mtaambiwa, kuliko kutudanganya tukatia tamaa wakati meli hii haiwezi kumalizika kwa hivi karibuni. Mhe. Spika, tunajua kuwa bado athari zinaendelea karibuni hivi kulitokea wimbi na watu wakazama, kwa hiyo umuhimu wa meli hii ni lazima upewe kipaumbele.

Mhe. Spika, jengine ningeomba kuzungumza kuhusu bandari. Mhe. Spika, tumeshatimiza miaka 50 tokea Mapinduzi. Tulikuwa watu kiasi laki tatu na kidogo sasa ni milioni moja na laki tatu na zaidi kila kitu kimeongezeka. Tulikuwa tukizungumza sana kuwa kwa hali ilivyo kwa sababu usafiri wetu mkubwa ni wa kwenye bahari ni lazima na bandari zetu ziongezeke.

Mhe. Spika, sioni sababu kwa miaka 50 hii na Serikali inaona na inajua umuhimu wake mpaka leo Zanzibar ikawa bado kuna bandari moja na kushindwa kuitengeneza bandari ile ya Mkokotoni ikafanya kazi ipasavyo ili tatizo la usafiri likaondoka. Tunakaa tu, tunapanga tu bandari ile hivi sasa tunajua inatumika katika mambo ambayo si mazuri na hata ukusanyaji wake wa fedha hasa kwa siku za Jumamosi na Jumapili haupo kabisa.

Kwa hiyo ningelimuomba Mhe. Waziri kwa maslahi ya nchi hii na kukuza mfuko wa taifa kwa kutumia bandari zetu, ile Bandari ya Mkokotoni ipewe kipaumbele angalau kwa Zanzibar napo kuwepo na bandari mbili. Inasikitisha kuwa Pemba zipo tatu kwa nini Zanzibar iwepo moja tu.

Mhe. Spika, jengine wakati watu wanaongezeka na huduma zinaongezeka ni lazima na sisi tubadilike. Tunapochukua wizara ni lazima tuwe na mipango ambayo ni ya baadae ili kuweza kulingana na hali inavyobadilika. Inasikitisha sana kuwa mpaka leo Pemba Bandari ya Mkoani, Bandari ya Wete, na Bandari ya Wesha bado zipo katika hali ile ile ambayo si ya kuridhisha katika kutoa huduma. Kwa hiyo ningelimuomba Mhe. Waziri anieleze yeye mwenyewe kaweka mpango gani endelevu ambao utahakikisha kuwa bandari zetu zitakuzwa na kuimarishwa ili ziweze kufanya kazi ipasavyo.

Mhe. Spika, nikiendelea nirudi katika bandari yetu kubwa iliyopo Malindi. Kwanza, nitoe pongezi kwa Sheikh Said Salim Bakhressa kwa namna bandari alivyoibadilisha.

Mhe. Spika: Mhe. Salim Abdalla Hamad tunakushukuru lakini tunakuomba radhi kwa sababu ya muda mchache. Waheshimiwa Wajumbe, niendelee kuwaomba radhi wachangiaji walioomba walikuwa wengi hatukuweza kumudu kuwasikiliza wote. Tulipata kama maombi 41 hadi kesho tukimaliza safu ya mawaziri itakuwa tumemudu kuwasikiliza jumla ya Waheshimiwa Wajumbe 30. Nafikiri itoshe kwamba tumejitahidi lakini wote hatukuweza kuwasikiliza. Na kama nilivyosema mapema basi wengine wataomba kutoa michango yao kwa maandishi.

Waheshimiwa Wajumbe, kesho penye majaaliwa tukiingia itakuwa tunawasikiliza safu ya mawaziri ambao ni pamoja na Mhe. Machano Othman Said, Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum, Mhe. Waziri wa Fedha, na hatimae Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano. Baada ya hapo tutamsikiliza Mhe. Waziri kumalizia majumuisho.

Basi baada ya machache hayo Waheshimiwa Wajumbe, sasa niakhirishe kikao hichi hadi kesho tarehe 13/06/2014 saa 3:00 za asubuhi ili tuweze kumaliza shughuli yetu. Ahsanteni.

(Saa 1:48 usiku Baraza liliakhirishwa mpaka tarehe 13/06/2014 saa 3:00 asubuhi)